

**KUCHUNGUZA DHANA ZILIZOBEBWA NA WAHUSIKA NA  
ZINAVYOLANDANA NA MAJINA YAO: UCHUNGUZI KATIKA RIWAYA  
YA KIU NA KIU YA HAKI**

**AMOUR RASHID ALI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA, IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA  
KUPATIYA SHAHADA YA UZAMILI YA (M.A) KISWAHILI FASIHI YA  
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2015**

## UTHIBITISHI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii itwayo:

***Kuchunguza Dhana Zilizobebwa na Wahusika na Zinavyolandana na Majina yao:***

***Uchunguzi katika Riwaya ya Kiu na Kiu ya Haki***, na kupendekeza ikubaliwe na

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya

Uzamili katika (M.A) Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

---

Profesa, Emmanuel Mbogo

**(Msimamizi)**

---

Tarehe

**HAKI MILIKI**

Haki ya kunakili tasnifu hii inalindwa na mkataba wa Berne, sheria ya haki ya kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali za kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya tasnifu hii, kwa ajili ya utafiti, kujisomea, au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili, Utafiti na Uchapaji kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

**IKIRARI**

Mimi, **Amour Rashid Ali**, nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba kwa haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Digirii yoyote.

---

Saini

---

Tarehe

**TABARUKU**

Nabaruku kazi hii kwa mke wangu mpenzi Bi. Maryam Shaali na watoto wetu wapenzi Ahlam, Asmaa na Adh-hariyu, namuomba Mwenyezi Mungu awakuze mkiwa na afya njema na awatunuku zawadi ya elimu (Amin).

## SHUKURANI

Kwanza kabisa, kabla sijasema neno lolote, ninapenda nitoe shukurani zangu zisizo na ukomo kwa ALLAH SUBHANAHU WATAALAH kwa kunijaalia afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu, kunipa nguvu, uwezo, akili, busara na maarifa katika muda wote wa masomo yangu ya Uzamili. Ninasema, kwa unyenyekevu, Alhamdulillah Rabbillaalamina.

Pili, ninawashukuru sana wazazi wangu, kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha na kunifunza maisha ya dunia na Akhera. Vile vile, shukurani za pekee ni za mke wangu kipenzi, Bi Maryam Shaali Ame kwa uvumilivu wake, huruma na kunitia moyo katika kuendeleza masomo yangu. Pia, kaka yangu mpenzi, Dkt. Hassan Rashid na dada yangu Bi Maryam Rashid, hawa walikuwa na mchango mkubwa mpaka nikafika hapa nilipo.

Tatu, napenda kumshukuru kwa dhati msimamizi wangu Prof. Emmanuel Mbogo kwa kunilea kitaaluma na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili. Sina neno linalofaa kutoa shukrani kwake bali namuombea afya njema na maisha marefu ili aendelee kutoa msaada wa kitaaluma kwa wanafunzi wanaohitaji maarifa zaidi.

Nne, napenda kumshukuru Prof. T.Y.S.M.Sengo kwa msaada wake mkubwa sana wa kitaaluma darasani na nikiwa nje ya darasa. Vile vile, napenda kumshukuru Mw: Bakari Kombo Bakari kwa ushauri wake nzuri alionipa wakati wote wa masomo.

Pia, napenda nimshukuru kwa hali ya pekee Mratibu wangu kazini Bi Isha Bakar Ali kwa kunihimiza, kunishauri na kunipa moyo kuhusu masomo yangu.

Mwisho shukurani zangu ziwaendee wale wote walioungana na mimi katika harakati za kufanikisha masomo yangu. Hapa nitawataja ingawa naamini siwezi kuwamaliza, hata hivyo, miongonimwao ni Bw. Ali Mussa Faki, Bw. Ali H. Mwadini, Bi. Kijakazi Saidi Omar, Mw. Mohammed Omar, Bw. Hemed Zatia, michango yao ilinisaidia sana kufanikisha kazi yangu hii. ninawashukuru ndugu zangu na wanachuo wenzangu wote, walioshiriki moja kwa moja na kwa namna yoyote nyingine, katika kuikamilisha kazi hii.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu **kuchunguza dhana zilizobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao katika riwaya ya *Kiu na Kiu ya Haki***. Ili kufikia lengo, mtafiti alichunguza na kubainisha wahusika, pia alichunguza mlandano wa wahusika kupitia mbinu mbali mbali na alichambua dhamira mbali mbali zilizobebwa na wahusika hao na jinsi zinavyolandana na majina yao katika riwaya teuliwa. Utafiti huu ulitumia mbinu ya maktabani. Riwaya teuliwa ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya malengo maalumu. Aidha, data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa mbinu ya kimaelezo kutoka katika riwaya teuliwa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya sosholojia na nadharia ya mwitiko wa msomaji. Utafiti huu uligundua kuwa, kazi hizo teuliwa zimetumia wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Pia, utafiti umegundua kuwa, waandishi wa riwaya hizo teuliwa wametumia mbinu mbali mbali za kuwasawiri wahusika na kuwafanya walandane na majina yao. Mbinu hizo ni pamoja na mbinu ya majazi au majina, kimaelezi, kidrama kuwatumia wahusika wengine, ulinganuzi na usambamba na uzungumzi nafsi wa ndani. Pia, utafiti umegundua kuwa, dhamira katika riwaya teuliwa zimelandana na majina ya wahusika. Dhamira hizo ni pamoja na umasikini, wizi na ujambazi, utamaduni, dhamira ya malezi, dhamira ya ujirani, dhamira ya mapenzi, umuhimu wa elimu, nakadhalika.



## YALIYOMO

<b>UTHIBITISHI</b> .....	<b>ii</b>
<b>HAKI MILIKI</b> .....	<b>iii</b>
<b>IKIRARI</b> .....	<b>iv</b>
<b>TABARUKU</b> .....	<b>v</b>
<b>SHUKURANI</b> .....	<b>vi</b>
<b>IKISIRI</b> .....	<b>viii</b>
<b>YALIYOMO</b> .....	<b>ix</b>
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	<b>1</b>
<b>1.0 UTANGULIZI WA JUMLA</b> .....	<b>1</b>
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	3
1.2 Tatizo la Utafiti .....	5
1.3 Lengo la Utafiti .....	6
1.3.1 Lengo kuu la Utafiti.....	6
1.3.2 Madhumuni Mahususi ya Utafiti huu ni: .....	6
1.3.3 Maswali ya Utafiti .....	6
1.4 Umuhimu wa Utafiti.....	6
1.5 Mipaka ya Utafiti.....	7
1.6 Vikwazo vya Utafiti.....	7
1.7 Utatuzi wa Vikwazo .....	7
1.8 Hitimisho.....	8
<b>SURA YA PILI</b> .....	<b>9</b>
<b>2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA ....</b>	<b>9</b>
2.1 Utangulizi.....	9
2.2 Kazi Tangulizi .....	9
2.3 Dhana ya Wahusika .....	9

2.4	Aina za Wahusika.....	12
2.4.1	Wahusika wa Miraba Minne na Wahusika wa Mraba Mmoja.....	13
2.5	Njia Nyingine za Kuwabainisha Wahusika .....	15
2.5.1	Mhusika wa Kijadi.....	16
2.5.2	Mhusika wa Kimuundo na Kimtindo .....	16
2.5.2.1	Mhusika wa Kiuamilifu .....	16
2.5.2.2	Mhusika wa Kiishara .....	17
2.5.2.3	Wahusika wa Kinjozi.....	17
2.5.2.4	Mhusika wa Kihalisi.....	17
2.5.2.4.1	Mhusika wa Mapinduzi.....	18
2.5.2.4.2	Mhusika wa Kisaikolojia.....	18
2.5.2.4.3	Mhusika wa Kidhanaishi.....	18
2.6	Mbinu za Usawiri wa Wahusika .....	19
2.6.1	Mbinu ya Kimaelezi .....	20
2.6.2	Mbinu ya Kidrama.....	21
2.6.3	Mbinu ya Uzungumzi Nafsi wa Ndani .....	21
2.6.4	Mbinu ya Kuwatumia Wahusika Wengine .....	22
2.6.5	Mbinu ya Ulinganuzi na Usambamba .....	22
2.6.6	Mbinu ya Majazi au Matumizi ya Majina.....	23
2.7	Kazi Tangulizi Kuhusu Uhakiki wa Wahusika.....	25
2.8	Dhana ya Dhamira .....	30
2.9	Uhusiano kati ya Fani na Maudhui.....	31
2.10	Mkabala wa Kinadharia .....	32
2.10.1	Nadharia ya Sosholojia .....	33
2.10.2	Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.....	33
2.11	Pengo la Utafiti.....	34

2.12	Hitimisho.....	35
<b>SURA YA TATU.....</b>		<b>36</b>
<b>3.0</b>	<b>MBINU ZA UTAFITI .....</b>	<b>36</b>
3.1	Utangulizi.....	36
3.2	Eneo la utafiti .....	36
3.3	Muundo wa Utafiti.....	36
3.4	Uteuzi wa Watafitiwa .....	36
3.5	Usampulishaji.....	37
3.6	Mbinu za Kukusanyia Data.....	38
3.7	Mbinu ya maktabani .....	38
3.8	Vifaa vya Utafiti.....	38
3.9	Hitimisho.....	39
<b>SURA YA NNE.....</b>		<b>40</b>
<b>4.0</b>	<b>UCHAMBUZI WA DATA .....</b>	<b>40</b>
4.1	Utangulizi.....	40
4.2	Ubainishaji wa Wahusika katika Riwaya ya <i>Kiu</i> .....	40
4.2.1.	Wahusika Wakuu.....	40
4.2.1.1	Bahati .....	40
4.2.1.2	Idi.....	41
4.2.1.3	Mwinyi.....	42
4.3	Wahusika Wasaidizi .....	42
4.3.1	Cheusi .....	42
4.3.2	Mwajuma .....	43
4.4	Wahusika Wajenzi katika Riwaya ya <i>Kiu</i> .....	45
4.4.1	Jaku .....	45
4.4.2	Kidawa .....	45

4.4.3	Tatu.....	45
4.4.4	Makame.....	46
4.4.5	Ali.....	46
4.4.6	Bi Mvita.....	47
4.4.7	Sihaba.....	47
4.4.8	Majirani.....	48
4.4.9	Bi Somo.....	48
4.4.10	Binti Songoro.....	48
4.4.11	Binti Jaku.....	49
4.4.12	Hadija.....	49
4.4.13	Baraka.....	49
4.4.14	Muuza Samaki.....	49
4.4.15	Awadhi.....	50
4.4.16	Mcha.....	50
4.4.17	Rehema binti Mwinyi.....	51
4.4.18	Rehema.....	51
4.5	Ubainishaji wa Wahusika katika Riwaya ya <i>Kiu ya Haki</i> .....	52
4.5.1	Wahusika Wakuu katika <i>Kiu ya Haki</i> .....	52
4.5.1.1	Mzee Toboa.....	52
4.5.1.2	Sikujua.....	53
4.5.2	Wahusika Wasaidizi katika Riwaya ya Kiu ya Haki.....	54
4.5.2.1	Pondamali.....	54
4.5.2.2	Mke wa Sikujua.....	55
4.5.2.3	Mzee Fundisha.....	55
4.5.2.4	Mama Fundisha.....	56
4.5.2.5	Inspekta Paukwa.....	56

4.5.3	Wahusika Wajenzi katika ya Kiu ya Haki .....	57
4.5.3.1	Jaji Pwagu .....	57
4.5.3.2	Jaji Pwaguzi .....	58
4.5.3.3	Mtayaona.....	58
4.5.3.4	Utakunywa .....	58
4.5.3.5	Somba .....	59
4.5.3.6	Killa .....	59
4.5.3.7	Kazamoyo .....	59
4.5.3.8	Swalehe .....	60
4.6	Kuchambua Mlandano wa Majina ya Wahusika katika Riwaya Teuliwa ...	60
4.6.1	Mbinu ya Uzungumzi Nafsi wa Ndani .....	60
4.6.2	Mbinu ya Kimaelezi .....	69
4.6.3	Mbinu ya Ulinganuzi na Usambamba .....	72
4.6.4	Mbinu ya Majazi au Matumizi ya Majina.....	74
4.6.4.1	Bahati .....	75
4.6.4.2	Idi.....	76
4.6.4.3	Bi Mvita .....	76
4.6.4.4	Sheikh Baraka .....	77
4.6.4.5	Cheusi .....	78
4.6.4.6	Mzee Toboa.....	79
4.6.4.7	Sikujua .....	80
4.6.4.8	Pondamali.....	81
4.6.4.9	Mke wa Sikujua.....	81
4.6.4.10	Mama Asha .....	82
4.6.4.11	Mzee Fundisha.....	82
4.6.4.12	Mama Fundisha .....	83

4.6.4.13 Swalehe .....	84
4.6.4.14 Inspekta Paukwa .....	84
4.6.4.15 Jaji Pwagu .....	85
4.6.4.16 Inspekta Pwaguzi .....	85
4.6.4.17 Wakili Mtayaona .....	86
4.6.4.18 Jaji Utakunywa .....	87
4.5.4.19 Somba .....	87
4.6.4.20 Killa .....	88
4.6.4.21 Kazamoyo .....	88
4.6.5 Mbinu ya Kuwatumia Wahusika Wengine .....	89
4.6.6 Mbinu ya Kidrama .....	91
4.7 Dhamira Zinazojengwa na Wahusika wa <i>Kiu</i> na jinsi Zinavyolandana na Majina yao .....	95
4.7.1 Dhamira ya mapenzi .....	96
4.7.2 Dhamira ya Utamaduni .....	98
4.7.3 Dhamira ya Malezi .....	100
4.7.4 Dhamira ya Ujirani .....	101
4.7.5 Dhamira ya Ulevi .....	103
4.7.6 Dhamira ya Umasikini .....	105
4.7.7 Dhamira ya Ujasiri .....	107
4.8 Dhamira Zinazojengwa na Wahusika wa <i>Kiu ya Haki</i> na jinsi Zinavyolandana na Majina Yao .....	108
4.8.1 Dhamira ya Haki .....	109
4.8.2 Dhamira ya Rushwa .....	112
4.8.3 Dhamira ya Ujambazi .....	113
4.8.4 Dhamira ya Siri .....	115

4.8.5	Dhamira ya Umuhimu wa Elimu.....	116
4.8.6	Dhamira ya Ukiukwaji wa Sheria.....	118
4.9	Hitimisho.....	118
<b>SURA YA TANO.....</b>		<b>119</b>
<b>5.0</b>	<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>119</b>
5.1	Utangulizi.....	119
5.2	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	119
5.2.1	Dhumuni la kwanza .....	120
5.2.2	Dhumuni la Pili .....	121
5.2.3	Dhumuni la Tatu.....	121
5.3	Mapendekezo ya Utafiti.....	125
5.3.1	Kwa Watafiti Wengine .....	125
5.3.2	Kwa Watunzi wa Fasihi.....	125
5.3.3	Kwa serikali .....	126
<b>MAREJELEO .....</b>		<b>127</b>

## VIFUPISHO

TUKI	Taasisi ya Ukuzaji Kiswahi
BAKIZA	Barza la kukuza Kiswahili Zanzibar
UDA	Usafiri Dar Es Salaam
OUP	Oxford University Press
LTD	Limited
DKT	Daktari
Bi	Bibi
Prof.	Profesa
Bw	Bwana



## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

Utafiti huu unahusu kuchunguza dhana zilizobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao katika riwaya ya *Kiu* na *Kiu ya Haki*. Utafiti una sura tano, sura ya kwanza inaelezea mambo ya msingi ya utangulizi. Mambo hayo ni utangulizi wa mada, mada iliyotafitiwa, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia teti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, sababu zilizomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu, vikwazo vya utafiti na namna vikwazo hivyo vilivyotatuliwa. Aidha, sura ya pili inaelezea utafiti wa kazi zilizosomwa na mtafiti zinazohusiana na mada iliyotafitiwa. Aidha, sura hiyo inaelezea nadharia zinazomuongoza mtafiti katika utafiti huu. Pia, sura imemaliza kwa kuonesha pengo la utafiti. Sura ya tatu imeelezea mbinu zilizotumika kukusanyia data na kuzichambua. Mbinu hizo ni pamoja na mbinu za maktabani, vitabu lengwa, vilivyoteuliwa ni riwaya za *Kiu* na *Kiu ya Haki*. Uchambuzi wa data ulifanywa kwa njia ya maelezo. Sura ya nne imeshughulikia uchambuzi wa data zilizokusanywa na mtafiti na sura ya tano inaelezea kwa muhtasari matokeo ya utafiti huu pamoja na mapendekezo.

Riwaya ya Kiswahili ni moja kati ya tanzu za karibuni ambazo zimewahi kushughulikiwa na waandishi wa kazi za fasihi. Riwaya hizo zimekuwa na mbinu za kibunilizi ambazo husaniwa na mwandishi ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Moja kati ya kipengele muhimu cha fani kinachotumiwa na waandishi wa kazi za fasihi, riwaya ikiwamo ni usawiri wa wahusika.

Kwa mujibu wa Senkoro (1982), wahusika ni watu, ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu, katika kazi za fasihi.

Katika ngano kwa mfano, kuna matumizi maalumu ya wahusika. Humo tunakutana na wanyama, wadudu, mimea, mashetani, miungu na viumbe wengine wakiwa ndio wahusika wakuu wa ngano hizo. Aghalabu hadithi fupi na ngano huwachukulia wahusika wake katika kiwango cha jumla jumla cha kuwakilisha tabia na matendo. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), wahusika wanaweza kuwekwa katika matapo makuu matatu; wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Mtafiti ametumia kigezo hiki katika kuchambua data za wahusika katika riwaya teuliwa.

Wahusika wakuu huwa ni nguzo na mwega kwa mwandishi wa kazi ya fasihi. Wahusika hawa ndio wanaobebeshwa majukumu makubwa ya kazi ya sanaa, ambapo kupitia kwao dhamira kuu hujitokeza. Wahusika wasaidizi hutumiwa na mwandishi kwa lengo la kuwasaidia wahusika wakuu ili kusawiri vyema malengo ya kazi yake. Wahusika wajenzi hutumiwa kuwajenga wahusika wasaidizi na wahusika wakuu ili kufanikisha lengo la msanii katika kazi yake.

Aidha, katika utafiti huu kumeelezwa mlandano wa wahusika kupitia mbali mbali. Mtafiti alizingatia mbinu hizo kama zilivyoielezwa na Wamitila (2002),: mbinu ya kimaelezi, kidrama, ulinganuzi na usambamba, uzungumzi nafsi wa ndani, kuwatumia wahusika wengine na matumizi ya majina au majazi.

### **1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Wahusika katika kazi za fasihi ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili wahusika ni binadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi, na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda. Wahusika huweza kutambulishwa pia na maelezo ya mhusika au msimulizi (Wamitila, 2002:18).

Nyenyembe (1996), anafasili wahusika katika kazi ya sanaa itumiayo lugha ni watu, wanyama, vitu nakadhalika. Wahusika hao kimsingi hujengwa kisanaa na mwandishi au fanani (msanii), ili aweze kukidhi na kuwakilisha dhana mbali mbali za maisha katika jamii.

Nao Nyangwine na Masebo (2006), wanafafanua kuwa, wahusika ni viumbe ambao hutumiwa na msanii katika mtiririko wa vitukio kueleza kisa chake. Wahusika hawa waweza kuwa ni watu, miti, wadudu, mizimu, misitu na wanyama. Wahusika huwa ni viumbe wanaotenda na kutendewa. Wanatumia na msanii kusimamia hali mbali mbali za binadamu katika jamii wanamoishi.

Wahusika wanazungumza na huzungumziwa. Hawa ndio uti wa mgongo wa fani ya fasihi. Bila wahusika mtiririko wa vitukio hukosa pahala pa kujishikilia. Wahusika ni viumbe maalumu wa mtunzi kwa vile ndio wanaotumiwa kutoa picha au kuwasilisha mawazo na fikra zake kwa jamii inayowakilishwa na wahusika hao.

Wahusika katika kazi ya fasihi ni uti wa mgongo wa kazi hiyo, bila ya uwepo wa wahusika hakuna fasihi kwani msanii anapoandika kazi yake huwatumia wahusika wake kwa mbinu kama za kielimu, kiuwezo, kimajukumu, kimavazi, na sifa nyengine nyingi ambazo kwazo huwabebesha wahusika wake kusawiri malengo ya kazi yake. Mbinu hizo huweza kujitokeza kwa ishara za majina yao.

Katika kujadili suala la wahusika, Wamitila (2002), anaeleza kwamba, kuna wahusika vielelezo ambao hawabadiliki na kupewa majina ambayo yanaafikiana na matendo pamoja na tabia zao. Majina ya wahusika hawa huwa kama kielekezi na kifupisho cha wasifu wao. Aidha, Kyando (2012) anaona kuwa wahusika hupewa majina kutegemea maumbile, tabia, kazi, mazingira, kielimu na namna ya kuzaliwa kwao. Anaeleza kwamba, majina hayo hutumia mbinu ya majazi.

Ingawa Kyando alitoa mawazo yaliyohusiana na jinsi ya kuwasawiri wahusika majina yao kwa kutumia mbinu ya majazi, hata hivyo, mtafiti aliona kuwa wahusika wanaweza kupewa majina kwa kutumia mbinu nyengine kadhaa na si ile ya majazi tu. Hivyo mtafiti alichagua kazi teuliwa ili kuchunguza ukweli wa dhana hii.

Sababu nyengine iliyomsukuma mtafiti ni kuwa baada ya kusoma tafiti nyingi kuhusu wahusika aligundua kwamba kazi za *Kiu* na *Kiu ya Haki* hazijawahi kufanyiwa utafiti katika uwanja wa kulandana kwa majina ya wahusika. Aidha mtafiti alisukumwa na kutaka kuona kuwa waandishi wa kazi hizi teuliwa wamemudu kuwalandanisha wahusika hasa kwa kuzingatia kuwa riwaya hizi zimetoutiana katika vipindi vyao vya uandishi kwa miaka kumi, pamoja na

mandhari zao zilizotumika kusanii kazi hizo. Hivyo mtafiti aliamua kufanya utafiti huu ili kuziba pengo la kitaaluma.

## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Mwandishi wa kazi ya fasihi huweza kutumia njia kadhaa tofauti katika kusawiri wahusika wake. Msanii ana uhuru sio tu wa kuwatumia wahusika wa aina fulani, bali wa kuiteuwa namna ya kuwawasilisha wahusika wenyewe na kuwalandanisha na majina yao. Kama wasomaji na wahakiki wa fasihi tunategemea sifa kadhaa za kuwaelewa wahusika: maumbile yao, mienendo na tabia zao, lugha zao, vionjo vyao, uhusiano wao na wahusika wengine, hisia zao kwao wenyewe, mazingira na mandhari yao, jamii yao nakadhalika (Wamitila, 2002).

Riwaya ya *Kiu* ya Mohamed S. Mohamed (1975), na *Kiu ya Haki* ya Zainab M. Mwanga (2004), ni miongoni mwa riwaya za Kiswahili ambazo ni maarufu sana katika jamii ya Tanzania na zinazoakisi jamii hiyo kwa kutumia wahusika wake kuiakisi jamii ya Tanzania na Afrika kwa ujumla. Watafiti kama vile Kyando (2012), Wafula (1999), Omar (2011), na Kenan (2007), wamewahi kufanya utafiti wa wahusika katika kazi mbali mbali za fasihi. Pamoja na umaarufu wa kazi hizi za fasihi, hadi sasa hakuna utafiti wa kina uliofanyika kulenga kuchunguza jinsi wahusika wanavyolandana na majina yao.

Hivyo, mtafiti ameona upo umuhimu wa kufanya utafiti ili, kuchunguza wahusika wanavyolandana na majina yao, ili kuziba pengo hili la kitaaluma katika uwanja huu wa Fasihi ya Kiswahili.

### **1.3 Lengo la Utafiti**

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi kama ifuatavyo:

#### **1.3.1 Lengo kuu la Utafiti**

Utafiti huu una lengo la kuchunguza dhana zilizobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao katika riwaya ya *Kiu na Kiu ya Haki*.

#### **1.3.2 Madhumuni Mahususi ya Utafiti huu ni:**

- i. Kubainisha wahusika waliotumika katika riwaya ya *Kiu na Kiu ya Haki*
- ii. Kuchambua mlandano wa majina ya wahusika katika riwaya teuliwa.
- iii. Kuchambua dhamira zinazobebwa na wahusika hao na jinsi zinavyolandana na majina ya wahusika wa riwaya teuliwa.

#### **1.3.3 Maswali ya Utafiti**

- i. Ni wahusika gani waliotumika katika riwaya teuliwa?
- ii. Je, kuna mlandano wa majina ya wahusika katika riwaya teuliwa?
- iii. Ni dhamira zipi zinazobebwa na wahusika hao na jinsi zinavyolandana na majina ya wahusika wa riwaya teuliwa?

### **1.4 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu una umuhimu mkubwa katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili, hivyo utafiti huu una umuhimu kama ifuatavyo:

Kwa upande wa utafiti huu utawasaidia wanafunzi, walimu, wahadhiri na wasomaji wa kawaida wa kazi za fasihi, hivyo utakuwa ni marejeleo muhimu sana katika kazi zao. Pia utaikuza dhana ya kulandana kiutamaduni kupitia kazi za fasihi.

### **1.5 Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu umejikita kuchunguza wahusika wa riwaya za *Kiu* na *Kiu ya Haki* na namna wahusika hao wanavyolandana na majina yao. Uchunguzi huu umeongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Sosholojia. Nadharia hizi ni muhimu sana katika kutathmini na kuihukumu kazi ya fasihi. Mbinu iliyotumika ni ya maktabani. Aidha, data zimekusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya maelezo. Hivyo utafiti huu haukushughulikia vitabu vyengine vya riwaya jinsi wasanii wa vitabu hivyo walivyoweza kuwalandanisha wahusika na majina yao. Aidha, utafiti huu haukutumia nadharia nyengine za kifasihi katika kuilinda kazi hii.

### **1.6 Vikwazo vya Utafiti**

Uhaba wa fedha kwa ajili ya shughuli nzima ya utafiti ni kikwazo kilichomkwaza mtafiti. Pia, mtafiti alikabilwa na ugumu wa kupata marejeleo ya kazi mbali mbali zinazohusina na utafiti huu. Hali hii imetokana na kwamba, hapa kisiwani Pemba ambapo mtafiti amefanyia utafiti wake hapakuwa na maktaba yenye utoshelevu wa marejeo yanayohusiana na mada yetu. Vile vile, kwa vile mtafiti ni muajiriwa na utafiti huu umefanyika wakati wa kazi, hivyo, ilikuwa ni vigumu mtafiti kufuata marejeo katika maeneo mengine nje ya kisiwa hiki.

### **1.7 Utatuzi wa Vikwazo**

Vikwazo vilivyomkumba mtafiti vilitatuliwa kwa kutafuta marejeo katika mtanadao wa intaneti ili kutatua tatizo hili la marejeo. Pia, mtafiti aliwafuata ndugu, jamaa na juhudi zake binafsi ili kupata fedha za kukidhi gharama ya utafiti. Aidha, kuhusu suala la ruhusa kazini, mtafiti aliomba ruhusa ili kupata muda wa kufanya utafiti.

### **1.8 Hitimisho**

Sura imeonesha uwasilishaji wa vipengele vya kiutangulizi vinavyotoa picha kamili ya nini kinataka kutafitiwa. Hili linathibitika kupitia vipengele vya mada ya utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, madhumuni mahsusi ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vyengine ni umuhimu wa utafiti na mipaka yake.



## **SURA YA PILI**

### **2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Katika sura hii mtafiti amejadili maana ya kazi tangulizi, dhana ya dhamira, mbinu mbali mbali za kuwasawiri wahusika pamoja na nadharia zilizotumika katika utafiti huu na namna zilivyosaidia katika uchambuzi wa data.

#### **2.2 Kazi Tangulizi**

Kazi tangulizi ni mpangilio maalumu na ufafanuzi na uchambuzi wa maandishi kuhusu habari inayohusiana na suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi lazima yaoneshe uhusiano na mada unayoifanyia utafiti. Kupitia tafiti mbali mbali zilizowahi kufanywa ambazo zina uhusiano na mada inayotafitiwa. Aidha, mapitio ya kazi tangulizi lazima yaoneshe ufafanuzi na mahitaji hususani, iwapo utafiti umewahi kufanywa hapo kabla unaohusu mada kama hiyo (Enon, 1998). Naye Mwakamele (2012:72), anaeleza kuwa kazi tangulizi ni mfumo wa kiuchambuzi na uainishaji wa maandishi wa habari inayohusiana na utoaji wa taarifa unahusu mada fulani ya taaluma.

#### **2.3 Dhana ya Wahusika**

Dhana ya wahusika katika kazi za fasihi imewahi kufasiliwa na watafiti kadhaa. Kama ilivyokwishaelezwa kuwa wahusika katika kazi za fasihi ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni binaadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi, na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa

na wanayoyasema na wanayoyatenda. Wahusika huweza kutambulishwa pia na maelezo ya mhusika au msimulizi, msingi wa hisia, hali ya kimaadili, mazungumzo na matendo ya wahusika ndio kiini cha motisha au uhamasishaji wa wahusika (Wamitila, 2002).

TUKI (1998:169), wamefasili wahusika kuwa ni watu, miti au viumbe vinavyowakilisha watu katika kazi za fasihi. Wahusika hutumiwa katika kazi za fasihi ili kuwakilisha hali halisi ya maisha ya watu katika jamii inayohusika. Katika mgogoro unaozungumziwa katika kazi ya fasihi hutumiwa kuwakilisha mawazo mbalimbali ya pande mbili au zaidi za mgogoro huo.

Maelezo hayo ya Wamitila na TUKI yalikuwa na umuhimu mkubwa katika kusukuma mbele kazi hii. Hii ni kutokana na kwamba, Wamitila amedokeza maswala muhimu sana katika kutoa maana ya wahusika katika kazi za fasihi. Sifa kama zile za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo huwa zinawatambulisha wahusika hao zilitupa mwanga na muongozo mzuri katika utafiti wetu huu uliolenga kuchunguza namna wahusika wanavyolandana na majina yao katika riwaya teuliwa.

Rono (2013) akimnukuu Msokile (1992:42-43), anaeleza kwamba, wahusika husawiriwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Mwandishi huwasawiri wahusika kwa wasomaji wake kwa kutumia sifa pambanuzi walizonazo, jinsi walivyo, mambo gani hawayapendi na yapi wanayapenda katika maisha yao na kadhalika. Wahusika hao hutumia misemo,

nahau, tamathali za usemi na methali katika mazungumzo yao ili kujenga tabia na hali ya kisanaa.

Rono (ameshatajwa), anaendelea kueleza kuwa, wahusika wa kazi za sanaa huwa na tabia zinazotofautiana kati yao kwa sababu mbalimbali. Kwanza kabisa inategemea mwandishi ana lengo gani analotaka kuonyesha katika kazi yake ya sanaa. Pili, aina ya kazi ya sanaa inaweza kuathiri aina ya wahusika jinsi walivyosawiriwa, kuaminika kwao, wanavyohusiana wao kwa wao, uwakilishi wao na majina yao. Wahusika katika hadithi ni mhimili mkubwa katika fasihi andishi na hata simulizi.

Aidha, Msokile (1992), akiwanukuu Penina Muhando na Ndyanao Balisdya wanasema kwamba wahusika wanaweza kuumbwa kinafsia, kiakili na kimwili. Kutokana na ujenzi wa aina hii, mhusika huonyesha wasifu wake wa ndani na nje au anaweza kuonyesha mabadiliko yake kila anapokutana na mazingira tofauti. Ataonyesha mabadiliko katika uhalisia wake kwa kuzingatia nguvu zinazomzunguka kama vile za utamaduni, siasa, uchumi na kadhalika.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008:369), wahusika ni nyenzo kuu katika fasihi kwa sababu wahusika ndiyo dira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi inayohusika. Mtazamo wa dhana ya wahusika hutofautiana kutegemea mkabala anaouchukua mhakiki na nadharia ya fasihi inayohusika.

Mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni, ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanadamu. Hii ndio maana neno “mhusika” linatumika bali si ‘mtu’ au ‘Kiumbe’. Mwelekeo wa kuwahusisha wahusika wa kifasihi na binadamu

wanaopatikana katika hali halisi huathiri kwa kiasi fulani matarajio ya usawiri wa uhusika. Upo mwelekeo mkubwa wa kuwachunguza wahusika wa kifasihi kwa kuwafungamanisha na binadamu halisi na hata, labda kutokana na athari za mielekeo ya kimaadili, tukitarajia kuwa wahusika, hasa wale wakuu watakuwa na maadili fulani.

Hata hivyo, tunakubaliana na Kundera (2007) kuwa, wahusika wa kifasihi hawahitaji kupendwa kutokana na maadili yao bali wanachotakiwa kufanywa ni kueleweka. Matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi huhusishwa na wahusika. Matendo hayo ni nguzo kuu ya dhamira na maudhui yanayoendelezwa katika kazi inayohusika. Mawazo hayo ya Kundera yalitupa mwanga mkubwa wakati wa kuwachungua wahusika na namna wanavyolandana na majina yao na namna walivyobebeshwa dhamira na waandishi wa riwaya teuliwa.

Kulingana na Njogu na Chimerah (1999:45), wahusika ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Mazingira haya yaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Wahusika hujadiliwa kwa namna wanavyoingiliana na dhamira na hili hujitokeza kutokana na maneno, tabia na matendo yao, yaani kulingana na hulka yao. Wahusika wa aina yoyote wawe watu au viumbe hurejelea na huakisi sifa na tabia za binadamu katika jamii husika.

#### **2.4 Aina za Wahusika**

Kuna njia nyingi za kuwaainisha wahusika katika riwaya. Wahusika wana sifa zinazofungamana na majukumu fulani na tofauti. Hali hii ina maana kuwa wahusika hao watakuwa na sifa zinazofungamana na majukumu yao hayo. Katika kazi hii

kwanza tuliwaainisha wahusika kupitia njia mbili kuu ambazo ni sifa na nafasi zao katika kazi husika. Baadaye tuliangalia njia nyingine za uainishaji.

Kulingana na Njogu na Chimera (1999), wamewaainisha wahusika wakizingatia kigezo cha sifa kama ifuatavyo:

#### **2.4.1 Wahusika wa Miraba Minne na Wahusika wa Mraba Mmoja**

Wahusika wa miraba minne wana sifa nyingi. Nyingine zikiwa nzuri na nyingine zikiwa mbaya. Maisha ya wahusika wa aina hii ni mapana katika tajriba na matukio ya kazi ya fasihi ambayo hutoa athari pana katika maisha ya jamii kila siku.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002:21-22), amewaainisha wahusika katika makundi mawili akizingatia mawazo ya Forster (1927). Makundi haya ni wahusika bapa na wahusika duara. Wahusika duara wanapatikana katika riwaya nyingi za Kiswahili za kisasa. Hawa ni wahusika wanaokaribiana kwa kiasi kikubwa na binadamu wa kawaida. Msingi mkuu wa kuwabaini wahusika hawa ni uwezo wao wa kuweza kutustukiza au kutushangaza. Uduara wa wahusika umo kwenye mabadiliko yanayowajia. Mabadiliko haya yaweza kuwa ya kitabia, kimawazo, kijamii, kiukuaji na kadhalika. Matendo na maisha yao yanaongozwa na hali halisi za maisha. Wanajibainisha kwa mapana na marefu yao kihisia na kimatendo. Hawa ndio wahusika wanaovutia zaidi kwa sababu wanaisukuma na kuisogeza mbele riwaya. Kwa mfano, Runo (2013), alipokuwa akifafanua dhana hii alitoa mfano wa mhusika Imani katika *Kidagaa Kimemwozea* (2012) kwamba mhusika huyo hana nguvu za kimwili za kuweza kukabiliana na mateso yanayompata. Lakini, polepole anabadilisha nia mara tu anapokutana na Amani karibu na ziwa Mawewa.

Anapevuka kiurazini na kuweza kukabiliana na mfumo wa uzalishaji mali unaomnyanyasa.

Kuhusu wahusika bapa ni kwamba hawa hutumiwa na mwandishi kusimamia wazo fulani. Yaani, tangu mwazo hadi mwisho wa hadithi, wahusika hawa wamebuniwa kuzingatia na kutenda matendo yanayolandana na sifa walizopewa. Hawabadiliki hata hali za maisha zinapobadilika. Mwandishi anawaelekeza kwa lengo maalumu, hasa kuhusu maadili fulani ya kijamii. Wahusika bapa huwa na sifa za wahusika wa mraba mmoja.

Wamitila (2002), anafafanua kwamba wahusika bapa huwa ni wa aina mbili, bapa sugu, wanajulikana kutokana na maelezo ya msanii. Huwa sugu katika hali zote za maingiliano na wengine na sifa zao au jinsi wanavyoelezwa na mwandishi. Wahusika bapa vielelezo hawabadiliki na hupewa majina ambayo yanaafikiana na matendo na tabia zao. Majina ya wahusika hawa, huwa kama kielekezi na kifupisho cha wasifu wao.

Kuhusu suala la wahusika bapa vielelezo, yalikuwa na manufaa makubwa sana kwa mtafiti, kwani, sifa za wahusika ni miongoni mwa dhumuni la utafiti huu. Kwa hivyo, mtafiti alitumia msingi huo ili kuona namna wahusika walivyopewa majina kutegemea sifa zao.

Kulingana na Wamitila (2002:23), kuna wahusika ambao huchukua nafasi kuu au wanaoitawala kazi kifasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hawa ni wahusika wakuu ambao husheheni hadithi nzima. Matendo na migogoro ya hadithi nzima

huwahusu. Kuna wengine ambao wanakuwa kama wasaidizi wa wahusika hao wakuu au hutumiwa kama wajenzi wa maudhui mbalimbali. Hawa ni wahusika wasaidizi na wajenzi.

Wahusika wasaidizi huhusiana kwa karibu sana na wahusika wakuu na hutumiwa na mwandishi kumfafanua zaidi mhusika mkuu. Sifa za mhusika mkuu hubainishwa wazi kupitia maingiliano baina yake na wahusika wasaidizi. Wahusika wajenzi hujenga wahusika wakuu na hujenga wahusika wasaidizi kwa hivyo kukamilisha dhamira za mwandishi katika riwaya. Kigezo hiki ndicho kilichotumiwa na mtafiti kuainisha wahusika katika riwaya teuliwa.

Kwa maoni ya mtafiti, anaona kwamba, ugawaji nzuri wa wahusika ni ule aliobainisha Wamitila (2002), ambapo anaonesha kwamba, wahusika huweza kuwa katika matapo matatu. Matapo hayo ni wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Mtafiti alipendezewa na mgao huo kutokana na kugundua kuwa, riwaya nyingi zinaakisi wahusika wanaoweza kuekwa katika matapo hayo.

### **2.5 Njia Nyingine za Kuwabainisha Wahusika**

Uchunguzi wa historia na maendeleo ya fasihi unadhihirishwa kuwa, wahusika wa kifasihi hubadilika kadri wakati unavyoendelea. Wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi za miaka ya zamani wanatofautiana kwa kiasi kikubwa na wahusika wanaopatikana katika kazi za fasihi za miaka ya baadaye.

Njogu na Chimera (1999:40-44), wanarejelea wahusika wanaozungumziwa Mlacha na Madumulla (1991).

Wamitila (2008: 382-392), amegawanya wahusika katika makundi manne. Mhusika wa jadi, mhusika wa kimuundo au kimtindo, mhusika wa kihalisi na mhusika wa kisasa.

### **2.5.1 Mhusika wa Kijadi**

Dhana ya kijadi inakwenda na suala la wakati na hasa wakati wa zamani. Mhusika wa aina hii basi ni anayeweza kuelezwa kama mhusika wa zamani. Mtindo huu wa kusawiri wahusika umetumiwa na baadhi ya waandishi mbali mbali wa kazi za fasihi. Kwa mfano, katika tamhiliya ya *Kivuli Kinaishi* (1990), mhusika Bi Kizee ni mfano wa mhusika wa kijadi. Aidha, katika tamhiliya ya *Mfalme Juha* (1971) wahusika Mfalme na Juha ni mfano wa wahusika wa kijadi kwa sababu hawa wamekuwa ni wahusika wa kimapokeo katika kazi mbali mbali za kisimulizi.

### **2.5.2 Mhusika wa Kimuundo na Kimtindo**

Mhusika wa kimuundo na kimtindo huainishwa kuhusiana na wahusika wanaorejelewa. Mawazo ya wana muundo ni ya kimsingi katika kuwainisha wahusika wa aina hii. Kulingana na Wamitila (2008), wahusika wa aina hii wameainishwa kama ifuatavyo:

#### **2.5.2.1 Mhusika wa Kiuamilifu**

Huyu ni mhusika ambaye anabainishwa kwa kuwa na sifa za aina moja ambazo kimsingi zinapangiwa kumfanya mhusika huyo kuwa chombo cha mwandishi ili kutimiza lengo fulani. Pia anaweza kubainishwa kwa kuangalia nafasi yake ya kiutendaji. Mfano nzuri ni Karama katika riwaya ya *Kusadikika* (1981), yeye atumiwa na msanii kufanikisha lengo lake akiwa kama mzalendo na mkombozi wa jamii.



### **2.5.2.2 Mhusika wa Kiishara**

Mhusika wa kiishara anatumiwa kiishara, yaani ni sehemu ya uashiriaji katika kazi ya kifashi. Kwa mfano Rono (2013), anamtumia Mhusika Amani katika *Kidagaa Kimemwozea* (2012), kama ni ishara ya mabadiliko katika jamii ambayo haiwezi kuuliwa na harakati za utawala mbaya wa kuyazuia mabadiliko yenyewe. Ndiye aliyelongoza katika uchunguzi wa nyendo za Nasaba bora wakiwa na Majisifu kisha wakagundua matendo yake maovu. Aidha, kisa cha fahali kumeza nguo katika riwaya hiyo ya *Kidagaa Kimemwozea* ni ishara ya nasaba bora aliyokuwa akitafuna ardhi na mali za raia wake bila huruma na kuwaacha maskini. Usimulizi wa mto Kiberenge na maji yake kutonywewa na wakazi wa maeneo yake ni ishara kuwa, wakati hao huafikiana na maswala fulani bila utafiti au uchunguzi wowote.

### **2.5.2.3 Wahusika wa Kinjozi**

Wahusika wa kinjozi ni wahusika wanaohusishwa na fantasia. Hupatikana katika ulimwengu wa ajabu. Kwa mfano, Mhusika Pama katika riwaya ya Siri za Maisha ni mfano wa Mhusika wa kinjozi kutokana na matendo yake ya kiajabu.

### **2.5.2.4 Mhusika wa Kihalisi**

Msingi mkuu katika uainishaji wa wahusika wa aina hii ni kanuni ya maisha halisi, kwa kutegemea kanuni ya ushabihii kweli. Mhusika wa kihalisia ana sifa nyingi zinazohusishwa na binadamu katika maisha ya kila siku. Kulingana na Wamitila (2008), tapo hili lina wahusika wa aina tatu, mhusika wa kimapinduzi, mhusika wa kisaikolojia na mhusika wa kidhanaishi. Wahusika hawa wamefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

#### **2.5.2.4.1 Mhusika wa Mapinduzi**

Mhusika wa kimapinduzi ana sifa zote zinazohusishwa na mtu anayeweza kupatikana katika maisha halisi. Mhusika huyu anasukumwa na kuchochewa na nia ya kutaka kubadilisha jamii yake. Wahusika Mdoe na Sikamona katika riwaya ya *Zawadi ya Ushindi* ni mifano mizuri, wanasukumwa na nia ya kutaka kuyabadilisha maisha katika jamii yao ambayo inaongozwa na viongozi walafi na wananchi wengine wenye tamaa ya kupata mali kwa njia zisizo za halali.

#### **2.5.2.4.2 Mhusika wa Kisaikolojia**

Mhusika wa kisaikolojia anaonyeshwa kwa undani zaidi na labda hata misukumo ya kisaikolojia ya matendo yake kuonyeshwa kwa njia bayana. Mama Ntilie katika riwaya ya *Watoto wa Mama Ntilie* ni mhusika wa kisaikolojia kulingana na yale anayopitia kutoka kwa mumewe Lomolomo na pia kufukuzwa kwa watoto wake shule kunapelekea kutumia akili yake zaidi ili apambane na hali hiyo na kumiliki nafsi yake isiathirike kisaikolojia.

#### **2.5.2.4.3 Mhusika wa Kidhanaishi**

Mhusika wa kidhanaishi anaakisi sifa kadhaa zinazohusishwa na falsafa ya udhanaishi ambayo msingi wake ni kudadisi ukweli, furaha na hali ya kuweco maishani. Mfano nzuri wa kazi za kifasihi zilizoandikwa na Kezilahabi kama vile *Nagona* na *Mzingile* zinasadifu sana matumizi ya wahusika wa kidhanaishi. Katika riwaya ya *Nagona*, wahusika Paa na Mimi wanawakilisha kundi hili.

Wafula na Njogu (2007), wanasema kwamba mhusika anaweza kuangaliwa kama mtu binafsi na maisha yake. Walirodhesha wahusika kama jaribosi au nguli, kivuli

na wengineo. Nguli aghalabu huwa mhusika mkuu mbae husafiri kwa sababu fulani. Mara nyingi safari hii huanzia utotoni hadi anapofikia utu uzima. Wakati mwingine hii inaweza kuwa safari ya kikweli ambapo nguli anajizatiti kukisaka kitu au kujisaka mwenyewe. Mkinzani wa nguli hupambana kuiharibu mipango ya nguli kwa kujaribu kumwangamiza. Aghalabu mhusika huyu huwa mzinzi, mlafi na wakati mwingine huwa tajiri kama vile Mzoka katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Aidha katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, mhusika Adili anasafiri kwa ajili ya kufanya biashara. Katika safari hizo tunaoneshwa ndugu zake Mwivu na Hasidi wanavyoamua kumtupa baharini kutokana na wivu na choyo. Mwisho tunaona namna anavyookolewa na mtoto wa Mfalme wa Kijini, Huria. Mjadala huu kuhusu matapo ya wahusika ulikuwa na manufaa sana kwa mtafiti, kwasababu, mtafiti alitumia mawazo hayo, ili kubaini aina za wahusika waliotumika katika riwaya teuliwa.

## **2.6 Mbinu za Usawiri wa Wahusika**

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mwandishi anaweza kutumia njia kadhaa na tofauti katika kuwasawiri wahusika wake. Msanii ana uhuru sio tu wa kuwatumia wahusika wa aina fulani, bali wa kuiteua namna ya kuwawasilisha wenyewe. Kama wasomi na wahakiki wa fasihi, tunategemea sifa kadhaa kuwaelewa wahusika hao: maumbile yao, mienendo na tabia zao, lugha zao, vionjo vyao, uhusiano wao na wahusika wengine, hisia zao kwao na wengine, mazingira na mandhari yao, kiwango chao cha elimu, jamii yao nakadhalika.

Mbinu zinazotumika kusawiri wahusika ni kama vile; mbinu ya kimaelezi, mbinu ya kidrama, mbinu ya uzungumzi nafsi wa ndani, mbinu ya majazi au matumizi ya

majina, mbinu ya kuwatumia wahusika wengine na mbinu ya ulinganuzi na usambamba.

Wamitila amesainisha na kuchambua mbinu zifuatazo ambazo hutumika katika kuwasawiri wahusika. Mbinu hizo zimetolewa ufafanuzi kama ifuatavyo:

### **2.6.1 Mbinu ya Kimaelezi**

Kwa mujibu wa Wamitila (2002:23-24), anayetumia mbinu hii huzieleza sifa za mhusika na mara nyengine hutoa picha ya maneno inayomwelezea mhusika anayehusika. Kwa kutumia mbinu hii, mwandishi anakuwa na nafasi ya kubainisha mapenzi au chuki yake dhidi ya wahusika fulani. Hii ni njia rahisi ya kuwasawiri wahusika na hasa kwa kuwa mwandishi anaweza kutoa maelezo machache yanayoifumbata tabia au wasifu wa mhusika ambao ungechukua muda mrefu kutokana na matendo yake mwenyewe. Hata hivyo, hii ni mbinu ambayo ina udhaifu pia.

Mbinu hii ya kimaelezi haimpi msomaji nafasi ya kushiriki katika kuitathmini tabia ya mhusika fulani. Analazimika kuukubali msimamo na kuridhika na maelezo ya mwandishi. Mfano unaofuata unaonesha namna ya mbinu hii inavyotumika; kutoka katika riwaya ya *Vuta n`kuvute* ya Shafi A Shafi:

“Yasmini alikuwa na kijuso kidogo cha mdawiri mfano wa tungule na macho makubwa ambayo kila wakati yalionekanwa kama yanalengwalengwa na machozi. Alikuwa na pua ndogo, nyembamba na chini ya pua hiyo ilipangana midomo miwili mizuri iliyokuwa haitulii kwa tabia yake ya kuchekacheka, huku akionyesha safu

mbili ya meno yake mazuri. Alikuwa na kichaka cha nywele nyeusi zilizokoza ambazo zilianguka kwa utulivu juu ya mabega yake. Alikuwa si mrefu lakini hakuwa mfupi wa kuchusha, na matege aliyokuwa nayo yalizidi kuutia haiba mwendo wake wakati anapotembea” (1999:1).

Haya ni maelezo ya mwandishi kumhusu mhusika huyu ambayo yanatokea katika sehemu ya mwanzo. Ingawa hasemi wazi wazi, uteuzi wake wa maneno unatuelekeza kuamini kuwa ana mtazamo fulani kumhusu mhusika na ambao huenda ukatuelekeza kwenye njia fulani.

### **2.6.2 Mbinu ya Kidrama**

Wamitila (2002), mbinu hii ya ki-muhakati (ki-mimesia), kama ilivyo katika tamthilia, huonyesha wasifu wa mhusika wake. Pia mbinu hii inamwezesha msomaji au mhakiki kumjua na kumweleza mhusika bila ya kuathiriwa na mtazamo wa mwandishi au msimulizi kumhusu.

### **2.6.3 Mbinu ya Uzungumzi Nafsi wa Ndani**

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mbinu hii hulinganuliwa na nyengine inayojulikana kama mkondo wa king’amuzi/kirazini. Mawaazo yanayopatikana katika mbinu hii huwa na mshikamano wa muwala, mawazo hayo yamepangika kama unavyoweza kutokea katika ung’amuzi nafsi wa kawaida, yaani pale endapo mhusika anapoongea peke yake.

Kwa upande mwengine, mkondo wa king’amuzi ni mbinu inayotumiwa kuonyesha mawazo hayo au hisia za wahusika bila ya kuyahariri mawazo hayo au kuyapanga

kwa namna yoyote ile iwayo. Hii ni mbinu inayotumiwa sana katika uandishi wa unaokita kwenye tapo la usasaleo.

Mbinu ya uzungumzi nafsi wa ndani hujulikana kama “mjadala wa ndani” au “mjadala mdogo”. Mjadala unaonekana hapa unazihusisha sauti mbili zinazohusika kwenye majibizano. Sifa muhimu ni kuwa lazima maswali au majibu yanayopatikana yaibuke katika sauti ambazo zinawakalisha mikabala, imani au sifa tofauti.

#### **2.6.4 Mbinu ya Kuwatumia Wahusika Wengine**

Wamitila (2002:26), badala ya kuyatumia majina ya wahusika, mwandishi anaweza kusawiri mhusika kupitia kwa kuelezwa na wahusika wengine. Wahusika wanaweza kuelezwa na wahusika wengine, yaani tunawajua kutokana na maneno ya wahusika wenzao. Hapa pana tathmini ya mhusika ambayo ni ya ndani (kwa wahusika wengine), kuliko ya nje kama ya masimulizi (mbinu ya kimaenzi).

Hata hivyo lazima tukumbuke maneno anayoyatamka mhusika A kumhusu mhusika B yanaweza kuangaliwa kwa njia mbili. Kwanza, yanaweza kutusaidia kumwelewa B kwa kutufichulia mambo ambayo hatuwezi kuyajua bila ya kuelezwa. Pili, inawezekana kauli anazozitamka A kumhusu B zikatuonesha alivyo mhusika A kuliko alivyo B.

#### **2.6.5 Mbinu ya Ulinganuzi na Usambamba**

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mwandishi anaweza kuitumia mbinu za usambamba na ulinganuzi katika kuwasawiri na kuwakuza wahusika wake. Ulinganuzi ni nini? Huu ni ulinganishi kwa kinyume. Kuweko kwa mhusika

ambaye ni kinyume cha mhusika fulani huweza kuwa ni mojawapo ya uhusika. Mwandishi anaweza pia kuwaweka wahusika au kuwaonyesha kwa namna ambazo ni sambamba na kwa njia hii humfanya msomaji au mhakiki aziwazie tofauti au mfanano wa sifa zao. Ni muhimu kukumbuka kuwa ulinganuzi sio tu mbinu ya uhusika bali hutumiwa katika usimulizi wa matukio na ukuzaji wa dhamira na maudhui.

Wakati huo huo mwandishi anaweza kuwasawiri wahusika kwa namna ambavyo tabia zao zinaonesha kupingana kwa aina fulani. Yaani tukimwangaalia mhusika kwa makini, tunahisi kuwa kuna kupingana kwa sifa fulani katika uhusika wake. Hapa tunasema kuwa za ki-nzani.

#### **2.6.6 Mbinu ya Majazi au Matumizi ya Majina**

Wamitila (2002), waandishi wa kazi za kifasihi huweza kuyatumia majina ya wahusika ambayo huakisi mandhari zao, wasifu wao, itikadi zao, vionjo vyao nakadhalika. Uchunguzi wa majina ya wahusika lazima uhusishwe na msuko, mbinu za utunzi, ucheshi, dhamira na maudhui na itikadi au motifu katika kazi inayohusika.

Tunapozungumzia kulandana kwa wahusika na majina yao katika kazi faulani ya fasihi, ni kule kuwiana kwa matendo ya wahusika na majina yao, sifa zao na majina yao, lugha yao na majina yao, kujiamini kwao na jinsi majina yao yalivyo, elimu yao na majina yao, maana ya majina yao na jinsi yanavyofanana na wao wenyewe ambapo msanii wa kazi ya fasihi huzitumia sifa hizi, katika kusadifu hali fulani iliyo zoeleka katika jamii.

Maelezo hayo yalikuwa na mchango mkubwa kwa mtafiti katika kusukuma mbele utafiti huu. Hii inatokana kuwa Wamitila ameweza kuonesha na kufafanua vipengele vya msingi ambavyo vilitumiwa na mtafiti katika kuchambua lengo la utafiti na hatimae kuweza kufikia lengo la utafiti huu.

Aidha, kamusi ya BAKIZA (2010:208), wamefasili neno kulandana kuwa, linatokana na nomino landa lenye maana ya kitendo cha kufanana na mtu ama kushabihiana. Landana pia ni kitendo cha mtu kuwa na sura inayofanana na mwenzake; shabihiana.

Ingawa maelezo ya BAKIZA juu ya neno kulandana hayakuelezwa kwa mkabala wa kifasihi, hata hivyo, maelezo hayo yalitoa mwanga kwa mtafiti, kuhusu maana halisi ya neno kulandana, ambapo alitumia dhana hiyo katika uchambuzi wa data zake.

Wamitila (2002:64), sadifa katika fasihi; kwake yeye, sadifa ni uzuri au ubaya. Sadifa ni utukiaji wa matukio kwa wakati mmoja na aghalabu kwa namna ya kushangaza inayoashiria bahati. Umuhimu wa dhana hii unatokana na kujitokeza kwake kwingi katika kazi kadhaa za fasihi ya Kiswahili. Kwa kuanzia ni muhimu kutaja kuwa sadifa hutumiwa kama mbinu au kipengele cha msuko au kimtindo. Katika baadhi ya tanzu, sadifa ni kipengele muhimu katika muundo wake.

Tuisomapo hadithi ya Jamaadar ya Mui huwa Mwema, yanayaona matumizi ya sadifa kuhusiana na Kotini na wahusika wengine. Vivyo hivyo katika riwaya za M.S.Abdulla. Katika riwaya za M.S.Abdulla huwa sadifa jinsi matukio ya wahalifu



yanavyokunjuka na hatimaye kufichuka. Sadifa katika kazi hizi ni kipengele cha lazima.

Maelezo haya ya Wamitila tunaona kuwa yana mnasaba na mshabihiano mkubwa katika mada yetu ya kuchunguza dhana zilizobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao, hivyo ni dhahiri kwamba kupitia maelezo haya tuliyatumia kama dira ya kufikia lengo la utafiti wetu.

Njogu na Chimera (1999), wameeleza kuhusu suala la sadifa kwa wahusika katika riwaya ya *Siku Njema*, ambapo wahusika Bi Rahma kasadifu vyema, Rashid Omar kasadifu na anakufa lakini kifo chake si cha kifasihi, Zawadi anasadifu kuolewa na Kongowe, mtoto wa miaka kumi na sita, ilihali yeye ana miaka ishirini na mitatu na akiwa na elimu ya juu. Pia wahusika wengine waliohakikiwa ni Alice MacDonald, Vumilia Abdalla, Amina na Juma Mukosi.

Ufafanuzi wa huu uliofanywa na Njogu na Chimera unaonekana kuwiana vyema na mada yetu hii ya kuchunguza dhana zilizobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao, hivyo kwa kuzingatia mbinu hii pia mtafiti alipata msaada mkubwa uliomwezesha kufikia malengo ya utafiti wake.

### **2.7 Kazi Tangulizi Kuhusu Uhakiki wa Wahusika**

Watafiti kama vile Kyando (2012), Wafula (1999), Omar (2011) na Kenan (2007), wamewahi kutafiti wahusika mbali mbali katika kazi za fasihi. Kwa mfano Kyando (ameshatajwa), alitafiti majina sadfa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Kichwa Maji*. Katika utafiti wake aligundua kuwa, wahusika katika riwaya hizo wamepewa majina kwa kuwagawa wahusika hao kutegemea wema na ubaya. Katika kusisitiza mtazamo wake juu ya Aisha na maadili katika jamii, mwandishi ameamua kuwapa

wahusika wake majina yanayosadifu sifa zao na uhusika wao. Uwiyano huu tunaupata kwa kuangalia maana halisi ya jina na mhusika na jinsi mwandishi alivyomchora katika kazi husika ili kusadifu jina hilo.

Aidha, riwaya ya *Kichwa Maji* imetumia majina ya wahusika kulingana na tabia zao wanakuwa na kubadilika. Tabia zilizobeba majina yao zimeonekana kuwa na umuhimu zaidi kuliko nyengine. Hii ndio hali halisi ya maisha ya binaadamu kukua na kubadilika kulingana na wakati pamoja na hali inayomkabili. Kwa mfano majina sadifa yaliyojiokeza katika riwaya ya *Kichwa Maji* ni Kazimoto; likiwa na maana ya kufanya kazi kwa bidii, Kalia; chukua nafasi ya mtu mwingine na kadhalika. Kyando, katika utafiti wake aliongozwa na mbinu ya majazi tu, hakuchunguza mbinu nyengine za kuwasawiri wahusika kama vile; za kimaelezi, kidrama, uzungumzi nafsi wa ndani, mbinu ya kuwatumia wahusika wengine na ulinganuzi na usambamba ambazo pia, mtafiti aliona hutumiwa na wasanii wa kazi za fasihi katika kuwasawiri wahusika na majina yao. Kwa hivyo, mtafiti alizitumia mbinu hizo, kuchunguza namna wahusika katika kazi teuliwa walivyolandana na majina yao.

Ingawa, Kyando hakutumia mbinu changamano, utafiti wake ulikuwa na manufaa sana kwa utafiti huu. Kwani mtafiti alipata muongozo wa namna ya kuchambua data zinazohusiana na wahusika walivyolandana na majina yao kupitia mbinu anuai.

Omar (2011), ameelezea majazi kuwa ni jina la kubuni linalotumiwa na waandishi, waimbaji, wasanii, waigizaji, wachezaji, watu au kundi badala ya jina halisi. Kwa kawaida ni jina linaloteuliwa kwa kuzingatia sifa za mtu. Kila mwandishi huwa na

lengo fulani pamoja na ujumbe anaoutaka kuufikisha kwa jamii, hivyo hutafuta namna ya kufikisha ujumbe huo. Malengo hayo ni pamoja na kuonesha maadili katika jamii pamoja na kumuwezesha msomaji kuelewa na kuwatambua wahusika kiurahisi.

Ingawa Omari hatoi ufafanuzi wa kina kuhusiana na majina ya wahusika katika mbinu ya majazi ili kutoa uwelewa wa kina wa namna inavyojidhihirisha. Hata hivyo mtafiti alitumia mjadala huu katika kuchunguza majina ya majazi yaliyojitokeza katika riwaya teuliwa na jinsi yanavyolandana na majina ya wahusika.

Gibe (1983), amehakiki majina ya wahusika katika tamthilia ya *Mwanzo wa Tufani* (1975), ameeleza kwamba baadhi ya majina yaliyotumika yamesaidia kuimarisha tamthiliaya hii kisanaa. Baadhi ya majina yanaonesha tabaka la mhusika, kama ni mnyonyaji au kama ni mnyonywaji. Kwa mfano, Kitambi ana jina linalosadifu hali yake. Yeye ameotesha na kufuga kitambi kutokana na jasho la wengine. Kitambi ni shibe ya dhulma.

Kazimoto ni wa tabaka linalonyonywa. Yeye ana imani na “kazi” zake. Lakini anaendelea kushikilia imani yake hiyo. Jina la Kazimoto ni zuri na mwangi wa kazi moto moto zinazofanywa na tabaka linalodhulumiwa.

Boratwende ni jina jingine zuri. Jina hili linawahimiza wanyonge kwenda mbele katika harakati zao. “Boratwende” kuliko kuzohalika. Uchambuzi huu wa majina uliofanywa na Gibe ulikuwa na manufaa makubwa kwa mtafiti.

Kazi ya Gibe, ilitoa maarifa mapya kwa mtafiti kuhusu namna ya kuwachambu wahusika na namna walivyolandana na majina yao kutegemea sifa, tabia, matendo, kazi, utashi, imani walizobebeshwa na wasanii wa riwaya za *Kiu* na *Kiu ya Haki*.

Mtobwa (2002), ameweza kuwafinyanga wahusika wake na kuwahusisha na majina yao. Ametumia mbinu ya kuwapa majina ambayo moja kwa moja yanawiana na matendo yao pamoja na sifa zao. Kwa mfano, tunamuona mhusika Maua alivyoumbika kwa sura nzuri inayopelekea kupendwa na wanaume wengi anaokutana nao. Kanda wa Kamkanda yeye amepewa sifa ya ujasiri na uzalendo hivyo anafichua wahujumu uchumi. Wahusika wengine kama Dora, Kandili Maulana, Bon, Chema wote hawa wanalandana vyema na majina yao. Kwa msingi huu riwaya hii ilitupa msukumo mkubwa wa kuweza kufikia malengo ya utafiti wetu.

Robert (2008), amehusisha majina ya wahusika wake na matendo yao pamoja na sifa zao. Kwa mfano mhusika Utu busara Ujinga Hasara, huyu amepewa matendo ya utu, hekma na busara kama jina lake lilivyo. Pia mhusika Mwalimu anatumia taaluma yake kuielimisha jamii juu ya masuala mbali mbali yahasuyo maisha ya jamii yake.

Ruhumbika (1995), amesawiri vyema wahusika wake katika kulandana na majina yao kwa mfano tukimwangualia mhusika Nzoka Yape, jina hili lina maana ya nyoka mweupe, ambapo mhusika huyu ana matendo ya nyoka mwenye sumu kali, ni kiongozi katiki, mwovu na mzizi, asiye na haya na mfisadi. Rose Mary, analandana

na jina lake kutokana sifa yake ya urembo aliyoumbwa nayo. Riwaya hii pia ilitupatia msaada mkubwa sana katika mada yetu ya utafiti.

Shafi (1994), katika riwaya yake ya *Kuli*, wahusika wake wote wamelandana na majina yao, kwa mfano Amina, maana yake ni kushukuru. Anaonekana kuridhia mateso anayoyapata mume wake huku akiwa na matumaini ya kuondokana na mateso hayo siku mosja. Majaaliwa linaonesha jinsi mhusika huyu alivyokirimiwa mawazo mema, busara, hekma na matani awapo kazini kwake. Aidha, Shafi (1999), ameyasawiri majina ya wahusika wake wengi katika riwaya ya *Vuta Nkuvute*, kwa mfano mhusika Raza yeye kapewa sifa ya utajiri kutoka kabila la wahindi ambao ni miongoni mwa makabila matukufu yaliyokuwa yakitukuzwa zama za ukoloni. Matendo na lugha yake yanalandana na jina lake. Mambo ni mhusika anayelandana sana na jina lake kutana na tabia yake ya uchale na uchepe anayoionesha, vichekesho vyake, kutokuwa na aibu mbele za watu na kufanya mambo ambayo wakati mwengine kwa mtu mwenye akili zake tumamu hawazi kayadhihirisha mbele za watu.

Naye Kiango (2012), alifanya uchambuzi wa vipengele vya fani na maudhui. Katika uchambuzi huo, wahusika ni miongoni mwa vingele vya fani vilivyoshughulikiwa. Hata hivyo, kazi yake ilikuwa ni tofauti na utafiti huu kwasababu, Kiango alichambua wahusika kutegemea na wasifu wao. Uchambuzi huo haukhusisha namna wahusika wanavyolandana na majina yao. Hivyo mtafiti katika utafiti huu amechambua wahusika wa riwaya teuliwa na kuonesha dhana zilizobebwa nawahusika na zinayolandana na majina yao.

Mapitio haya tuliyofanya yanaonesha kuwa kuna uhusiano wa wahusika wa kazi hizo walivyobeba dhana zinazolandana na majina yao. Hivyo, kazi hizi zilimsukuma mtafiti kuchunguza wahusika wa riwaya za *Kiu* na *Kiu ya Haki* jinsi walivyobeba dhana zinazolandana kwa kutumia mbinu anuai. Mtafiti aliamua kuzifanyia kazi kwasababu aligundua kwamba ni miongoni mwa kazi ambazo zilikuwa bado hazijafanyiwa katika kipengele cha wahusika wanavyolandana na majina yao hasa katika mbinu za kidrama, mbinu ya kuwatumia wahusika wengine, mbinu ya ulinganuzi na usambamba, mbinu ya majazi, mbinu ya kimaelezi na mbinu ya uzungumzi nafsi wa ndani.

## **2.8 Dhana ya Dhamira**

Kwa mujibu wa Senyamanza (2012), dhana ya dhamira haipaswi kuchanganywa na dhana ya maudhui kwasababu dhana hizo ni tafauti. Dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi katika kazi yake. Dhamira ni sehemu mojawapo tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Kwa kawaida dhamira kuu ndiyo hujenga kiini cha kazi mzima ya kazi ya fasihi. Dhamira kuu husindikizwa na dhamira ndogo ndogo na hizi ndizo zijengazo dhamira kuu. Wazo kuu ambalo hasa ndilo libebalo wazo kuu hutoa dhamira kuu.

Nae Madumulla (2009), anaeleza kuwa dhamira ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Anaendelea kueleza kuwa, Senkoro anatahadharisha kuchanganya dhamira na maudhui, jambo ambalo hutokea kwa wengi. Dhamira ni sehemu tu ya maudhui. Na aghalabu, dhamira kuu ndio hujenga kiini cha kazi yafasihi. Dhamira kuu ndio husindikizwa na dhamira ndogo ndogo. Wazo kuu hubeba funzo kuu.

Mjadala kuhusu dhamira kama ulivyoielezwa na Senyamanza (2012) na Madumulla (2009), ulikuwa na umuhimu mkubwa kwa utafiti huu, kwani mjadala huo ulimpatia mtafiti mawazo mapya ya namna ya kugundua dhamira katika riwaya teuliwa jambo ambalo lilifanikisha kujibu swali la utafiti.

Kwa maoni ya mtafiti anaona kwamba, dhamira ni lengo la mwandishi ambalo kwalo hulifikisha kwa jamii ili iweze kufuata mwenendo bora wa maisha. Dhamira katika kazi ya fasihi huweza kuwa zaidi ya moja. Kwa mfano, katika riwaya ya *Watoto wa Mama Ntilie* kunapatkana dhamira kama vile; umaskini, umuhimu wa elimu, madawa ya kulevya, wizi na ujambazi, ulevi, uongozi mbaya, suala la malezi na kadhalika.

### **2.9 Uhusiano kati ya Fani na Maudhui**

Kwa mujibu Masebo na Nyangwine (2000), suala la uhusiano wa fani na maudhui limezua mjadala mkubwa miongoni mwa wataalamu wa kazi za fasihi. Mjadala huo umewagawa wataalamu katika kambi kuu mbili. Wapo wanaodhani kwamba fani haina uhusiano wowote na maudhui. Wao wanaamini kwamba vipengele hivyo, vinaweza kutenganishwa bila kuathiri maudhui ya kazi husika. Kambii hii inawaitifaki kama vile Mkwera, Kiango, Sengo, Mhando na Balisidya. Kwa mfano, Mkwera analinganisha fani na maudhui na kikombe cha chai. Kikombe kinachukuliwa kama ndio fani na chai ndio maudhui, mnywaji wa chai hiyo, analinganishwa na msomaji wa kazi ya fasihi.

Mtazamo wa pili, ni ule wa kiyakinifu. Mtazamo huu unaona kwamba, fani na maudhui ni vitu visivyoweza kutenganishwa, kwani vipengele hivyo vinategemeana

na kuathiriana. Mtazamo huu, unashikiliwa na wataalamu kama vile; Kahigi, Senkoro na Mulokozi. Mathalan, Masebo na Nyangwine (wameshatajwa), wanamnukuu Senkoro akilinganisha fani na maudhui na sura mbili za sarafu moja, na sirahisi wala sahihi kuzitenga na kuziweka katika upweke bila kuzihusisha na nyengine. Umuhimu wa sura moja unategemea kuwepo kwa sura ya upande wa pili. Sura moja ya sarafu ikikosekana, basi sarafu hiyo, haiwezi kuwa na hadhi ya kisarafu.

Kwa maoni ya mtafiti ni kwamba, fani haiwezi kutenganishwa na maudhui. Kwasababu, vipengele hivyo hutegemeana katika kusanii kazi ya fasihi. Aidha, ukweli ni kwamba vipengele vya fani kama vile wahusika, mandhari, mtindo, muundo, na matumizi ya lugha ndio hutumiwa na mwandishi kubebea madhui yake. Bila vipengele vya fani tusingekuwa na kazi ya kifasihi.

### **2.10 Mkabala wa Kinadharia**

Nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo mkuu wa mtu au watu (jamii), wa pahala fulani, wakati fulani, kwa sababu fulani, Sengo (2009:1). Aidha, Njogu na Wafula (2007), wanafafanua kuwa, nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Nadharia ni maelezo ya jambo kufungamana na vigezo vinavyowekwa au vinavyozalika kutokana na majaribio ya jambo hilo.

Hivyo, utafiti huu uliongozwa na nadharia za sosholojia na mwitiko wa msomaji.

Nadharia hizo zimefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:



### **2.10.1 Nadharia ya Sosholojia**

Nadharia ya Sosholojia ni nadharia inayohusishwa na mwanasosholojia Adam Smith mwaka 1970, kama ni muasisi wa nadharia hii huko Marekani. Nadharia hii imejikita zaidi katika uhusiano wa mwanaadamu na jamii yake, kwani nadharia hii inaonyesha kuwa jinsi wasomaji wanavyoipokea, kuitathimini na kuihukumu kazi fulani ya kifasihi huathiriwa pia na mazingira ya wasomaji hao. Mfano Msokile anafafanua kuwa, nadharia hii huikabili kazi ya kifasihi kwa kuangalia jinsi inavyohusiana na mazingira ya kijamii, hivyo nadharia hii inaonesha kuwa hakika kuna uhusiano mkubwa kati ya kazi ya fasihi na jamii ambayo kazi hiyo imeandikiwa. Anaendelea kufafanua kuwa sanaa haijengwi katika ombwe, ni kazi ya mwandishi katika mazingira na wakati maalumu akiwajibika kwa jamii inayomuhusu ambayo ni sehemu yake muhimu. Mazingira ya jamii ndio huwezesha kubadili maudhui ya kazi ya fasihi.

### **2.10.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji**

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni nadharia ya kifasihi ambayo huwa inajikita katika kumuangalia msomaji (hadhira), uzoefu wake juu ya kazi za kifasihi. Ni nadharia ambayo imeasisiwa na Hans Robert James, Wolfgang Iser na Harald Invenrich mwishoni mwa miaka ya 1960, na mwanzoni mwa miaka ya 1970. Wananadharia hawa wanaeleza kuwa, kazi ya fasihi inapaswa kutazamwa kulingana na mila na desturi au utamaduni wa msomaji kwani msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake na si kutokana na uzoefu wa mwandishi.

Wanaendelea kusema kuwa kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira mbali mbali, kwa hiyo kutokana na taswira na ishara hizo matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja.

Wananadharia hawa huiona kazi ya fasihi kuwa ina mapengo mengi ambayo yanamlazimisha msomaji kuyaziba. Katika kuyaziba msomaji atajikuta ametunga matini nyengine mpya inayotokana na matini ile ya asilia. Kwa hivyo basi kazi kubwa ya msomaji ni kusoma kazi kwa ufuatiliaji wa hali ya juu kabisa na hatimaye kufasili kazi hiyo kutoka na uzoefu pamoja na uzoefu wake.

Katika utafiti wetu huu tumeongozwa na nadharia ya Sosholojia na nadharia ya Mwitiko wa msomaji. Tumechaguwa nadhari hizi kwa sababu nadharia ya Sosholojia ilituongoza kuangalia uhusiano na tabia za wa wahusika hao na jinsi wanavyolandana na majina yao. Pili nadharia ya Mwitiko wa Msomaji tumeichaguwa kwa vile imetusaidia kupima na kuhukumu namna gani wahusika wa *Kiu na Kiu ya Haki* wanavyolandana na majina yao kupitia matendo, sifa zao, elimu zao, kujiamini kwao, maana ya majina yao, lugha yao, mahusiano na wahusika wengine, na mikabala yao.

### **2.11 Pengo la Utafiti**

Baada ya kuzipitia kazi za watafiti mbali mbali ambao wamewahi kufanya utafiti unaohusiana na utafiti wetu tumegunduwa kuwa hakuna utafiti wa kina uliofanyika unaohusu kuchunguza dhana zinazobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao katika vitabu vya riwaya za *Kiu na Kiu ya Haki*. Hivyo katika kazi hii

tulichunguza namna wahusika katika riwaya hizo walivyobeba dhana na zinavyolandana na majina yao ili kuziba pengo hilo.

### **2.12 Hitimisho**

Kazi tangulizi zilizosomwa na mtafiti zilimpa msaada mkubwa wa kuelewa msingi wa mawazo ya watafiti hao na jinsi ya kuweza kuziba pengo waliloliacha. Aidha, nadharia alizozitumia mtafiti zimeakisi lengo la utafiti huu na kuilinda kazi hii kutokana na uchambuzi wake. Kwa mfano kupitia nadharia ya Sosholojia mtafiti ameweza kuwalandanisha wahusika wa riwaya teuliwa na majina yao na jinsi walivyobeba dhamira mbali mbali kulinangana na mandhari waliyotokea ya kiusanii.

## SURA YA TATU

### 3.0 MBINU ZA UTAFITI

#### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ametaja na kufafanua mbinu zilizotumika katika kukusanya data. Aidha, sura imetaja muundo wa utafiti, sampuli na usampulishaji.

#### 3.2 Eneo la utafiti

Eneo la utafiti ni eneo la kijiografia ambapo mtafiti alikwenda kukusanya data. Hivyo, utafiti huu ulifanyika katika Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tawi la Pemba, Maktaba kuu Pemba, Maktaba ya chuo cha Ualimu cha W.B. Mkapa na maktaba ya Skuli ya Sekondari ya Fidel Castro za Pemba. Eneo hili limechaguliwa na mtafiti kwa sababu utafiti wetu ni wa maktabani na kwa sababu utafiti huu ulifanyika wakati shule ziko wazi na kwa vile mtafiti ni muajiriwa hakuwa na muda wa kwenda nje ya kisiwa cha Pemba na kwenda maeneo mengine.

#### 3.3 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Enon (1999:24), anaeleza kuwa muundo wa kimaelezo ni njia ya ukusanyaji na uchambuzi wa data kwa njia ya kimaelezo ambapo nambari huwa hazitumiki. Hivyo, data katika utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya maelezo.

#### 3.4 Uteuzi wa Watafitiwa

Utafiti huu ulichunguza dhana zilizobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao katika riwaya za *Kiu* ya Mohamed S. Mohamed na *Kiu ya Haki* ya Zainab M. Mwanga. Kazi hizo ziliteuliwa na mtafiti akiamini kuwa zitafikia madhumuni aliyoyakusudia. Aidha, mtafiti ailiteua riwaya hizi kutokana na kuwa

riwaya ya *Kiu* imetumia mandhari ya Zanzibar wakati ya *Kiu ya Haki* imetumia mandhari ya Tanganyika, hivyo aliamini kuwa atakuwa ameweza kuiwakilisha Tanzania mzima.

Sababu nyengine ni kuwa riwaya ya *Kiu* imeandikwa na mwandishi wa kiume wakati ya *Kiu ya Haki* imeandikwa na mwanamke, hivyo mtafiti aliamini kuwa atazingatia usawa wa jinsi zote mbili katika kutafiti mchango wao wa maarifa hasa katika uwanja wa mlandano wa wahusika katika fasihi ya kiswahili.

### **3.5 Usampulishaji**

Sampuli ni istilahi inayotumika kumaanisha watu walioteuliwa kujibu maswali ya utafiti kutoka katika kundi husika (Kothari, 1990). Naye, (Keys:1980), anafafanua kuwa sampuli na kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa katika kundi kubwa na kuwa ndio wakilishi wa kundi hilo lote.

Usampulishaji ni kitendo cha kuchaguwa au kupata kikundi fulani ili kuwakilisha kundi lengwa. Hivyo, katika utafiti huu mtafiti ametumia usampulishaji lengwa. Usampuli lengwa ni ule wa mtafiti wa kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data anazozihitaji. Pia ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huiteua akiwa na imani kwamba, itampatia data itakayomwezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake Newman ( 2006:22). Kwa msingi huu basi, sampuli lengwa hapa ni riwaya ya *Kiu* na *Kiu ya Haki* kama tulivyokwisha zitaja hapo awali. Mtafiti amezitumia hizi akiamini kuwa zitampa majibu ya maswali ya utafiti wake.

### **3.6 Mbinu za Kukusanyia Data**

Kothari (1990), anafafanua dhana ya ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika malengo yake ya utafiti. Aidha, Kothari anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji wa data. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya maktabani. Mtafiti alisoma vitabu teuliwa, makala, majarida na maandishi mengine yaliyompatia data za utafiti huu.

### **3.7 Mbinu ya maktabani**

Mbinu ya maktabani inahusu mapitio mbali mbali ya kazi zilizofanywa na watafiti waliotangulia kuhusiana na mada ya utafiti. Kazi hizo zinaweza kuhusu nadharia mbali mbali au hata uchambuzi wa dhana zinazohusiana na mada ya utafiti husika (Kothari, 1990). Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya maktabani. Mtafiti alisoma vitabu teuliwa, makala, majarida na maandishi mengine yaliyompatia data za utafiti huu.

### **3.8 Vifaa vya Utafiti**

Mulokozi (1983), anaeleza kuwa vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti, lakini aghlabu baadhi ya vifaa hivi kama si vyote hutumika, kalamu na karatasi, shajara ya uwandani, tepu rekoda na vifaa vyake, video/ kamrekoda na vifaa vyake, kamera na vifaa vyake, komputa na vikorokoro vyake, hojaji na dodoso, vifaa vya kupimia na kuhesabu, darubini, viona mbali nakadhalika. Katika utafiti huu mtafiti alitumia vifaa vya utafiti kama vile kalamu, karatasi, vitabu, majarida na komputa. Vifaa hivi vilitumika ili kukusanya, kuhifadhi data na kutayarisha data hizo.

### **3.9 Hitimisho**

Mbinu ya maktabani inahusu ukusanyaji wa data kwa kusoma kazi mbali mbali zinazohusiana na mada ya utafiti. Data za msingi zilikusanywa na mtafiti kwa kusoma kwa makini riwaya za *Kiu* na *Kiu ya Haki*. Kwa upande mwengine data zilikusanywa kutoka katika majarida, vitabu na tasnifu zenye mahusiano na kazi hii.

## SURA YA NNE

### 4.0 UCHAMBUZI WA DATA

#### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii zimechambuliwa data zilizokusanywa na mtafiti kutegemea malengo ya mtafiti. Data hizo zilikusanywa na kufanyiwa uchambuzi wa kimelezo na malengo ya utafiti yaliweza kufikiwa kama ilivyokusudiwa kama ifuatavyo:

#### 4.2 Ubainishaji wa Wahusika katika Riwaya ya *Kiu*

Katika kuchambua data zinazohusu dhumuni mahsusi hili mtafiti alibaini kuwa Riwaya hii ya *Kiu* imetumia aina zote tatu za wahusika ambao aliwafanyia uchambuzi kama wafuatavyo.

##### 4.2.1. Wahusika Wakuu

Wahusika wakuu hujitokeza mwazo hadi mwisho wa kazi ya fasihi. Pia wahusika hao hubebishwa dhamira kuu za mwandishi. Aidha, mhusika mkuu ni muhimili na mweka wa kazi ya kifasihi ambapo wahusika wengine kwa kawaida huhusishwa na mhusika mkuu.

Riwaya ya *Kiu* imemtumia mhusika Bahati, Idi na Mwinyi kama wahusika wakuu katika kazi hiyo. Wahusika hawa waliweza kufanyiwa uchambuzi na mtafiti kama ifuatavyo:

##### 4.2.1.1 Bahati

Mhusika Bahati ni mtoto wa Mzee Jaku na Bi Cheusi. Bahati ni mhusika mkuu wa riwaya hii. Bahati amejitokeza mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Matukio na visa mbali mbali vinamuhusu yeye kiasi kwamba angelikuwa hayupo katika hadithi basi pia hadithi isingelileta maana iliyokusudiwa na mwandishi.



Msanii amemuonesha Bahati tangia bado ni msichana mdogo mwenye umri wa miaka kumi na nne akiishi pamoja na mama yake. Bahati anakutana na Idi na kuwa chanzo cha kupendwa na Idi pamoja na Mwinyi. Maisha ya Bahati katika ndoa yake na Idi yanatawaliwa na vituko, maudhi na huzuni. Bahati pia anakutana tena na Mwajuma akiwa kama mfanyakazi wake wa ndani ya nyumba na baadaye anakuwa mshauri wake mkubwa katika maisha yake ya ndoa hadi kuvunjika kwa ndoa yake na Idi. Baadae, Bahati anarejea tena kwa mama yake huko Selea na kuishi pamoja ambapo mwisho anapotea katika mazingira ya kutatanisha. Mtafiti aligundua kuwa, Bahati ni mhusika mkuu kwani tangu mwanzo hadi mwisho anatumiwa na mwandishi katika kujenga matukio na visa mbali mbali vinavyosukuma mbele kazi hiyo.

#### **4.2.1.2 Idi**

Ni kijana, dereva wa Mwinyi, mlevi, mwongo na mwenye ari na huruma, ni dhalimu anamdhulumu tajiri yake mali kwa kumdanganya kuwa Bahati anampenda na hatimaye anamuoa yeye. Idi pia ni mhusika mkuu katika riwaya hii kutokana na kubebeshwa dhima kubwa na mwandishi wa riwaya ya *Kiu* mwanzo hadi mwisho. Kama alivyo Bahati, Idi ukimuondoa katika riwaya, lengo la mwandishi litafifia na hata kukosekana kabisa.

Idi anamuoa Bahati, lakini anaonekana kutomthamini kwa kufanya mapenzi na wanawake wengine nje ya ndoa na hata kudiriki kuwaleta ndani ya nyumba yake. Pia, kauli zake kwa Bahati ni za kukatisha tamaa, jeuri na zilizosheheni matusi. Idi anamuacha Bahati na huo ndio unakuwa mwisho wa ndoa yao. Vile vile, Idi anamtumia Bahati barua kwa lengo la kukaa na kujadili juu ya kugawana mali

walioipata kutoka kwa Mzee Mwinyi, na matokeo yake huo ndio unakuwa mwisho wa maisha yake.

#### **4.2.1.3 Mwinyi**

Ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Kiu*. Yeye ni tajiri mwenye tabia ya umwinyi (kufanyiwa kila jambo na watu wengine). Aidha, anamtegemea Idi ili azungumze na Bahati kuhusu suala lake la ndoa yake na Bahati. Pia, anaendeshewa gari na Idi. Vilevile ana mtumishi katika nyumba yake ambaye ndiye anaemhudumia kwa chakula, usafi wa nyumba na mambo mengine madogomadogo. Mwinyi anatumiwa na Mwandishi kujenga dhamira za mapenzi, ndoa, dhuluma ambazo pia zinatokea kwa wahusika Bahati na Idi.

### **4.3 Wahusika Wasaidizi**

Wahusika wasaidizi waliojitokea walifanyiwa uchambuzi na mtafiti kama ifuatavyo:

#### **4.3.1 Cheusi**

Ni mama yake Bahati. Cheusi ana mapenzi na huruma na mtoto wake. Ni mama mwenye msimamo katika malezi unozingatia utamaduni wa kiislamu. Siku zote anapingana na fikra na maamuzi ya Bahati ya kushirikiana na Idi katika maisha ya dhulma na pia yanayokwenda kinyume na utaratibu wa ndoa za Kiislamu. Kwa mtazamo wake anaona kuwa kila jamii ina mila na desturi zake ambazo zinapaswa kufuatwa na wanajamii kwa lengo la kujenga mustakbali bora katika maisha ya kila siku juu ya mambo kama vile mavazi, ndoa, malezi na mengine. Kwa mfano msanii anaeleza:

“Mame mtu alifuta machozi kwa ncha ya kanga ili amuone vyema mwanawe anayeshtakia hali yake. Unampenda kijana mmoja, na kijana mwenyewe ni nani?...”

.....Idi, Idi ndiye anayekuhangaisha? Ah, mwanangu we, umepata kuona wapi mambo kama hayo kufanywa na mtu Islamu?. Unaiga uzungu, uzungu unakuhusu nini?” Cheusi alimwuliza kwa hasira. (uk:25).

Cheusi, pia ni mhusika anaendeleza mila za ushirikina katika maisha yake. Anamzinguwa mwanawe baada ya kupokea posa kutoka kwa Idi, ili asidhurike na maadui (uk:62).

Cheusi anaishi na mwanawe tu baada ya mumewe kuelekea Kongo. Maisha yake yanakuwa magumu hata hivyo, anajishughulisha na biashara ya maandazi ili kupunguza ukali wa maisha (uk:28).

Kutokana na hali hii, Cheusi anatumiwa na mwandishi kuwajenga wahusika wakuu hasa Bahati na Idi na kupelekea kusawiri vyema kwa dhamira za ndoa, na malezi. Cheusi pia anasaidiana na Bahati na Bimvita ili kuibua dhamira za mwandishi.

#### **4.3.2 Mwajuma**

Mwajuma ni mtumishi wa nyumbani kwa Mzee Mwinyi, mwenye nidhamu na hodari wa kazi. Hata baada ya kutoweka Idi, Mwajuma aliendelea kuishi na Mwinyi na kumsaidia kwa nguvu zake zote bila kuonesha kuchoka wala kukimwa. Mwandishi anasema:

“Baada ya kutoweka kwa Idi, Mwinyi hakuwa na msaidizi mwengine  
ila mtumishi wake Mwajuma...”(uk:72).

Pia, Mwajuma anamhurumia Bahati kutokana na hali ya ndoa yake na Idi. Daima alionekana kumliwaza na kumhurumia Bahati. Msanii anadokeza hilo kwa kusema: Twende tukatembee bustanini .....(uk:73).

Aidha, Mwajuma ni msichana mkweli na mwazi, anamueleza ukweli Bahati kuhusu tabia ya mumewe (Idi), aifanyayo wakati Bahati akiwa ameondoka nyumbani. Idi aliendeleza tabia yake ya kuleta wanawake na kufanya nao mapenzi katika chumba kile kile cha Bahati, huku akitoa matusi na dharau dhidi ya Bahati pamoja na kunywa pombe. Kutokana na tabia yake hiyo, Mwajuma anamshauri Bahati kudai haki yake ya talaka.

“Kuwa mimi ni mke ningemstahamia mume wangu kwa yote  
ispokuwa kunila kivuli.....lakini kunizinia nyuma yangu, akanifanya  
mimi si mwanamke kitu baada ya kunichagua mwenyewe; hilo  
nisingelikubali. Bora niishi mjane kuliko kuishi na mume kama huyo”  
(uk. 110).

Mwandishi anamtumia Mwajuma kama mhusika msaidizi kwa jinsi anavyoendelea kushirikiana na Bahati kumsimulia visa vya Idi avifanyavyo anapokuwa hayupo pale nyumbani kwake, huku akimlaumu Bahati kwa tabia yake ya ustahamilivu ulichupa mipaka kususuri kuridhia vituko hivyo. Kupitia muongozo anaoupata Bahati, kutoka kwa Mwajuma, Bahati anasawiri dhamira ya ukombozi, ujasiri na ukweli.

#### **4.4 Wahusika Wajenzi katika Riwaya ya *Kiu***

Mtafiti baada ya kuchambua data aliweza kugundua kuwa wahusika wajenzi wametumiwa na msanii wanavyowajenga wahusika wakuu na wasaidizi . Aidha wametumiwa kama daraja la kufikia malengo ya mwandishi anayoyawasilisha kwa jamii. Wahusika hao walifanyiwa uchambuzi na mtafiti kama wafuatavyo:

##### **4.4.1 Jaku**

Huyu ni mume wa Cheusi na baba yake Bahati. Ni masikini, anamuachia ulezi mkewe Cheusi wa mtoto wao Bahati na kuelekea Kongo (uk:28). Msanii anamjaalia Jaku katika kumjenga Cheusi ili kuibua dhamira ya malezi na umasikini uliokithiri kwa Cheusi.

##### **4.4.2 Kidawa**

Ni shoga yake Bahati, ni mke wa Makame, ni mwenye tabia ya umbeya, hapendi tabia ya mume wake ya wivu usio na msingi. Kwa mfano mwandishi anasema:

“...nikwambie nini mambo ya bwana huyu! nikueleze kutwa hayeshi na utoshe huo wivu aliokuwa nao; na litoshe hilo domo lake. Si nguo si kula, yeye mwambie wivu na hamaki tu, basi!” (uk:58).

Kwa ujumla, mwandishi anamtumia Kidawa kuendelea kukamilisha dhamira yake ya ndoa na matatizo yake.

##### **4.4.3 Tatu**

Tatu ni shoga wa Kidawa, na ni mke wa Ali, ambaye anatoka katika familia ya kitajiri. Pia, ni msomi. Pia, Tatu ana matatizo katika ndoa yake. Kwa mfano, katika (uk. 60-61), mwandishi anasimulia:

“...nina mume jina tu, sijui njaa yake, sijui shibe yake, wala siyajui matembezi yake. Hivi ninavyokwambia, basi sijamuona machoni leo ya tatu” (uk. 60-61).

Kama alivyo Kidawa, msanii amentumia Tatu kujenga na kukamilisha dhamira ya ndoa na matatizo yake.

#### **4.4.4 Makame**

Makame ni mume wa Kidawa, ni mwenye wivu wa kupindukia uliochanganywa na bughuza katika ndoa yake ambao unamfanya Kidawa kuchukia maisha ya ndoa. Msanii ameeleza:

.....kitu kinachonikera zaidi ni wivu wake tu, si wivu aliojaaliwa bwana huyu. Hivi sasa sijui kama hayuko darini anatusikiliza, nikitoka nje kaniganda, nikiingia ndani yuko nyuma, nikiulizwa hujambo, vita, nikizungumza na mtu yumo pembeni anasikiliza! mradi sina raha. (uk. 58-59).

Mtafiti ameona kuwa, Makame ni mhusika anayehusishwa na maelezo ya Kidawa ili kumjenga Bahati ambaye naye anakumbwa na tatizo la ndoa.

#### **4.4.5 Ali**

Ni mume wa Tatu, ni mlevi asiemjali mke wake kwa kutembea na wanawake wengine wa nje ya ndoa yake. Msanii amentumia Ali kujenga dhamira ya ulevi, ambayo pia dhamira hii inasjitokeza kwa mhusika Idi. Vilevile, Ali anaendeleza kuakisi na kujenga dhamira ya ndoa na athari zake kupitia ndoa yake na Tatu. Mwandishi anatusimulia hili kama ifuatavyo:

“...aniage mimi ? he- ee! siku hizi yeye na ulevi na wanawake tu, basi. Litazame hili jumba toka huku mpaka kule, nakaa peke yangu mtoto mdogo kama mimi, usiku kucha nasoma dua naomba atokee... (uk:61).

Dondoo hili linatudhirishia namna mhusika Ali alivyotumika kumjenga Tatu kutokana na uoza wa ulevi unaomsababisha kuijutia ndoa yake.

#### **4.4.6 Bi Mvita**

Huyu ni miongoni mwa wahusika wajenzi walio muhimu sana katika riwaya ya Kiu ya Mohammed S. Mohammed. Huyu ni somo yake Bahatia (aliyempa mafunzo alipovunja ungo). Bi Mvita ni mhusika anayetetea na kuendeleza utamaduni wa ndoa za kale zenye kujali maadili ya jamii ya Kizanzibar. Pia, huyu ni mhusika mwenye mawazo na mipango mizuri. Fikra zake zinamfanya Cheusi asipate tabu ya kuendesha shughuli ya arusi ya mtoto wake. Ni mkweli na mwazi. Pia, ni mwenye kujiamini katika kutenda mambo na kutoa maamuzi. Msanii amemtumia kuendeleza na kukamilisha dhamira ya utamaduni, hasa utamaduni wa ndoa kwa kumjenga mhusika Bahati katika maswala ya Kiutamaduni, kwa kumpa mafunzo kupitia unyago siku ya harusi yake. Kwa mfano, mwandishi anasema:

“...Bi Mvita alipenda kuendesha arusi kwa mila za zamani za Kiswahili, ambazo zilihitaji mambo mengi ya kufanya....Bahati aliambiwa kwa mkato kuwa jioni atakoshwa kwa unyago.” (uk: 69-70).

#### **4.4.7 Sihaba**

Ni mtoto wa Bi Mvita. Tunaelezwa kuwa, Cheusi anakwenda nyumbani kwake ili ampigie simu mama yake, ili, ahudhurie katika harusi ya Bahati. Yeye anatumiwa

na mwandishi kumjenga Bahati katika kufanikisha kupatikana kwa taarifa za Bi Mvita ambaye ni mtu muhimu katika shughuli ya harusi ya Bahati.

#### **4.4.8 Majirani**

Salama, Mwandawa, Riziki na Bi Mtawa ni majirani na marafiki wa Cheusi, wanatumiwa na msanii kushirikiana na Cheusi ili kumjenga mhusika Bahati katika kufanikisha harusi yake. Wahusika hawa wanachorwa kuwa na sifa ya ujirani mwema.

#### **4.4.9 Bi Somo**

Mhusika huyu ni jirani wa Cheusi na mwalimu wake Bahati wa chuoni (qur ani). Anaungana na Cheusi, Mwandawa, Salama, Riziki na Bi Mtawa kukamilisha ujenzi wa mhusika Bahati kama mhusika mkuu.

#### **4.4.10 Binti Songoro**

Ni jirani yake Cheusi, anamuazima nyumba yake ili kufikia wageni wa Cheusi wanaohudhuria sherehe ya arusi ya Bahati, msanii anaeleza:

“Ndugu yangu unifae kwa langu nikufae kwa lako; wageni wamezidi, nataka uniazime nyumba yako,” alisihi.

“Ah, mpenzi wangu we, nyumba gani hii ya kukaribisha wageni? alijibiwa .

“Haidhuru, dada kupata si kukosa; sina la kufanya”

“Haya basi, wakaribishe ngoja nifagie kidogo”(uk:65).

Dondo hili, limetumika kumuonesha namna mhusika Binti Songoro alivyotumika kumjenga mhusika Bahati ili kuonesha umasikini ulioikumba familia ya mhusika huyo.



#### **4.4.11 Binti Jaku**

Ni wifii yake Cheusi. Anashirikiana na Cheusi katika harusi ya mtoto wao. Huyu ni mhusika mjenzi kutokana na kumjenga Cheusi na Bahati ili kufanikisha dhamira ya ndoa.

#### **4.4.12 Hadija**

Hadija ni mtoto wa mama yake mdogo Cheusi. Kama walivyokuwa Binti Jaku, Binti Mvita na yeye pia anashirikiana na Cheusi katika kufanikisha sherehe ya arusi ya Bahati.

#### **4.4.13 Baraka**

Huyu ni shehe aliyefungisha ndoa ya Bahati na Idi. Ni mrefu mwenye tambo la kugozana. Sheikh Baraka pia anatumika kuandika talaka ya ndoa ya Idi na Bahati. Mwandishi anamtumia kukamilisha suala zima la ndoa na talaka. Hivyo, mhusika huyu anatumika kumjenga mhusika Bahati na Idi katika swala la kufunga ndoa na kuvunja ndoa yao. Kwa mfano;

“Punde, aliwasili shekhe Baraka, muozaji mashuhuri,....alikalialia mkeka, akatoa saa yake yenye mkufu wa fedha, ambayo siku ya mavuno kama hii huirekebisha mapema.....na pale katika moshi wa udi na ubani, mbele ya shekhe na waliohudhuria, Idi alikula kiapo cha ndoa. Papo hapo, Idi na Bahati wakawa mke na mume”. (uk. 71).

#### **4.4.14 Muuza Samaki**

Huyu ni mfanya biashara ya kuuza samaki, ana mazoea na Cheusi kutokana na biashara yake baada ya kuwa ni mnunuzi wake. Pia, mhusika huyu anatumika

kumjenga mhusika Cheusi. Msanii anatubainishia mazoea kati ya Cheusi na muuza samaki kama ifuatavyo:

“Punde alisikia sauti ya mchuuza samaki, akachukua sahani ya bati chanjani, akajitanda kanga , na kwenda kupokea kitoweo”.

“Haa! Mwenye samaki alicheka na kufunua kinnywa chake chenye meno yalioachana yenye tabaka ya ukoko wa rangi ya kahawia. “Leo mambo! Chagua samaki umtakea, kimwana!” (uk. 34)”.

#### **4.4.15 Awadhi**

Ni mshihiri mwenye biashara za mkahawa, ana tabia ya kuchukua maandazi kwa Cheusi na kuweka katika mkahawa wake. Mhusika huyu anahusishwa na Cheusi ili kumjenga katika kukamilisha dhamira ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Mhusika huyo anaonesha namna mwanamke leo hii anavyoshiriki katika biashara ndogo ndogo ili kuihudumia familia yake. Mwandishi anatueleza:

“Sauti kutoka jikoni ikajibu, mwambie apite hapo kwa Awadhi, huyo Mshihiri mwenye mkahawa ninapoweka maandazi yangu, amwambie ampe shilingi moja katika hesabu ya maandazi ya leo” (uk: 34).

#### **4.4.16 Mcha**

Rafiki yake Idi aliyemkopesha sh 1500/-, anumika kumjenga mhusika mkuu Idi. Mwandishi anaonesha namna Idi baada ya kupata pesa alivyokuwa akikaa na kufanya hesabu juu ya pesa alizonazo na zile anazowadai watu wengine. Msanii anatueleza kwa kusema:

“Halafu, elfu mbili alizokuwa nazo mfukoni, na elfu moja na mia tano, alizomkopesha rafiki yake Mcha”. (uk. 50)”.

#### **4.4.17 Rehema binti Mwinyi**

Huyu ni mtoto wa marehemu Mzee Mwinyi anaishi Ulaya, ni msomi ametajwa kuwa ndiye mrithi pekee wa marehemu baba yake, anaandikiwa barua na Mwajuma kupewa taarifa za kifo cha baba yake. Mhusika huyu anachorwa na mwandishi ili kumjenga mhusika Mwinyi, kuonesha taarifa zake kuhusu kizazi. kwa mfano:

“Baada ya mazishi, ilikabidhiwa serikali kungojea warithi. Mali hii ilikuwa lile gari, vyombo vya nyumbani, nyumba yenyewe, shamba na kila kilichokuwa mali yake...Alipofika kwao tu alifanya wajibu wake wa mwisho wa kumuandikia barua Rehema binti Mwinyi kumwarifu kifo cha baba yake.” (uk. 79)”.

#### **4.4.18 Rehema**

Huyu ni hawara wa Idi. Anafanya mapenzi katika chumba cha Bahati. Ni mlevi, mjuvi na mwenye lugha ya matusi. Mhusika huyu anahusishwa na mhusika Idi ili kumjenga Idi kuonesha dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa yaliyokithiri miongoni mwa wanajamii pamoja na wanandoa wasiokuwa waaminifu. Msanii anatubainishia hili kwa kusema:

“ Aliruka akafyatuka mpaka chini ya ukuta wa nyumbani kwake na kuchungulia. Yule pale mumewe! Yule pale hawara wake! Wamekaa kando ya meza kati ya uwanja. Yule mwanamke kamuegemea mumewe! Mwanamke mwembamba, mrembo, mwekundu, mwenye

nywele za kuchoma zilizotolewa shungi kubwa utosini. Mkono mmoja wa mumewe, Idi ulikuwa umeganda kwenye kiuno cha mrembo, na wa pili akimiminia mvinyo katika bilauri mbili.” (uk. 120)”.

#### **4.5 Ubainishaji wa Wahusika katika Riwaya ya *Kiu ya Haki*.**

Baada ya kuchambua data zinazohusu kubainisha wahusika katika riwaya ya *Kiu*, mtafiti alichambua data zinazohusu ubainishaji wa wahusika waliomo katika riwaya ya *Kiu ya Haki*. Wahusika hao walifanyiwa uchambuzi na mtafiti kama ifuatavyo:

##### **4.5.1 Wahusika Wakuu katika *Kiu ya Haki***

Wahusika wakuu waliojitokeza walifanyiwa uchambuzi na mtafiti kama ifuatavyo:

##### **4.5.1.1 Mzee Toboa**

Ni mhusika anayependa haki, dereva wa taksi, mwaminifu, mzalendo na mwenye kuelewa mambo mengi ya nchi yake. Mzee Toboa, ndiyo nguzo ya riwaya hii. Anatumiwa na mwandishi kupambanishwa na Sikujua katika mkasa wa mauaji ya Pondamali Malipesa, ambayo yaliyofanywa na Sikujua. Toboa baada ya kupata taarifa za kutosha kuhusu mauaji ya Pondamali anaamua kutoa taarifa Polisi ili haki itendeke. Kwa mfano, tunaelezwa na mwandishi kuwa:

“baada ya kusalimiana, Mzee Toboa hakupenda kupoteza muda, hivyo alimueleza Paukwa kilichompeleka ofisini mwake asubuhi ile. Alimtobolea kisa chote cha kifo cha Pondamali kama alivyoelezwa na Sikujua”(uk:39).

Katika harakati za kesi zikiwa zinaendelea Inspekta Paukwa anapata safari na kumkabidhi Inspekta Pwagu jukumu la kusimamia kesi hiyo. Toboa, anasalitiwa na

Pwagu na kujikuta anaingia katika kipindi kigumu, anatiwa pingu na kupelekwa Polisi kwa uchunguzi zaidi, kwa mfano, tunaelezwa na mwandishi kama ifuatavyo:

“NIAMBIENI makosa yangu! nchi hii mnawafunga pingu hata watetezi wa haki? Allah Akbar! uhuru gani huu? mnipitisha nyumbani angalau nikamwaga mke wangu,” Mzee Toboa bin Mambo alikuwa akilalamika ndani ya gari la Polisi ambalo....”( uk:1).

Hata hivyo haki inapatikana, mahakama inamuadhibu Sikujua kwa kunyongwa na kufariki, majambazi yanafungwa jela miaka mitatu na Fundisha na mke wake wanatozwa faini kwa kuficha ukweli. Mzee Toboa anapata heshima yake kama raia mwema. Kwa mfano tunaelezwa na mwandishi:

“ Mahakama inamwachia huru Mzee Toboa baada ya kuridhika na ushahidi wake..... Mzee Toboa ni mfano bora wa raia mwema. Mfano wake mwema uigwe na raia wengine, sina shaka serikali itafikiria tunu kwa Mzee Toboa”( uk:89).

#### **4.5.1.2 Sikujua**

Huyu ni rafiki wa Pondamali, na ni dereva wa teksu, anamuua rafiki yake kwa sababu ya fedha na mapenzi. Sikujua anafanya mauaji bila kufikiri baadaye anajuta. Kwa mfano msanii anatueleza mkasa huo kwa kusema:

“ ...aliniambia eti mke wangu kamfilisi. Kila siku alidai fedha na starehe zingine ambazo zilimfanya ashindwe kuweka fedha na kwamba muda wake mwingi wa kazi alikuwa akiupoteza kwa mke wangu mimi niwapo kazini, mimi kusikia hivyo damu ilinichemka,

mapigo ya moyo yalibadilika mwendo, nikajisikia nakosa pumzi!  
 ...tulipeana makonde hadi nilimpomshinda nguvu na kumwangusha  
 chini. Nilimkalia tumboni, nilimkaba koo mpaka akakata roho”  
 (uk:28).

Baaada ya mauaji, Sikujua anakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria na hatimaye anahukumiwa kunyongwa hadi kifo chake. Tunaelezwa na mwandishi kama ifutavyo:

“Sikujua amepatikana na hatia ya kuuwa kwa makusudi. Mahakama hii haina adhabu nyingine ya kumpa bwana Sikujua bali, adhabu ya kunyonga hadi afe!” (uk:90).

#### **4.5.2 Wahusika Wasaidizi katika Riwaya ya Kiu ya Haki**

##### **4.5.2.1 Pondamali**

Pondamali ni rafiki wa Sikujua, ambaye alikuwa anafanya kazi ya udereva wa tekisi kama alivyokuwa Sikujua. Pondamali anahusiana kimapenzi na mke wa Sikujua. Baada ya kuyateka majambazi wanagombana na Sikujua kuhusu kugawana fedha. Pondamali anakasirika na kutoa siri ya mahusiano yao na mke wa rafiki yake. Hiyo, ndiyo inakuwa sababu ya kifo chake.

Pondamali, anatusaidia katika kuwaelewa wahusika wakuu hasa Mzee Toboa na Sikujua kutokana na kwamba mkasa wote wa hadithi umemuhusu yeye licha ya kuwa anafariki mapema, lakini hatuwezi kuacha kumzungumzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya.

#### 4.5.2.2 Mke wa Sikujua

Huyu anafanya mapenzi na Pondamali, ana tabia ya kupenda umbeya, apigwa na mume wake baada ya Sikujua kupata taarifa za mahusiano yao na Pondamali. Pia anatoa siri ya mauaji ya Pondamali na kumpa shoga yake (Mke wa Fundisha). Kwa mfano, tunaelezwa na msanii:

“Siku ya Jumamosi alipokuwa nyumbani kwa marehemu kuhudhuria msiba, Mke wa Sikujua alikuwa alitoa siri ya mumewe kwa jirani yake, Mke wa Fundisha. Mke wa Sikujua alikuwa anamwamini sana jirani yake...” (uk:13).

Pia, Mke wa Sikujua anashirikiana na mumewe ili wantumie Inspekta Pwagu awasaidie katika kesi ya mauaji. Hivyo, anakwenda kwa Mke wa Fundisha kukopa pesa ili watoe hongo kwa Jaji Pwaguzi, kama tunavyoelezwa:

“.....Alimwomba mkewe akope pesa kwa jirani yao, Mke wa Fundisha. Alimfahamisha mkewe kwa juu o pesa alitaka ampe Inspekta Pwagu na Jaji Pwaguzi ili wamsaide katika kesi, kwani Mzee Toboa alikwisha mchongea..” (uk:54).

#### 4.5.2.3 Mzee Fundisha

Huyu ni mzee wa Kimanga anaefanya kazi ya kuuza mkahawa. Anaelewa taarifa kuhusu mauaji ya Pondamali alizozipata kutoka kwa mke wake. Lakini anakuwa mwoga, kutoa taarifa hizo Polisi kwa kuchekelea kupata usumbufu. Aidha, Fundisha ni rafiki wa Mzee Toboa, mwisho anakuwa shahidi wa Toboa mahakamani lakini, mahakama inamtoa faini ya shilingi 300/- kwa sababu ya

kuficha ukweli aloujua tangu zamani kuhusu mauaji ya Pondamali. Kwa mfano, mwandishi anaeleza:

“....Mzee Fundisha na mkewe wanatozwa faini ya shilingi 300/= kila mmoja kwa kosa la kumficha muuaji. Vilevile wanapongezwa kwa ushahidi wao nzuri uliowezesha Mahakama kumjua muuaji...”  
(uk:89).

#### **4.5.2.4 Mama Fundisha**

Ni mke wa Mzee Fundisha, pia ni shoga yake Mke wa Sikujua ambaye anapata habari za mauaji ya Pondamali kutoka kwa shoga yake ile siku ya kilio cha Pondamali. Mama Fundisha anakuwa mwoga kupeleka habari hizo Polisi badala yake anampa mumewe habari hizo za mauaji.

Kwa mfano tunaelezwa na mwandishi:

“Siku ya Jumamosi alipokuwa nyumbani kwa marehemu kuhudhuria msiba, Mke wa Sikujua alitoa siri ya mumewe kwa jirani yake, Mke wa Fundisha.....hivyo alimpa siri hiyo bila ya wasiwasi baada ya Mke wa Fundisha kumuuliza kisa cha kuvimba uso na mkono. Mke wa Fundisha alimpa siri hiyo mumewe, Mzee Toboa siri hiyo siku ya Jumapili alipokwenda kunywa kahawa” (uk:13).

#### **4.5.2.5 Inspekta Paukwa**

Mhusika huyu ni Ofisa wa Polisi aliyepewa kibali cha kuendesha kesi Mahakama Kuu. Ni mhusika anayehusika na upelelezi wa kesi ya mauaji ya Pondamali. Pia, Inspekta Paukwa anapewa taarifa za Mzee Toboa. Wakati wa kesi, anapata safari



na kumkabidhi Jaji Pwagu kusimamia kesi hiyo ya mauaji kama tunavyoelezwa na msanii.

“Wakati upelelezi wa kesi unaendelea, Inspekta Paukwa alipata safari ya ghafla. Alimkabidhi Inspekta Pwagu jalada la kesi...” (uk:44).

Inspekta Paukwa baadaye anarudi na kulazimika kuwa Wakili wa kesi hii baada ya Inspekta Pwagu na Jaji Pwagu kula rushwa. Ambapo msingi wa kazi hii uliwalazimisha kutoendelea.

Paukwa ni ofisa anaeipenda kazi yake na anayeifanya kwa uaminifu. Mwandishi amemchora kuwa mhusika wa kuweza kuigwa.

#### **4.5.3 Wahusika Wajenzi katika ya Kiu ya Haki**

##### **4.5.3.1 Jaji Pwagu**

Ni ofisa wa polisi mwenye shahada ya sheria ya chuo kikuu. Anapewa kibali maalumu na serikali cha kuendesha kesi katika Mahakama Kuu kutokana na upungufu wa majaji uliokuwepo.

Ni mhusika anayetawaliwa na tamaa mbaya ya kupata fedha kwa njia zisizokuwa za halali. Anaamua kuchukuwa hongo kutoka kwa Sikujua baada ya kukabidhiwa kuendesha kesi ya mauaji ya Pondamali yaliyofanywa na Sikujua.

Aidha, baadae serikali inamzuilia kuendelea kuwa Jaji katika kesi hii baada ya kupatikana na tuhuma za kula njama za kumzamisha Toboa katika kesi ya mauaji ya Pondamali kwa kuchukua hongo ya shilingi laki moja kutoka kwa Sikujua. Mwandishi anatubainisha haya kwa kusema:

“Mahakama ilikutana tena tarehe 14 Agosti kusikiliza kesi ya mauaji ya Pondamali Malipesa. Jaji Utakunywa ndie aliechaguliwa kusikiliza kesi hii badala ya Jaji Pwaguzi, kwa upande wa mwendesha mashtaka wa pili, Inspekta Paukwa aliwajibika kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Inspekta Pwagu ili asaidiane na Wakili Mtayaona” (uk.83).

#### **4.5.3.2 Jaji Pwaguzi**

Huyu naye ni ofisa wa Polisi anayeendesha kesi ya mauaji ya Pondamali. Anashirikiana na Jaji Pwagu kuchukua hongo kutoka kwa Sikujua ili wamsaidie katika kesi yake ya mauaji.

Anafanya kazi kwa misingi mibovu ya kutokuzingatia kanuni na maadili ya kazi yake. Jaji Pwagu anasitishwa kuendelea kusimamia kesi ya mauaji ya Pondamali kutokana na tuhuma za kuchukua fedha kutoka kwa Sikujua. Mhusika huyu anatumiwa na mwandishi ili kumjenga Sikujua katika kufanikisha dhamira ya rushwa.

#### **4.5.3.3 Mtayaona**

Ni wakili wa Mahakama Kuu, anayeendesha kesi ya mauaji ya Pondamali, anafanya kazi yake kwa misingi ya haki na uadilifu. Anashirikiana na Jaji Utakunywa na Inspekta Paukwa kuendesha kesi ya mauaji ya Pondamali. Mtayaona anatumika kujenga dhamira ya haki.

#### **4.5.3.4 Utakunywa**

Yeye ni Jaji wa Mahakama Kuu anayesimamia kesi ya mauaji ya Pondamali akishirikiana na Wakili Utakunywa na Inspekta Paukwa. Mhusika huyu ni

mwadilifu katika kazi yake. Pia, anaelezwa kutokuwa na upendeleo, ndiye aliyetoa hukumu ya kesi ya mauaji ya Pondamali. Kwa mfano, tunaelezwa:

“...baada ya kuchambua maelezo kutoka kwa washtakiwa wote na ushahidi ulotolewa, sasa natoa adhabu kwa wenye hatia,” aliendelea Jaji Utakunywa... Somba, Killa na Kazamoyo wanahukumiwa kifungo cha miaka mitano na kazi ngumu kwa kila mmoja kwa kosa la ujambazi (uk. 89).

#### **4.5.3.5 Somba**

Ni jambazi, anayeshirikiana na Kila na Kazamoyo kuwateka nyara Sikujua na Pondamali na kuwanyang'anya fedha na saa ya mkononi. Pia, baada ya siku kadhaa wanakwenda kuiba tena nyumbani kwa Sikujua na kusomba fedha zote alizokuwa nazo Sikujua.

#### **4.5.3.6 Killa**

Kama alivyo Somba, Killa ni jambazi anayetumia silaha ya moto (bastola), kuwateka nyara Sikujua na Pondamali. Kila ni jambazi katili, anakamatwa na kupelekwa mahakamani na kufungwa miaka mitatu jela na kazi ngumu.

#### **4.5.3.7 Kazamoyo**

Anashirikiana na Kila na Somba katika shughuli za ujambazi. Kazamoyo ni katili, baada ya kukamatwa na Polisi na kupelekwa Mahakamani anahojiwa, baadaye anaukaza moyo wake na kuongea ukweli kuhusu kuteka nyara gari za Sikujua na Pondamali. Pia, Kazamoyo anafungwa jela pamoja na Killa na Somba. Wanatumiwa na mwandishi kujenga dhamira ya ujambazi na wizi.

#### 4.5.3.8 Swalehe

Huyu ni mtoto wa Mzee Fundisha. Ni mwaminifu, anamsaidia baba yake kuuza mgahawa, pia alimsaidia Mzee Fundisha kupokea fedha siku amabayo Polisi walipokwenda kumuhoji kuhusu biashara yake. Msanii anaeleza:

“Dakika moja kwanza, mabwana,” aliitika Mzee Fundisha huku wasiwasi ukimwiingia. Alimkabidhi mwanawe Swalehe kazi ya kupokea pesa, akatoka nje.” (uk.7).

#### 4.6 Kuchambua Mlandano wa Majina ya Wahusika katika Riwaya Teuliwa

Dhana ya kulandana kwa wahusika na majina yao ni jinsi wahusika hao wanavyopatiwa majina kutegemea maumbile yao, mienendo na tabia zao, lugha zao, vionjo vyao, uhusiano wao na wahusika wengine, hisia zao kwao wenyewe, mazingira na mandhari yao, kiwango chao cha elimu, jamii yao na kadhalika (Wamitila, 2002).

Baada ya kukusanya data, mtafiti alizichambua na kugundua kwamba, kwa kiasi kikubwa wahusika katika riwaya teule wametumia mbinu kadhaa zinazosawiri majina yao. Hivyo, data hizo zilionesha kuwa, kuna uhusiano wa wahusika na majina yao, kutegemea mbinu anuai. Data hizo zilifanyiwa uchambuzi na mtafiti kama ifuatavyo:

##### 4.6.1 Mbinu ya Uzungumzi Nafsi wa Ndani

Katika riwaya ya *Kiu*, mbinu ya uzungumzi nafsi wa ndani imetumiwa na mwandishi kumuelezea mhusika Bahati. Mwandishi amemuonesha Bahati akizungumza na nafsi yake juu ya sababu iliyomfanya Idi akasirike na kuchanganyikiwa mara Bahati alipokataa maelezo ya Idi ya kumtaka afanye

mahusiano ya kimapenzi na Mzee Mwinyi, ili kupata mali kutoka kwa Mzee Mwinyi. Kwa mfano:

“Ingawa Bahati alimtupia Idi jicho la hasira, moyoni alitarajia kwamba lingetokea jambo baya. Kwa hivi aliona hofu na kutetemeka maana hakupata kumuona Idi amesawijika vile. Je, ni maumivu tu ya majaraha aliyokwishampa, au ni ishara ya kuwa jambo jengine lingetokea? Pengine, aliwaza ...” (uk.19).

Aidha, mbinu hii imetumika kumsawiri Bahati kutokana na historia ya hali yake ya maisha iliyokuwa imegubikwa na dimbwi la umaskini. Mwandishi anajaribu kudokeza namna Bahati yeye mwenyewe alivyokuwa anajua kwamba, yuko katika hali hiyo. Ingawa mwisho anaonekana akipata bahati ya kuondokana na umaskini kama miujiza fulani. Mwandishi anatueleza kwa kusema:

“Bahati kwa mara ya mwanzo katika maisha yake alihisi umaskini, sasa alijijua kuwa yuko katika hali mbaya ya umaskini; ndie yeye mpigana na tumbo, mmezea mate. Mara aligeuka na kutazama chumba chake, kanzu yake ya waridi yenye maua makubwa na nyengine ya makunguru ikinin`ginia ukutani juu ya misumari...” (uk. 27-28).

Mhusika mwengine aliyetumia mbinu ya uzungumzi nafsi wa ndani ni mhusika Idi. Kama lilivyo jina lake, Idi anaonekana kuzungumza na nafsi yake kuhusu ushindi anaoupata wa kummiliki Bahati. Kwa mfano, mwandishi anaeleza:

“Kwake Idi, jambo hili lilikuwa ushindi. Hii ilikuwa hatua ya mwanzo, ikambashiria sasa njia ilikuwa nyeupe kabisa. Aliyaona maisha yakimchekea akajua kua mipango yake ya kimoyomoyo inakwenda vizuri. Hapo akajipa mkono wa pongezi mwenyewe kwa kuwa bingwa. Aliwaza akaona kuwa madam Bahati alikuwa kichwani mwa mzee, hakuwa na kizuizi chochote asiinuke.” (uk. 37-38).

Jina la Idi lina maana ya furaha, mafanikio na sherehe fulani. Mbinu ya uzungumzi nafsi wa ndani imelandana na jina la mhusika Idi kutokana na jinsi mhusika huyo alivyokuwa katika furaha ya kupata mafanikio yake binafsi, kutokana na kuamini kwamba, atamtia mikononi Bahati. Wazo hilo linakuja kutokana na hali ya uzee alionao Mzee Mwinyi.

Kwa upande wa riwaya ya *Kiu ya Haki*, mtafiti aligundua kuwa, mbinu ya uzungumzi nafsi wa ndani imetumiwa na mwandishi kumuelezea mhusika Mzee Toboa. Tunaelezwa kuwa, mhusika huyu anajiuliza maswali peke yake katika nafsi yake kuhusu matendo mbali mbali yafanywayo na wahusika wengine wanaovunja haki za wengine na pia anaendelea kutafuta mbinu ya kupambana ama kuondoa matatizo hayo, ili haki ipatikane.

Kwa mfano, tunaelezwa:

“Mzee Toboa alikuwa anayahesabu mambo aliyoyajua na kuyapambanua kichwani mwake kuhusu kifo cha Pondamali. Kwanza, aliona gari la marehemu na gari la Sikujua yote yakiwa yamegeshwa pamja kando ya barabara ya Bagamoyo. Pili, alipishana

na gari likiendeshwa kwa kasi sana mita chache kabla ya kuyafikia magari ya Pondamali na Sikujua. Tatu, alisikia kuwa Mke wa Sikujua alikuwa mpenzi wa marehemu na nne, Mzee Fundisha alimwambia kuwa kifo cha marehemu kimesababishwa na fedha na mapenzi. “Hivi kutokana na ujuzi wao wa kupeleleza mambo, Polisi watashindwa kugudua ukweli wa mkasa huu baada ya kuwepa vidokezo hivi” alijiuliza?” (uk:14).

Mfano wa hapo juu, unaonyesha namna mawazo yalivyokuwa yakimshughulisha Mzee Toboa katika kufikiri chanzo cha mauaji ya Pondamali na jinsi ya kupata taarifa za uhakika na baadaye aweze kutoboa siri hiyo ya mauaji katika vyombo vya sheria.

Katika harakati za kutafuta ukweli wa mauaji ya Pondamali, Toboa anamkabiliki Sikujua kumuuliza. Hapa kama tunavyooneshwa ndani ya riwaya hii kuwa, Sikujua alikuwa katika hali mbaya sana wakati wa mahojiano yao. Lakini Toboa hakujali alitaka ukweli udhihirike, kama tunavyoelezwa:

“...Toboa alimuonea imani kijana huyo kwa hali mbaya iliyompata. Lakini alitaka ukweli wa mambo na kutekeleza yale yanayompasa akiwa kama Mzee mzalendo, bwana Toboa Mambo. Dalili za waswasi alizoziona kwa kijana huyu zikampa tamaa ya kutaka kujua zaidi.” Si bure, moyoni mwa huyu bwana mdogo habari nyingi haikosi zimefichana,” aliwaza (uk:18).

Kwa ujumla mhusika Toboa analandana na jina lake kutokana na tabia yake ya kutoboa siri mbalimbali zinazohusu kashfa mbalimbali, rushwa, ulanguzi na magendo pamoja na ile ya mauaji ya Pondamali yaliyofanywa na Sikujua bila kujali lolote litakaloweza kumtokea. Kwa mfano, tunaelezwa:

“Jumatano asubuhi Toboa alipanda basi la UDA kutoka Ilala hadi kitio cha kati cha Polisi. Teksi yake aliiacha nyumbani. Alipofika alienda hadi mapokezi na kuuliza ofisi ya Inspekta Paukwa....Yeye ndiye aliyekuwa akipeleleza kesi ya mauaji ya Pondamali...baada ya kusalimiana, Mzee Toboa hakupenda kupoteza muda....alimtoboa kisa chote cha kifo cha Pondamali kama alivyoielezwa na Sikujua” (uk:39).

Mhusika mwengine anayetumia mbinu hii ni Sikujua. Tunaelezwa kuwa, Sikujua daima amekuwa akijutia tendo alilofanya la kumuua rafiki yake, Pondamali Malipesa kwasababu ya fedha na mapenzi. Mara nyingi amekuwa akiwaza na kujisema ndani ya nafsi yake kwanini kaamua kufanya tendo lile la jinai, zaidi ni pale anapobaini kuwa, siri yake imeshajulikana na watu mbalimbali kama vile; Mzee Toboa, Mzee ambaye anakuwa na tabia ya kutoboa siri mbalimbali za uhalifu kwa vyombo vya sheria kwa nia ya kupatikana kwa haki za wale wanaodhulimiwa na watenda maovu. Kwa mfano:

“Bwana Inspekta sisi siyo wazungu.” Alieleza Sikujua...

“Hapa ni nyumbani kwako,” alimaliza. Alikuwa bado ana wasiwasi mkubwa.” Inakuwaje Inspekta anafika kumtembelea. Makubwa yamenifika, alijisemea moyoni.” Ni hivi majuzi tu nimetoa siri ya



mauaji ya Pondamali kwa Mzee Toboa ndio tuseme kanichongea? au yale majambazi yameshatoa siri yake? Lakini mbona kesi yenyewe haijaanza kusikilizwa?” maswali yote haya yalipita kwenye ubongo wake kwa kasi kubwa” (uk:51).

Licha ya Sikujua kuwa na wasiwasi wa kukamatwa na Polisi kuhusu mauaji aliyoyafanya, ya Pondamali, pia tunaelezwa alijenga chuki kubwa dhidi ya Mzee Toboa hasa pale alipoelezwa na Jaji Pwagu kuwa Mzee Toboa alitoa siri yake kwa Inspekta Paukwa na fedha alizomuhonga, ili amtunzie siri alizipeleka Polisi. Kwa mfano, tunaelezwa:

“Sikujua aliendelea na kazi yake kama kawaida lakini chuki juu ya Mzee Toboa iliujaza moyo wake.” Mzee huyu alikuwa na maana gani kukataa shilingi laki moja ?” alijiuliza Sikujua .” Pesa zote hizo nilizompa, yeye anazipeleka Polisi na kunishtaki mimi baada ya kuzitumia na kujinyamazia!” Sikujua alijiuliza tena na tena juu ya vitimbi vya Mzee Toboa Mambo.. (uk:54).

Kutokana na data, mtafiti aligundua kuwa, mhusika Sikujua analandana na jina lake. Hii inatokana na tabia yake ya kujutia tendo la mauaji alilolifanya baada ya kugunduliwa siri yake hiyo, na kuripotiwa Polisi. Sikujua kama lilivyo jina lake, hakujua kwamba hakuna siri ya watu wawili, pale alipompa siri ya mauaji mke wake ambaye na yeye alimpa shoga yake, Mke wa Fundisha. Mke wa Fundisha akamsimulia mumewe Mzee Fundisha nayeye akampa Mzee Toboa, na hatimaye Mzee Toboa akatoa siri hiyo kwa Polisi. Hali hii inasimuliwa na mwandishi kama ifuatavyo:

“Baada ya ushahidi huo Sikujua aliomba kuingia kizimbani tena, alikuwa anapewa fursa ya kujitetea kwa mara ya mwisho. Sikujua alikuwa katika hali mbaya, woga, wasiwasi, aibu na hasira vilitawala ubongo wake. Hakutegemea kabisa kama kulikuwa na mtu aliyejua siri yake zaidi ya mkewe na Mzee Toboa. Hivyo, hakuandaa mashahidi. Alijuta! (uk:85).

Pia, mtafiti amebaini kuwa, mhusika aliyetumia mbinu hii ya uzungumzi nafsi wa ndani ni Insekta Paukwa kama lilivyo jina lake, tunaelezwa kuwa, yeye alikabidhiwa kusimamia kesi ya mauaji ya Pondamali Malipesa, ili kuipeleleza. Baada ya kupata uthibitisho wa mauaji hayo, yaliyofanywa na Sikujua kutoka kwa Mzee Toboa, anapata safari ya kikazi na anakabidhi kesi hiyo kwa Inspekta Pwagu ili aisimamie.

Paukwa anaonekana kuzungumza na nafsi yake mara baada ya kurudi tena kazini na kusikia maelezo ya Sikujua pale Mahakamani ambayo yaliashiria kuwa Mzee Toboa ndie aliyemuua Pondamali na sio Sikujua. Msanii anaeleza hilo kwa kusema:

“Inspekta Paukwa aliposikia maelezo ya Sikujua aligeuka, kulizuka utatanishi akilini mwake” je! inawezekana kuwa kweli kwamba Mzee Toboa amenihadaa? Na zile fedha alizonikabidhi zilikuwa na maana gani? Huenda kweli hizo fedha zilikuwa ni fedha alizochukua kwa majambazi ....”

Kwa data hizo ni wazi kwamba, Inspekta Paukwa analandana na jina lake, kwani yeye ndiye aliyekabidhiwa kesi ya mauaji ya Pondamali akiwa kama Jaji wa

Mahakama na baadae aliondoka, lakini hatimaye ndiye yeye aliyerudi tena na kusimamia kesi hiyo baada ya Jaji Pwagu na Pwaguzi waliokabidhiwa kesi hiyo kubainika kula rushwa kutoka kwa Sikujua kwa lengo la kumzamisha Mzee Toboa. Hivyo, Inspekta Paukwa anakabidhiwa tena kesi hiyo na kuitolea hukumu akisaidiana na Jaji Mtakunywa.

Kwa mfano, mwandishi anatueleza:

“Mahakama ilikutana tena tarehe 14 Agosti kusikiliza kesi ya mauaji ya Pondamali Malipesa, Jaji Utakunywa ndiye aliechaguliwa kusikiliza kesi hii baada ya Jaji Pwaguzi kwa upande wa mwendesha mashtaka wa pili, Inspekta Paukwa aliwajibika kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Inspekta Pwagu ili asaidiane na Wakili Mtayaona”(uk:83).

Aidha, mtafiti amebaini kuwa, mke wa Sikujua ametumia mbinu ya uzungumzi nafsi wa ndani. Mhusika huyu anaonekana kutumia mbinu hii pale alipogombana na mke wa Mzee Toboa (Mama Asha), kuhusu kuwekwa ndani kwa Mzee Toboa, wakati aliyefanya makosa ni Sikujua. Baada ya Mama Asha kutoa maneno anaogopa na kujisemea ndani ya nafsi yake. Kama tunavyoelezwa:

“...basi subiri ukaseme huko huko Mahakamani,” alijibu mkewe Sikujua kwa jeuri,” kama unajua mumeo hana hatia kitu gani kimekuleta huku kama siyo kutafuta umbeya wa kupeleka Mahakamani?” aliuliza mkewe Sikujua kwa dharau .

“kelele, nakwambia! mimi sikjua kwako. Nimekuja kwa mke Fundisha,” alidakiza Mama Asha kwa hasira.

“Kelele wewe mwenyewe!” alijibu mkewe Sikujua.”

“Basi, jamani, ugomvi wa nini!?” aliwasihi mkewe wa Fundisha. Mke wa Sikujua aliondoka kurejea kwake kwani hasira za Mama Asha zilimtisha. Hakutaka ugomvi uendelee halafu aadhirike hadharani “huenda kweli, anaijua hiyo siri anayoisema,” alijisemea moyoni ”(uk:76-70).

Kutokana na mfano huo hapo juu, Mke wa Sikujua, analandana na jina lake kutokana na tabia yake ya kumuamini sana Mke wa Fundisha, na kuamua kumpa siri yote ya mauaji ya Pondamali. Pia, alimueleza Mke wa Fundisha kuhusu njama walizopanga mume wake na Jaji Pwagu, ili amsaidie katika kesi hiyo, na kumtia hatiani Mzee Toboa bin Mambo baada ya kumpa hongo ya shilingi laki moja. Sikujua hakujua kuwa, hakuna siri ya watu wawili katikaa maisha. Hivyo, anaonekana kujuta kutokana na hali hii ya kutoa siri, lakini maji ndiyo yakisha mwigika hayazoleki. Kwa mfano, katika kazi hiyo msanii anatueleza kwa kusema:

“...basi siku ya pili, tarehe 25 Julai nilipoona mumewe amekwenda kazini, nilimwendea.... Baada ya kusalimiana nikamuona anakwepa kwepa kunieleza nilichoendea....Wenzetu siku hizi mnatembelewa na Ma Inspekta, sijui kuna kheri au shari?” Nilijua hapo nimempata, atanipa tu. Alinipa siri ya mumewe kilioni kuwa ndiye aliyemuuwa Pondamali. Akanipa siri nyengine kuwa mumewe aliibiwa fedha na yale majambazi yaliyomteka nyara yeye na marehemu Pondamali. Atashindwa kunipa siri yao na huyo Inspekta na hali pesa nimemkopesha? Alicheka kidogo, lakini kwa

kujilazimisha. Aliniambia eti Inspekta alikwenda pale kutaka pesa ili yeye na Jaji Pwaguzi wamsaidie mume wake kwenye kesi. Eti Mzee Toboa amewaarifu Polisi, kuwa Sikujua ndiye muuwaji wa Pondamali. Baada ya kutoa taarifa hiyo kwa Inspekta Paukwa, Toboa akaomba asiitwe kwenye ushahidi ili asijulikane kuwa ndiye aliyemsaliti...(uk:71-72).

#### **4.6.2 Mbinu ya Kimaelezi**

Baada ya kuchambua data zilizokusanywa, mtafiti aligundua kuwa, mwandishi wa riwaya ya *Kiu* ametumia mbinu hii ya kimaeelezi katika kuwajenga wahusika wake. Aidha, data hizo zilibainisha kuwa, kuna uhusiano kati ya ujenzi wa wahusika hao na majina waliyopewa na msanii. Hivyo, katika riwaya hii mtafiti aliweza kubaini hilo kama ifuatavyo:

Kwanza, mhusika Mzee Mwinyi amesawiriwa kwa njia ya kimaeelezi. Mhusika huyo ameelezewa wasifu wake. Ambapo anaelezwa namna ya mavazi na maisha yake kwa jumla yalivyokuwa. Kwa mfano msanii anaeleza:

“Mwinyi alikuwa amevaa shuka nyeupe ya thamani na fulana nyeusi yenye mikono, iliyomtoa tumbo. Upara juu ya kichwa chake ulikuwa unaongezeka na sasa alibakiwa na nywele mbuye mbuye za kahawia juu ya masikio na kichogoni. Ule upara ulifanya uzidi kufupika, na pua yake tapaya izidi kutapanyika. Rangi yake ilikuwa nyeusi titi, na wala hakuwa na umbo la afya. Maungo yake hakuchukuwana, maana alikuwa mfupi wa kimo, kaviringa kati, kachongeka juu na

chini.....Mwinyi na Idi waliketi uso kwa uso na kwenye makochi. “Umekwenda?” Mwinyi aliuliza kwa hamu.” (uk. 13-14).

Maelezo hayo, yanatudhihirishia namna mhusika Mwinyi anavyolandana na mbinu hii ya kimaenzi. Hii ni kwa sababu, tunaelezwa sura, umbile na tabia pamoja na matendo aliyokuwanayo. Inaelezwa kwamba, Mzee Mwinyi alikuwa anafanyiwa kila kitu na Idi. Hiyo ni tabia ya Mamwinyi wengi ulimwenguni.

Kwa upande wa riwaya ya *Kiu ya Haki* ya Zainab M. Mwangi, mtafiti alibaini kwamba, msanii ametumia mbinu hii ya kimaenzi katika kuwajenga wahusika wake. Aidha, data hizo zilibainisha kwamba, kuna uhusiano kati ya ujenzi wa wahusika hao na majina waliyopewa na msanii. Hivyo, katika riwaya hii mtafiti alichambua data kama ifuatavyo:

Kwanza, mtafiti amebaini kwamba, mhusika Toboa ni miongoni mwa wahusika waliojengwa kwa kutumia mbinu hii ya kimaenzi. Msanii anatuchorea sifa na matendo ya mhusika huyu kwa kutuelezea matendo yanayotendwa na Mzee Toboa. Yanapotolewa maelezo hayo, yanatuchorea picha ya tabia alizonazo Mzee Toboa. Aidha, maelezo hayo yanatupa picha ya mhusika huyu na jina lake kwa namna anavyotoboa siri za wahalifu. Kwa mfano tunaelezwa:

“Mzee Toboa ni dereva wa teksi kwa miaka mingi jijini Dar es salaam. Kutokana na uzoefu wa kazi yake, uaminifu, uzungumzaji na ucheshi kwa wateja wake, aliweza kujipatia chumo nono kila siku....alikuwa na umri wa miaka arobaini au hamsini hivi, mwenye umbo la wastani si mnene wala si si mfupi. kichwa chake hakikuwa

kikubwa lakini kilijaa busara, hulka njema na hekima yake kubwa vilimfanya aheshimiwe na watu.

“Japokuwa hakusoma sana, Mzee Toboa alijaaliwa kujua siasa ya nchi yake barabara, alikuwa na tabia ya kuongea na kila mtu, watoto, vijana, wazee, viongozi, matajiri na makabwela. Kwa maneno mengine, Mzee Toboa alikuwa mtu mcheshi na mwema. Kwa tabia yake hiyo aliweza kujua matukio mbalimbali mitaani kwa urahisi kabisa, yeye hakupenda uovu wala dhuluma (uk:2).

Hivyo, Mzee Toboa analandana na jina lake kutokana na tabia yake ya kuchukia maovu na dhuluma zinazofanywa na watu waovu, jambo linalomsukuma kutoa siri za waovu hao katika vyombo vya sheria, ili mwenye haki aipate. Msanii anaendelea kutueleza kama ifuatavyo:

“Kila alipofanikiwa kumjua mwovu ama chanzo cha maovu, hakusita kwenda kutoa taarifa kwa wanausalama kuhusu mtu au kikundi cha watu waliohusika na maovu hayo.(uk:2).

Mhusika mwengine aliyesawiriwa kwa kutumia mbinu ya kimalezi ni Inspekta Paukwa. Mwandishi ametueleza kuwa:

“Inspekta Paukwa alikuwa ofisa wa Polisi mwenye cheo cha mrakibu mwandamizi, alikuwa na shahada ya sheria na alikuwa amelitumikia jeshi la Polisi kwa miaka kumi na moja sasa. Alikuwa hodari sana katika kazi yake, aliona raha kufanya kazi yake, si hivyo tu, alijivunia pia.

Yeye, ndie alikuwa akipeleleza kesi ya mauaji ya Pondamali, ni yeye vilevile, kwa sababu ya upungufu wa mawakili wa serikali, alipewa kibali maalumu na mwendesha mashtaka, D.P.P, asaidiane na Wakili Mtayaona kuendesha kesi hiyo ya mauaji ya Pondamali Mahakama Kuu” (uk:39).

Kama mfano unavyoonesha hapo juu, Inspekta Paukwa analandana na jina lake kutokana na kitendo chake cha kufanya kazi ya jeshi la Polisi kama Wakili wa Mahakama Kuu kuendesha kesi ya mauaji ya Pondamali. Pia, alipata nafasi ya kuondoka kikazi na baadae akarejea tena, na kupata nafasi tena ya kuendesha kesi hiyo hiyo baada ya Jaji Pwagu na Pwaguzi kushindwa kutimiza maadili ya kazi yao. Msanii anatueleza hilo kwa kusema:

“...wakati upelelezi wa kesi hii unaendelea Inspekta Paukwa alipata safari ya ghafla, alimkabidhi Inspekta Pwagu jalada la kesi  
 ...(uk:44).

#### **4.6.3 Mbinu ya Ulinganuzi na Usambamba**

Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha kwamba, mwandishi wa riwaya ya *Kiu* alitumia mbinu hii ya ulinganizi na usambamba katika kuwalinganisha mhusika Tatu na Kidawa huku akionyesha tafauti zao. Imeoneshwa kwamba, mhusika Kidawa walitofautiana na Tatu kwasababu, Kidawa aliolewa na muume mwenye wivu, bughdha, domo na mvivu kiasi ambacho maisha yake hayana furaha. Lakini mhusika Tatu amepata bahati ya kuolewa na mume tajiri na msomi huku akiishi katika nyumba ya kifahari. Hata hivyo wote katika ndoa zao wanaelezwa kuwa wana matatizo. Kwa mfano, msanii anatueleza:



“Tatu hakuwa kama Kidawa maana alikuwa na bahati kuolewa na mume mwenye kuzaliwa na wazee wenye chao. Yeye alikuwa mtu aliyesoma na kuelimika. Tatu na mumewe walikuwa wakiishi mtaa wa Piku piku katika nyumba nzuri ya kisasa.”

Mbinu hii ya ulinganuzi na usambamba imelandana na majina ya wahusika Kidawa na Tatu. Kwa mujibu kamusi ya BAKIZA (2010), wanaeleza kuwa, neno kidawa lina maana ya samaki mdogo mpana mwenye rangi ya huzurungi anayeelea juu ya maji kama jani. Pia, wanaeleza kuwa, neno “tatu” ni idadi kamili kati ya mbili na nne. Hivyo, majina ya wahusika hawa yamelandana na mbinu hii kutokana na kulinganishwa maisha ya Kidawa yakiwa yanaelea kutokana na kukumbwa na matatizo, wakati maisha ya Tatu yamekamilia. Tatu anakumbwa na matatizo ya ndoa lakini bado ametulia.

Kwa upande mwingine, mwandishi wa riwaya ya *Kiu ya Haki* iliyoandikwa na Zainab M. Mwanga, imetumia mbinu hii ya ulinganuzi na usambamba kwa wahusika Inspekta Paukwa na Inspekta Pwagu. Inspekta Paukwa sifa yake kubwa ni kuwa, anafanya kazi yake kwa misingi ya uadilifu, ili haki ipatikane. Pia, alikuwa na lengo la kuendesha kesi ya mauaji ya Pondamali bila kumshirikisha Mzee Toboa kama shahidi.

Inaelezwa kuwa, baada ya kupata safari, Paukwa anamkabidhi kesi Inspekta Pwagu akishirikiana na Jaji Utakunywa. Kwa mfano, msanii anasema:

“...wakati wa upelelezi wa kesi hii unaendelea. Inspekta Paukwa alipata safari ya ghafla. Alimkabidhi Inspekta Pwagu jalada la kesi. Inspekta Pwagu alikuwa ofisa wa Polisi kama Inspekta Paukwa,

Inspekta Pwagu naye alikuwa na shahada ya Chuo Kikuu. Naye alikuwa na kibali maalum cha Mwendesha Mashtaka D.P.P. kushughulikia kesi hii Mahakama Kuu (uk:44)”.

Kwa upande wa Inspekta Pwagu, yeye alikuwa anafanya kazi yake kwa misingi ya rushwa na hongo. Hata baada ya kukabidhiwa kesi hii, tamaa ya kuchuma pesa kupitia kesi hii ilimtawala. Shauku yake ilionekana kufifisha haki na kushamiri kwa uovu na dhulma katika moyo wake. Msanii anatueleza:

“Katika kusoma, jalada lile, hasa aliposoma taarifa ya Mzee Toboa, Inspekta Pwagu alipata wazo la kutumia kesi hiyo kuchuma fedha, miiko na desturi za kazi yake zinakataa uchumaji mali kwa njia hiyo aliyokuwa anafikiria..”(uk. 44).

Inspekta Paukwa analandana na jina lake, kwani alikabidhiwa kesi na baadae akaondoka na kumkabidhi Inspekta Pwagu, na mwishoni anarejea na kuendelea na kushughulikia kesi ile ile baada ya Jaji Pwagu kuchukua hongo kutoka kwa Sikujua.

Ama, Inspekta Pwagu kulandana kwake ni kule kutokana na tabia yake ya kutoa kauli ambayo ni kinyume na matendo yake. Anamuahidi Inspekta Paukwa kutenda haki lakini baadaye anakwenda kinyume.

#### **4.6.4 Mbinu ya Majazi au Matumizi ya Majina**

Mtafiti baada ya kukusanya data na kuzichambua, aligundua kwamba, katika riwaya ya *Kiu*, wapo wahusika waliosawiriwa majina yao kwa kutumia mbinu ya majazi. Wahusika hao walifanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

#### 4.6.4.1 Bahati

Kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010), wanaeleza neno “bahati” lina maana ya jambo zuri linalotokea bila ya mtu kutarajia au kukusudia. Pia, wanahitimisha kwamba, neno hilo huweza kuwa jambo baya. Aidha, Mshindo na Snoxall, (2002), wanatoa ufafanuzi wa neno “bahati” kuwa kuna bahati nzuri na bahati mbaya. Mhusika Bahati alizaliwa akiwa na sura nzuri. Kutokana na uzuri wake unawafanya watu wengi wanaokutana na Bahati kumpenda licha ya kuwa ametokea katika familia masikini. Hivyo, Bahati anajikuta akiangukia katika mapenzi ya Idi na Mwinyi yanayomfanya aishi maisha ya kifahari. Mwisho, mhusika huyo, anapata bahati mbaya ya kusalitiwa na Idi katika ndoa yake. Tunaona anavyokosa raha na hatimae anarejea tena nyumbani kwao, kuishi maisha ya ujane. Mwandishi anatueleza:

“...Idi alimshika kwa mikono yake miwili huku akimwambia,  
“Nitakuoa, mpenzi, tuwe pamoja milele!”

Kwa dakika chache hivi walikumbatiana, kila mmoja akiwa na hamu  
na mwenzake, roho moja, ya mapenzi, katika raha na adhabu ya  
kutakana.” (uk. 54)

Mtafiti amegundua kuwa, mhusika Bahati analandana na jina lake kwasababu, baada ya kuzaliwa akiwa na uzuri unaowavutia wengi, kuishi maisha mazuri, kusalitiwa katika ndoa yake na pia kuzaliwa katika familia masikini na kulelewa na mama aliyetelekezwa na mume wake. Hivyo, kwa upande mmoja, Bahati ni mwenye bahati nzuri na kwa upande mwengine ni mhusika mwenye bahati mbaya.

#### 4.6.4.2 Idi

Kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010), neno “idi” ni miongoni mwa sikukuu za Kiislamu, ambapo watu siku hizo hula vizuri, huvaa vizuri na kunywa vizuri pamoja na hata wengine kutenda matendo ya kiuhalifu. Siku ya Idi, watu wengi huishi maisha ya anasa ingawa hawana uwezo huo. Msanii anamtumia mhusika Idi, akiwa na tabia za kupenda ufahari na kupenda maisha ya anasa na ulevi. Msanii anatueleza kwa kusema:

“Mwajuma akaendelea,” wiki mbili hizi nilizokaa hapa, bibi niliyoyaona ukitendewa mimi yamenitia huzuni, je wewe unayetendewa?....

...ulipokuwa spitali nilimuona mumeo akija na mwanamke siku zote, akilala naye juu ya kitanda kilekile ambacho ni haki yako wewe tu, bibi...” (uk.110-111)

Kutokana na maelezo hayo, mtafiti amegundua kuwa, mhusika Idi amelandana na jina lake kutokana na tangu kuzaliwa kwake, maisha yake na matendo yake yote kupenda starehe tu, anasa pamoja na ulevi wa kupindukia.

#### 4.6.4.3 Bi Mvita

Neno Mvita, linatokana na neno “vita”, katika lugha ya Kiswahili lenye maana ya mapigano. Katika kazi hiyo, Bi Mvita ni mhusika anayesimamia na kuendeleza mila na tamaduni za Kiafrika. Kwa mujibu wa Manzi (2007), utamaduni ni pamoja na mila, desturi, itikadi za jamii fulani ambazo huzifuata katika maisha yao ya kila siku. Msanii ameonesha kuwa, kabla ya kufanyika kwa arusi, wanawake hupewa mafunzo ya unyago wanapopata ukubwa (kuvunja ungo), ili kuwaandaa kuweza

kumudu nyumba zao. Hivi ndivyo alivyokuwa Bahati binti Jaku, ambaye tunaelezwa kuwa, Bi Mvita alimpa mafunzo ya unyumba wakati alipovunja ungo.

Kwa mfano msanii anasema:

“Mwanangu unasema wiki ijayo?” Cheusi alimuuliza,” husemi mwezi ujao? Kuna somo yake Bi Mvita, ndugu zangu, wahisani wangu, hao wote lazima niwapate tushirikiane. Hasa Bi Mvita lazima awepe, alimtambikia sana huyu mtoto alipovunja ungo, anampenda kama kwamba kamzaa mwenyewe.”(uk:63).

Data zinaonesha kwamba, Bi Mvita analandana na mbinu hii ya majazi kutokana na kupiga vita tamaduni za kigeni na kuendeleza utamaduni wa Kiafrika. Wazo hilo linathibitishwa kutokana na tabia yake ya kumpa Bahati mafunzo wakati anapopata ukubwa.

#### **4.6.4.4 Sheikh Baraka**

Kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010), neno “baraka” lina maana ya heri au wema. Kimsingi neno “Baraka” lina maana ya kinyume cha “shida”. Mhusika Baraka katika riwaya ya *Kiu* anatumiwa na mwandishi kama shekhe anayefungisha ndoa ya Bahati na Idi na ni yeye anayehusika na kuivunja ndoa hio. Mwandishi ametumia mbinu ya majazi kumsawiri mhusika huyu, kutokana na kazi yake ya kufungisha na kuandika talaka katika ndoa ya Idi na Bahati ni cha wema. . Kwa mfano, mwandishi anaelezea suala hili kwa kusema:

Punde aliwasili Shehe Baraka, mwozaji mashuhuri, mwenye kufuata barabara taratibu za kidini....kijana mmoja akaleta sinia la marashi, chetezo cha mkaa ya moto, na kisahani chenye udi na ubani,

akaviweka mbele ya shehe.....na pale katika moshi wa udi na ubani, mbele ya shekhe na waliohudhuuria, Idi alikula kiapo cha ndoa. Papo hapo, Idi na Bahati wakawa mume na mke ( uk. 71).

Hivyo, kutokana na mfano huo hapo juu, mtafiti amegundua kwamba, mhusika Baraka analandana na jina lake, kwa kubarikiwa kupata riziki zake za maisha kupitia kufungisha ndoa. Aidha, ni mhusika ambaye analeta utulivu miongoni mwa wanandoa. Kwa mantiki hiyo, anabebeshwa dhana ya heri miongoni mwa wanajamii.

#### **4.6.4.5 Cheusi**

Mtafiti amegundua kuwa, msanii amesanii jina hilo kiishara. Dhana hii inaweza kutupatia taswira ya kiza, usiku ama matatizo. Aidha katika utamaduni wa Mwafrika neno “cheusi”, linaashiria matatizo na hali ngumu ya maisha ukiwamo umaskini.

Tunaelezwa kuwa, Cheusi alikuwa akiishi katika nyumba ndogo, kongwe na chakavu. Aidha, mhusika huyo, alikimbiwa na mume wake, Jaku na kumuachia ulezi wa mtoto wao; Bahati huku akiwa na majonzi, simanzi na mfazaiko mkubwa.

Kwa mfano, msanii anatueleza:

“Mwisho wa ukumbi, kando ya mlango wa kutokea uani, palikuwa na mtungi wa maji ya kunywa uliosimama juu ya chanja ya miguu mitatu. Kata yake ya kifuu cha nazi ikining’inia penye msumari ukutani... ua wenyewe haukuwa mkubwa, kuta mbili za kimo cha mtu mrefu ziliunga nyumba na banda. Hilo banda ndilo lililokuwa na jiko

na choo, nafasi ile ya ua ilisaidia kuweka vitu ambavyo havikufaa kukaa bandani wala nyumbani...(uk:23-24).

Pia, tunaelezwa kwamba, ilikuwa vigumu kwa Cheusi kupata hata kile cha kutia mdomoni kutokana na hali ya umasikini iliyomkumba. Kwa mfano tunaelezwa:

“Bahati na mama yake walikuwa wamekwisha lemaa katika umaskini, hasa tangu kuondoka kwa mwenzao Jaku, baba yake Bahati, maisha yalikuwa ya tabu na dhiki. Ingawa Jaku mwenyewe hakuwa mchumi kitu, lakini walisaidiana kupangusana machozi, na maisha yalikuwa afadhali kidogo (uk. 28).

Mtafiti alibaini kwamba, jina la mhusika Cheusi linalandana na mbinu ya majazi kutokana na matatizo ya umasikini na hali ya maisha magumu aliyonayo mhusika huyo. Kwa jumla, maisha ya mhusika huyu, yamekumbwa ni kila aina ya misuko suko, tabu na dhiki.

Kwa upande mwengine, mtafiti alifanya uchambuzi wa data alizozikusanya katika riwaya ya *Kiu ya Haki*, na kubaini kwamba, pia mbinu ya majazi imetumika katika kuwasawiri wahusika katika riwaya hiyo. Uchambuzi huo unajidhihirisha kama ifuatavyo:

#### **4.6.4.6 Mzee Toboa**

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010), neno “toboa” lina maana ya kitendo cha kutia tundu kitu kwa kutuma kitu chenye ncha au makali (tomoa). Tunaelezwa kwamba, Mzee Toboa alikuwa muaminifu, mkweli na mpenda haki. Hata hivyo,

kwa upande mwingine aliwafichua wahalifu na wahujumu uchumi wa Taifa.

Kutokana na tabia hiyo, analinganishwa na kuwatoboa wahalifu. Kwa mfano:

...wakati Mzee Toboa na mkewe wanaondoka kuelekea nyumbani  
baada ya kustarehe, kijana huyo aliwafuata, na Mzee Toboa Mambo  
alimwona... Siku iliyofuata Mzee Toboa alikwenda kutoa tarifa  
Polisi kuhusu msukosuko huo, na mtu aliyemshuku...(uk:36).

Mhusika Toboa, analandana na jina lake kwa kutoboa siri zilizofichika na za maovu ili haki ipatikane.

#### **4.6.4.7 Sikujua**

Kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010), neno “sikujua” linatokana na kitenzi chenye maana ya “kutoelewa jambo au matukio ya jambo fulani unalolitenda”. Tunaeleza kwamba, Sikujua alifanya mapenzi na mke wa Pondamali na alimpiga mke wake kwa hasira, huku akimtolea siri ya mauaji ya Pondamali. Matendo yote hayo aliyatenda bila kutambua kitakachotokea baadae. Kwa mfano msanii anaeleza:

“ Nilifadhaika sana kuona kuwa nimeuwa bila kutegemea, Mzee Toboa. Mwili wa Pondamali uliishiwa na uhai wake. Nilisikitika lakini sikujuta. Alistahili kufa! Hadi wakati huo yaani baada ya kuua, mwili wangu ulikuwa na nguvu za ajabu kutokana na hasira eti mke wangu kamfilisi! Kwani nilimtuma? Ingawa kwa sasa nasikitika na najuta kufanya kitendo hicho....”(uk:28-29).



Mhusika Sikujua analandana na jina lake kutokana na kitendo cha kumuua Pondamali kwa sababu ya fedha na mapenzi. Sikujua anajuta baada ya kuuwa na hatimaye anaishia gerezani.

#### **4.6.4.8 Pondamali**

Jina hili limepatikana kwa kuunganishwa kitenzi “ponda” chenye maana ya kitendo cha kuvuruga kitu ili kiwe laini, na nomino “mali” yenye maana ya kitu cha thamani kama vile gari, nyumba, fedha nakadhalika (BAKIZA, 2010). Waswahili husema kuwa, “ponda mali kufa kwaja”. Wakimaanisha mtu atumie alichonacho kwa hali yoyote ili kimfaidishe yeye binafsi, bila kujali matumizi hayo yanafaa au hayafai.

Mhusika Pondamali analandana na jina lake kutokana na tabia yake aliyokuwa nayo ya uzinzi. Tunaelezwa kuwa Pondamali alitembea na Mke wa Sikujua na alishindwa kuweka akiba benki na hata kuo na badala yake fedha zake zote alizitumia kwa kustarehe na Mke wa Sikujua. Hali hii inaendana na msembo wa Waswahili ulionukuliwa unaosema ‘Ponda mali kufa kwaja’, kama alivyokuwa mhusika huyo.

#### **4.6.4.9 Mke wa Sikujua**

Kimsingi mtafiti amgundua kwamba, mhusika huyu hakupewa jina jengine ispokuwa kuegemezwa na mume wake. Mhusika huyu, amekuwa akifanya mapenzi ya siri na Pondamali. Pia, anatoa siri ya mauaji ya Pondamali kwa shoga yake, Mama Fundisha. Hakujua kuwa hakuna siri ya watu wawili. Kwa mfano:

“...vilevile alipata fununu kuwa Mke wa Sikujua anafanya mapenzi ya siri na marehemu...”(uk:4),

Mke wa Sikujua analandana na jina lake, kutokana na tabia zake hizo. Yeye alikuwa hajui masaiibu yatakayompata kutokana na tabia yake ya kufanya mapenzi nje ya ndoa.

#### **4.6.4.10 Mama Asha**

Ni mazoea kwa familia nyingi za Kiafrika wanapopota mtoto wa kwanza, mama au baba hunasibishwa jina lake na mtoto wao. Hivyo jina la Mama Asha limetokana na kuwa na mtoto mwenye jina la Asha. Kwa mfano:

“Mkosi gani huu Yarabbi? Nilihisi mimi. Haya basi, yametokea” aliropoka. “Najua ni hizi habari za Sikujua tu, ndiyo zimemfanya akamatwe. Mwanangu futari ipo jikoni.”Nipeleke nikamwone. Baba, aah, baba...sina mtu mwengine... maskini ...Asha hayuko, na mimi sijui kuendesha gari ,” alisema huku anatemeka kwa wasiwasi na hasira.(uk. 73-74).

Hivyo, Mama Asha amelandana na jina lake kutokana na kuwa na mtoto anayeitwa Asha.

#### **4.6.4.11 Mzee Fundisha**

Baada ya kuchambua data, mtafiti amebaini kwamba, jina hili limetokana na kitenzi “fundisha” chenye maana ya kutoa mafunzo au kusomesha. Mhusika Fundisha wa *Kiu ya Haki*, analandana na jina lake kutokana na Mahakama ilipompiga faini ya shilingi 300/=, baada ya kuficha ushahidi alioupata kutoka kwa Mke wa Sikujua ambaye mume wake alimuua Pondamali. Kitendo cha

kupigwa faini ilikuwa ni somo kwa wengine wenye tabia ya kuficha ukweli kama Fundisha. Kwa mfano tunaeleza:

“Mashahidi wawili wa Mzee Toboa wameonekana na kosa la kutotoa taarifa Polisi mara walipomjuwa muuaji. Aliendelea Jaji Utakunywa....Mzee Fundisha na mkewe wanatozwa faini ya shilingi 300/= kila mmoja kwa kosa la kumficha muuaji....(uk:89-90).

Kwa maelezo hayo, ni wazi kwamba jina la mhusika huyu limetumia mbinu ya majazi, na hivyo limelandana na mhusika huyo, mahakama kumtumia yeye kuifundisha jamii kuepuka rushwa na hongo kama ilivyotokea kwa Jaji Pwagu na Inspekta Pwaguzi.

#### **4.6.4.12 Mama Fundisha**

Jina hili limetokana na muunganiko wa nomino ‘mama’ yenye maana ya mke, mlezi, ama mzazi, na kitenzi ‘fundisha’, kitendo cha kutoa mafunzo kwa wengine. Mama Fundisha analandana na jina lake kutokana na kuwa yeye ni mke wa Mzee Fundisha, lakini pia kama alivyokuwa mume wake walishindwa kutoa taarifa Polisi mara baada ya kumjua muuaji, Mahakama ikaamua kuawadhibu kwa kuwatoza faini ya shilingi 300/= kila mmoja. Pia, anashirikiana na mume wake kuipa funzo jamii juu ya umuhimu wa kuwafichua wahalifu katika jamii ili haki itendeke.

Kwa hivyo, mtafiti amebaini kwamba, kutokana na adhabu inayotolewa kwa mhusika huyo, amelandana na jina lake.

#### 4.6.4.13 Swalehe

Kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010), neno “swaleh” limetokana na lugha ya Kiarabu lenye maana ya mtu mwema. Tunaelezwa kwamba, Swaleh alishirikiana na baba yake katika harakati za biashara. Hivyo, mhusika huyu anachorwa akiwa ni muaminifu na mtoto mwema kwa wazazi wake. Kutokana na tabia yake hiyo, alipendwa na Mzee Fundisha. Kwa mfano, msanii anasema:-

“Fundisha hakujibu kitu. Badala yake alimwita kijana wake mmoja akamkabidhi kazi ya kupokea pesa na kumwashiria Mzee Toboa amfuate sebuleni wapate faragha ya kuongea (uk:5-6).

Mhusika Swalehe analandana na jina lake kutokana na tabia yake ya uaminifu, anamsaidia baba yake kupokea fedha.

#### 4.6.4.14 Inspekta Paukwa

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010), neno “Paukwa” ni tamko linalotumika mwanzo wa kutamba hadithi. Inaelezwa kwamba, alikuwa ndie jaji wa mwanzo wa kesi ya Ponda Mali. Jaji huyo alipata safari na kumuachia kesi hiyo, Jaji Pwagu. Hata hivyo, kama waswahili wasemavyo; “Paukwa Pakawa”. Baada ya kuondoka alikalia kiti cha ujaji, Jaji Pwagu, ambaye hakuwa muaminifu. Kwa mfano tunaelezwa:

“Wakati wa upelelzi wa kesi hii unaendelea, Inspekta Paukwa alipata safari ya ghafla. Alimkabidhi Inspekta Pwagu jalada la kesi .....kabila ya kusafiri, Inspekta Paukwa aliongea na Wakili wa serikali, Bwana Mtayaona, kuhusu habari zote za kesi na taarifa ya Mzee Toboa na nia yake yeye Paukwa, kumlinda Mzee huyo...”(uk:44).

Mtafiti amebaini kwamba, mhusika huyo amelandana na jina lake, kutokana na kitendo chake cha kuondoka baada ya kukabidhiwa kesi ya Pondamali. Hivyo, jalada alilolitayarisha ndilo lililotumika kuwa ni marejeleo kwa jaji wengine. Aidha, neno pawkuwa lina maana chanya miongoni mwa jamii ya Waswahili, hivyo, mhusika huyo alikuwa anakubalika kutokana na kufuata misingi ya sheria.

#### **4.6.4.15 Jaji Pwagu**

Kwa mujibu wa kamusi la BAKIZA (2010), neno “pwagu” ni sawa na “pwaguzi”, likiwa na maana ya mtu amabaye kauli zake si za kutegemewa kutokana na tabia yake ya kutokuwa na busara na mazingatio. Kwa mfano tunaeleza:

“Unazo shilingi laki moja? Kesi hii si ndogo. Tena kumbuka tuko wawili” alisema Inspekta Pwagu na uso mkavu bila aibu...baada ya kukabidhiwa hizo fedha Inspekta Pwagu aliaga na kumwambia Sikujua kwamba atapanga siku inayofaa kukutana ili wamfundishe namna ya kujitetea Mahakamani siku atakapoitwa” (uk:54).

Kutokana na maelezo hayo, mtafiti amebaini kwamba, mhusika Pwagu analandana na jina lake, kwani yeye anadiriki kuchukuwa hongo kutoka kwa Sikujua kwa lengo la kumkandamiza Mzee Toboa. Anafanya kazi yake kinyume na maadili ya kazi hiyo kama lilivyo jina lake. Hivyo, anaonekana hana msimamo wa kutegemewa.

#### **4.6.4.16 Inspekta Pwaguzi**

Kama ilivyokwisha fafanuliwa maana ya jina Pwaguzi hapo juu, mhusika Pwaguzi anaashirikiana na Jaji Pwagu kula hongo kutoka kwa Sikujua ili wamsaidie katika

kesi yake ya mauaji ya Pondamali. Hivyo, ni dhahiri kuwa, analandana vyema na jina lake.

#### **4.6.4.17 Wakili Mtayaona**

Kwa mujibu wa kamusi la BAKIZA (2010), neno “mtayaona” limetokana na kitenzi “ona”, chenye maana ya kitendo cha kupata hisia ya jambo fulani. Kitendo hicho kimeambishiwa na kupata neno “Mtayaona”. Likiwa na maana ya kuwaeleza watu kuwa watapata hisia kwa njia ya kuona litakalotokea. Kama Waswahili wasemavyo; “utaona cha mtemakuni”, wakimaanisha “kupata adhabu, kipigo, mateso au maudhi kutokana na kile mtu alichokitenda”. Msanii anatuelezea mhusika huyu kwa kusema:

“Sikujua amepatikana na hatia ya kuuwa kwa makusudi. Mahakama hii haina adhabu nyengine ya kumpa bali, adhabu ya kunyongwa hadi afe!” (uk. 90).

Mhusika Mtayaona analandana na jina lake kutokana na tabia yake ya kufanya kazi kwa misingi ya haki, ambapo aliendesha kesi ya mauaji ya Pondamali akiwa kama Wakili wa serikali katika Mahakama Kuu na haki ikapatikana. Mwisho, watu wanamshuhudia Sikujua akiona aibu kutokana na kitendo cha mauaji alichokifanya. Pia, watu wote waliohudhuria Mahakamani waliona kwa macho yao baada ya ukweli kudhihiri.

#### **4.6.4.18 Jaji Utakunywa**

Jina la Utakunywa limetokana na kitenzi “kunywa” ambacho kimenominishwa na kuwa Utakunywa ikiwa na maana ya mtu anayekunywa kinywaji fulani (BAKIZA, 2010).

Mhusika Utakunywa ana sifa ya kutoa hukumu kulingana na kosa lilivyo, ni mwadilifu na mwenye uchu wa kukomesha uovu. Msanii anaeleza:

“Baada ya kuchambua maelezo kutoka kwa washtakiwa wote na ushahidi ulioteuliwa, sasa natoa adhabu kwa wenye hatia” aliendelea Jaji Utakunywa. “Somba, Kila na Kazamoyo, wanahukumiwa kifungo cha miaka mitano na kazi ngumu kila mmoja kwa kosa la ujambazi.....Sikujua amepatikana na hatia ya kuuu kwa makusudi, Mahakama haina adhabu nyengine ya kumpa bwana Sikujua bali, adhabu ya kunyongwa hadi afe.” (uk.89-90).

Mtafiti amegundua kuwa, mhusika Utakunywa, analandana na jina lake hasa baada ya kutoa hukumu kwa majambazi, Sikujua na Fundisha na mke wake bila kujali lolote. Wote, walikunywa adhabu kulingana na ukubwa wa makosa yao.

#### **4.5.4.19 Somba**

Kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010), neno “somba” ni kitendo cha kuzoa kwa pamoja vitu bila ya kutumia taratibu. Tunaelezwa kwamba, mhusika Somba aliwateka nyara Pondamali na Sikujua, na kuwanyang’anya vitu ikiwemo saa ya mkononi na pesa taslimu kwa njia ya nguvu. Kwa mfano, msanii anasema:

“Mzee Toboa alipofika nyumbani kwake, mkewe alimpa habari za kusikitisha kuhusu Sikujua. Alimwambia kuwa Sikujua aliingiliwa na majambazi usiku wa Jumanne....aliibiwa pesa zote na vitu vyengine”(uk:40).

Hivyo, mtafiti amegundua kwamba, mhusika Somba analandana na jina lake, kutokana na tabia yake ya ujamabazi. Ambapo, anashirikiana na Killa na Kazamoyo kuwateka nyara Pondamali na Sikujua na kuwanyanganya fedha zao. Yote hayo ni matendo yasiyofuata taratibu zinazokubalika na jamii.

#### **4.6.4.20 Killa**

Kwa mujibu OUP (2009), neno “Killa” (killer), linatokana na neno “kill” lenye maana ya mtu au mnyama anayeua. Msanii alitumia neno hilo, kama ilivyo tabia ya vijana wengi ambao hujipatia au kupatiwa majina kutokana na tabia zao au sifa zao. Mhusika Killa, amepatiwa jina hilo kutokana na tabia yake ya mauaji. Kwa mfano, tunaelezwa:

“Yule abiria aliyenilenga bastola aliniongoza hadi kichakani, ambako alinipekuwa mifukoni.....” (uk.20).

Mhusika Killa analandana na jina lake. Mhusika huyu ni jambazi anayemteka nyara Sikujua na Pondamali huku akiwa na silaha za moto (bastola).

#### **4.6.4.21 Kazamoyo**

Kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010), neno “kaza” limetokana na muunganiko wa kitenzi “kaza” kikiwa na maana ya kitendo cha kufunga kitu kwa nguvu na nomino moyo lenye maana ya ujasiri wa kufanya jambo gumu au zito.



Mhusika Kazamoyo, anaelezwa kuwa amejitolea katika kufanya matendo ya kijambazi bila kujali linaloweza kumfika. Mhusika huyu haogopi hata mkono wa sheria. Kama tunavyoelezwa:

“Inspekta Pwagu: Bwana Kazamoyo sasa unakubaliana na usemi wa Wakili Mtayaona kuwa Killa aliumia katika harakati za ujambazi, na sio kwa kujikwaa kwenye matofali?”

Kazamoyo: Ni kweli mheshimiwa Jaji, Killa alipigwa jiwe mguuni na mmoja wa madereva wa tekisi tuliowateka” (uk.63).

Mhusika Kazamoyo analandana na jina lake. Mhusika huyu anaukaza moyo wake kufanya matendo mazito ya ujambazi na kumpora fedha na saa ya mkononi Sikujua bila ya kujali kinachoweza kumtokea. Pia, Kazamoyo anaukaza moyo wake na kuzungumza ukweli Mahakamani baada ya kuhojiwa. Hivyo, kwa upande mwengine, mhusika huyo ni jasiri kutokana matendo hayo.

#### **4.6.5 Mbinu ya Kuwatumia Wahusika Wengine.**

Wamitila (2002:26), badala ya kuyatumia majina ya wahusika au maelezo, mwandishi anaweza kumsawiri mhusika kupitia kwa mhusika mwengine. Wahusika wanaweza kuelezwa na wahusika wengine, yaani tunawajua kutokana na maneno ya wahusika wenzao.

Mtafiti amebaini kwamba, katika riwaya ya *Kiu ya Haki*, mbinu hii ya kuwatumia wahusika wengine imetumiwa na mhusika Sikujua kumsawiri Mzee Toboa Mambo. Kupitia mhusika Sikujua, tumeweza kumtambua Mzee Toboa kuwa ni mtu asiyependa uhalifu na dhuluma. Kwa mfano, tunavyoelezwa:

“...vilevile, nakuomba sana, na nakutafadhalisha sana Mzee wangu uitunze siri nitakayokupa. Uwe mtu wa msaada mkubwa kwangu kama unavyoniahidi. Niko tayari kukupa chochote utakachonitajia ili mradi uitunze siri hii. Najua wewe na mambo ya uhalifu ni maji na moto, na ndio maana nimeamua nikupe siri yote kwa kujiamini”  
(uk:19-20).

Kutokana na data hizo, mtafiti amebaini kwamba, Mzee Toboa amelandana na jina lake kwa sababu, amehusishwa na Sikujua anayemtaka amtunzie siri. Hata hivyo, baada ya kupewa siri hiyo, anakwenda kutoboa siri hiyo Polisi ili haki ipatikane. Pia, kupitia mhusika Pondamali anatumiwa na mwandishi kumsawiri kwa kumuelezea Mke wa Sikujua. Kutokana na maelezo, tumeweza kumuelewa Pondamali kuwa, alikuwa akifanya mapenzi na mke wa rafiki yake. Tumeitambua tabia ya Mke wa Sikujua kupitia Pondamali pale alipomueleza Sikujua kwa uchungu. Kwa mfano tunaelezwa.

“...hasira yake ilimfanya aseme maneno mengi, hadi kumtolea siri ya maudhi ambayo mimi sikuwa naifahamu. Aliniambia eti mke wangu kamfilisi! Kila siku alidai fedha na starehe zingine ambazo zilimfanya ashindwe kuweka fedha, na kwamba muda wake mwingi wa kazi alikuwa akiupoteza kwa mke wangu mimi niwapo kazini...”  
(uk. 28).

Hivyo, mtafiti amegundua kuwa, mke wa Sikujua analandana na jina lake kutokana na kuhusishwa na mhusika Pondamali ili kufichua tabia yake aliyokuwa nayo ya kufanya mapenzi na Pondamali. Alishindwa kujua kuwa mapenzi nje ya

ndoa ni fedheha na hakuna siri ya watu wawili. Mwisho, siri yao ya mapenzi imeanikwa juani na Pondamali na hatimae anajuta.

#### 4.6.6 Mbinu ya Kidrama

Baada ya mtafiti kukusanya data na kuzichambua aligundua kwamba, katika riwaya ya *Kiu ya Haki*, wapo baadhi ya wahusika waliosawiriwa majina yao kwa mbinu ya kidrama kama ifuatavyo:

Mtafiti amebaini kwamba, Mzee Toboa ni mhusika ambaye ametumia mbinu ya kidrama kati yake na Mama Asha. Wakati Toboa anamshauri mke wake kuripoti na kuzipeleka fedha alizopewa na Sikujua Polisi. Mama Asha haungani na mume wake katika shauri hili, anatawaliwa na tamaa ya kupata fedha, ili anunue vitu vingi vya thamani. Mjadala huu wa kidrama unajidhihirisha kama ifuatavyo:

“Mzee Toboa: Fedha usizozitolea jasho mke wangu, alisema Toboa kwa sauti nzito, ” huyeyuka kama barafu. Zitayeyuka mikononi na kutuagamiza.

Mama Asha: Kama kawaida yako, alisema kwa dharau Mama Asha, nilijua tu ungesema hivyo,” kabisa? Nimechoka na mahubiri yako!

Mzee Toboa: Fanya subira mke wangu, usiwe na papara. Fikiria kwanza ndio unijibu, kumbuka kuwa bure ghali, Mama Asha. Alisema Mzee Toboa kwa sauti ya mkazo (uk.33).

Majibizano hayo, yanatuunganisha na kutuonyesha kuwa Mzee Toboa analandana na jina lake kwa tabia yake ya kupenda haki itendeke ambapo baada ya kupata taarifa huzipeleka Polisi. Pia kwa upande wa Mama Asha naye pia analandana

na jina lake kwa kule kuwa na tama ya kupata vitu vingi vya thamani kama vile mkufu wa dhahabu, nguo nzuri akiwa kama mama na mke wa Toboa na akiwa mwanamke.

Wahusika wengine waliotumia mbinu hii ni kati ya Inspekta Pwagu na Sikujua. Inaelezwa kwamba, Pwagu alipokwenda nyumbani kwa Sikujua kwa lengo la kumtaka ampe pesa ili amsaidie katika kesi ya mauaji ya Pondamali aliyoifanya Sikujua, kulikuwa na mjadala wa kidrama baina ya wahusika hao. Kama tulivyoielezwa na msanii:

Inspekta Pwagu: ....ee, bwana nimekuja kukunong'oneza kuhusu jina lako kutajwatajwa katika kesi ya mauaji ya Pondamali.....

Sikujua: Natajwa! Natajwa vipi Bwana Inspekta? aliuliza Sikujua. Alikuwa karibu kuzimia kwa masikitiko. Matone mazito ya maji yalionekana kwenye paji la uso wake. Macho yalikuwa yamemtoka kama samaki mbichi aliyevuliwa dakika chache zilizopita!.

Inspekta Pwagu: Inavyoonekana wewe ndiye aliyemuuwa rafiki yako Pondamali. Aliendelea Inspekta Pwagu kumtia moto Sikujua... (uk:51-52).

Inspekta Pwagu analandana na jina lake, kama inavyoonekana katika mazungumzo yao na Sikujua kutoka na tabia yake ya kutokuwa na uaminifu katika kazi yake na kudiriki kuchukua hongo, huku akisahau miiko na madili ya kazi yake. Pia Sikujua analandana na jina lake kama inavyoonekana hapo, anaendelea kutoa hongo huku akishindwa kuelewa njia hii itaendelea kumpa fedheha nyengine.

Wahusika wengine waliotumia mbinu ya kidrama ni kati ya Wakili Mtayaona na majambazi Killa, Somba na Kazamoyo, kwa mfano katika (uk.58-59), tunashuhudia mazungumzo ya mahojiano ya Wakili Mtayaona na Killa, Somba na Kazamoyo kuhusu kesi ya mauaji ya Pondamali yaliyofanywa na Sikujua.

Mhusika, Mtayaona analandana na jina lake hasa pale anapowahoji majambazi hayo na kuwabana hadi wakaongea ukweli na watu wote waliokuwepo Mahakamani wakaona.

Pia, data zinaonesha kwamba, majambazi Killa, Somba na Kazamoyo yamesawiriwa kwa upande mwingine kwa kutumia njia hii ya kidrama. Kwa mfano, Kazamoyo yeye anakaza moyo wake na kuzungumza ukweli wa mambo ulivyokuwa. Kwa mfano tunaelezwa:

Mtayaona: Kwa hiyo unakubali kuwa mlikuwa ndani ya gari la marehemu?.

Kazamoyo: Ndiyo siwezi kupinga uamuzi wa alama za vidole, lakini tuliwahi kuingia katika gari la marehemu kabla ya kifo chake.

Mtayaona : Lini taja tarehe na siku.

Kazamoyo: Sikumbuki (uk:61-62).

Pia, mbinu hii ya kidrama imetumika kwa mhusika Inspekta Pwagu na askari wengine wawili dhidi ya Mzee Toboa Mambo, walipokwenda kumkamata na kumpeleka kituoni kuhusu kesi ya mauaji ya Pondamali. Tumeelezwa na mwandishi:

Ofisa Upelelezi: “Habari yako Mzee?” Ofisa upelelezi mmoja ambaye hakuvaa sare alimsalimu.

Mzee Toboa: “Nzuri mabwana, nzuri” alijibu Mzee Toboa kwa shaka”

Inspekta Pwagu: “ Tunakuhitaji Mzee,” alisema Inspekta Pwagu huku anakapua macho yake’

Mzee Toboa: Kwa shughuli gani? aliuliza Mzee Toboa. Alikuwa amesimama nje ya gari lake. Hakujibiwa bali alifungwa pingu mikononi na Polisi wa pili (uk:69).

Kutokana na dondoo hizo, ni wazi kwamba, mbinu ya kidrama imewasawiri vyema Inspekta Pwagu na askari wengine wawili aliofuatana nao wanaonekana kulandana na majina yao hasa katika kutekeleza wajibu wao. Pia, uwepo wa tamaa ya kupata fedha kupitia kesi hiyo. Aidha, Mzee Toboa yeye analandana na jina lake kutokana na majadiliano yaliyomfanya akamatwe baada ya kutoboa siri ya mauaji kwa Polisi.

Mbinu ya kidrama, pia imetumiwa na wahusika Mama Asha, Mke wa Fundisha na Fundisha, pale ambapo Mama Asha alipokwenda kuwaomba wakae mashahidi katika kesi ya mumewe. Wahusika hawa wote wanalandana na majina yao, Mzee Fundisha na Mama Fundisha wanakubali kukaa mashahidi na kutoa fundisho kwa wengine kuwa hakuna siri ya watu wawili na vitendo viovu malipo yake ni maovu. Kwa mfano tunaelezwa;

Mama Asha: “Shoga yangu,” alianza kueleza Mama Asha mara tu walipofika chumbani,” umefanya vizuri sana kunipa habari za uovu wa Sikujua na wanzake. Nakuomba usichoke, tafadhali sana

nakuomba wewe na mumeo mkubali kuwa mashahidi wetu katika kesi hii, mzungumze na mumeo, mtusaidie. Tutafanya nini masikini, mambo yametufika,” alimaliza Mama Asha.

Mke wa Fundisha: Pole sana Mama Asha! nimesikia, nisubiri kwanza kidogo nikamwite,” alijibu Mke wa Fundisha ...”(uk:77).

Wahusika Mtayaona na Mke wa Fundisha pia nao wametumia mbinu hii ya kidrama. Wakili Mtayaona anatekeleza wajibu wake Mahakamani kwa kumuuliza Mke wa Fundisha hatua alizifichukua baaada ya kupata ushahidi wa mauaji. Tunaelezwa na msanii kuwa:

Mtayaona: Mama Fundisha, unaweza kutuambia ulichukuwa hatua gani baada ya kupata kisa chote cha kifo cha Pondamali kutoka kwa Mke wa Sikujua?

Mke wa Fundisha: Nilimweleza mume wangu tu. Niliogopa kupeleka habari hizi Polisi kwa wasiwasi wa kuweza kujulikana kwa Sikujua..(uk. 80).

#### **4.7 Dhamira Zinazojengwa na Wahusika wa *Kiu* na jinsi Zinavyolandana na Majina yao**

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), anaeleza kuwa, dhana ya dhamira ni jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake. Tunaweza kutambua maana ya kazi fulani kwa kuisoma kazi hiyo kwa kina na makini, huku tukielewa na kutambua uhusiano wa visehemu mbali mbali pamoja na jinsi visehemu hivyo vinavyohusiana na kazi

nzima na kuvyanza kitu kimoja. Visehemu vilivyoelezwa na Wamitila ambavyo huweza kutupatia dhamira ni pamoja na wahusika, muundo na mtindo, msuko na mandhari.

Katika riwaya teuliwa, mtafiti alichunguza kipengele cha majina ya wahusika na namna majina hayo yanavyoibua dhamira za mwandishi wa riwaya hizo teuliwa.

Mtafiti aligundua kuwa zipo dhamira zinazolandana na majina ya wahusika hao.

Katika riwaya ya *Kiu* zimejitokeza dhamira za Mapenzi, Utamaduni, Malezi, Ujirani, Ulevi, Umasikini na Ujasiri ambazo mtafiti baada ya kuchambua data aligundua kuwa zimelandana na majina ya wahusika wa riwaya ya *Kiu* kama ifuatavyo:

#### **4.7.1 Dhamira ya mapenzi**

Katika riwaya ya *Kiu*, suala la mapenzi limejitokeza katika sura tofauti. Msanii anaamini kuwa, mapenzi ni jambo la hiari ya mtu. Wapo wanaopendwa lakini wao binafsi hawawapendi wanao wapenda. Msanii amesawiri wahusika watatu Mwinyi, Idi na Bahati, wote wakiwa na kiu ya mapenzi kwa viwango tofauti.

Kwanza, msanii amemuonesha Mwinyi, mzee wa miaka sitini na mbili akiwa na kiu ya kumpata Bahati, ili awe mpenzi wake na ikiwezekana waishi kama mke na mume. Mwinyi anategemea taarifa za faraja kutoka kwa Idi, ambaye ndiye aliyemtuma kuzungumza na Bahati kuhusu suala la mapenzi. Hata hivyo mambo hayakuwa kama alivyoyatarajia. Mwandishi anatueleza hilo kwa kusema:

“Punde hivi, dereva wake aliingia bila ya kubisha hodi, Mwinyi alishtuka na kumuuliza” Mbona umekawia”?



Idi ...kwa masikitiko na kusema, nimekuta kufuli mlangoni”

Maneno yake yalimkata Mwinyi ini lake. Alishuka mabega akanyweya juu ya kiti, akaona maisha yakimuoneya, kusubiri na kusiko na kikomo. Miezi sita imepita tena na kutamani kusiko danganyika? yote haya aliyaona yanamtwisha. Alikuwa amekwisha vumilia vya kutosha, bado hakujua ni lini siku ya faraja (uk:7-8).

Msanii ameonesha kuwa suala la mapenzi halina umri maalumu, ni jambo la kawaida kwa mwanadamu anaekula akishiba na mzima wa afya. Mwinyi alikuwa tajiri mkubwa, lakini, utajiri wake wote aliokuwa nao, haukuweza kumpatia alichokitaka, ili aondoe kiu yake. Utajiri wake haukuwa na maana kwa wakati ule kwasababu, ulishindwa kutosheleza kiu yake. Kitu cha pekee ambacho hakiwezi kununulika na kupatikana kwake kulitegemea zaidi masikizano kuliko utajiri wake alionao. Lakini, mtu mwenyewe hakuonekana rahisi na mwepesi wa kuridhia kutokana na tadi na kiburi alichokuwa nacho. Kiu hii ya mapenzi ilikuwa ghali kuweza kuipoza na kuiondoa katika nafsi yake iliyokuwa ikimkosesha raha maishani mwake.

Pia, msanii ameonesha jinsi Mzee Mwinyi alivyokuwa haoni mbele wala nyuma. Mawazo yake yote yalikuwa katika kuondoa kiu yake ya mapenzi.

Dhamira hii ya mapenzi imelandana na jina la Bahati. Kama ilivyoelezwa awali kuwa, Bahati mtoto wa kimaskini alipata bahati ya kupendwa na tajiri ingawa Bahati hakumpenda Mwinyi. Pia, Bahati anapata bahati ya kupendwa na Idi, ingawa, Idi alimpenda kwa lengo la kumfanya kama chanzo cha mapato. Aidha

Bahati anapata bahati ya kupendwa na mama yake kupindukia akiwa kama mtoto wa pekee katika familia ya Cheusi na Jaku.

#### **4.7.2 Dhamira ya Utamaduni**

Kwa mujibu wa Manzi (2007), utamaduni ni pamoja na mila, desturi, itikadi za jamii fulani, ambazo huzifuata katika maisha yao ya kila siku. Mohammed S. Mohammed katika riwaya ya *Kiu* ametumia mandhari ya Zanzibar katika kusawiri vyema dhamira yake ya utamaduni hasa katika utamaduni wa ndoa. Msanii ameonesha kuwa, kabla ya kufanyika kwa arusi, wanawake hupewa mafunzo ya unyago wanapopata ukubwa (kuvunja ungo), ili kuwaandaa kuweza kumudu nyumba zao. Hivi ndivyo alivyokuwa Bahati binti Jaku, ambaye tunaelezwa kuwa, Bi Mvita alimpa mafunzo ya unyumba wakati alipovunja ungo. Kwa mfano;

“Mwanangu unasema wiki ijayo?” Cheusi alimuuliza,” husemi mwezi ujao? Kuna somo yake Bi Mvita, ndugu zangu, wahisani wangu, hao wote lazima niwapate tushirikiane. Hasa Bi Mvita lazima awepe, alimtambikia sana huyu mtoto alipovunja ungo, anampenda kana kwamba kamzaa mwenyewe.”(uk:63)

Vilevile, ili ndoa ikamilike kisheria ni lazima iweze kuzingatia taratibu za watu. Posa ni ishara ya kufanyika kwa tendo la arusi. Utamaduni huu umekuwa ukitumiwa sana na jamii za Zanzibar kwa lengo la kujenga heshima na maadili ya jamii. Hivyo, pia tumeelezwa kuwa Idi alikwenda nyumbani kwao Bahati na kupeleka posa.

“Alhamis, mfunguo sita, ilikuwa ni siku iliyobarikiwa faraja kwa Bahati. Mambo yalikuwa kangaja, maana siku ile Idi alifika Selea kwa mama yake kuleta posa .

Posa ilipokelewa kwa furaha na vigelegele. Kwa mara ya kwanza kabisa, Idi aliyaona meno ya Bi Cheusi, mama yake Bahati, atakaekuwa mkwewe...” Inshaallah mwanangu, kusudi iwe ndoa ya heri, awe mkeo, mkae msikizane, mzae kama mlivyojaliwa nyinyi...”(uk:62).

Unyago ni mafunzo mengine ya kiutamaduni anayopewa bi harusi, ili kuendelea kukamilishwa taaluma ya kumkabili mume. Kwa kawaida mafunzo haya hupewa harusi kutoka kwa watani wake, wifii, ama hata somo yake aliyempa mafunzo wakati alipovunja ungo. Katika harusi ya Bahati, Bahati alipata fursa ya kupewa mafunzo haya chini ya uongozi wa Bi Mvita, mtu ambaye alimpa mafunzo wakati alipovunja ungo. Mwandishi anatueleza haya kwa kusema:

“Jioni unyago ulianza. Wapigaji walikaa uwani na wachezaji waliojifunga vibwebwe, wanawake vijana, waliwazunguka wapigaji, wakatapaka hadi jikoni na ukumbini, mpaka nje, uani. Cheusi, Hadija, na binti Jaku wakiwatunza wachezaji, ambao wakipokea tunza zao kwa midomo, wakizidi kukatika ...” njoo nikubebe!” Bi Mvita alimkaripia .” unaogopa kitu gani?”

Hapo Bahati akajizoa kitandani, na kukaa kifudifudi mgongoni. Bi Mvita alinyanyuka naye taratibu huku akimweka vizuri na kisha akatoka naye. Hadija akapaza sauti na kuimba:

“Bibi aingilie chooni;  
 Aingilie koga marashi  
 Uvumba na udi....” (uk. 70-71)

Mhusika Bi Mvita analandana na jina lake na kusababisha kutokea kwa dhamira ya utamaduni kutokana na tabia yake ya kupiga vita masuala yanayoenda kinyume na mila, silka na destururi za utamaduni wetu, huku akisisitiza kufanyika kwa masuala muhimu ya utamaduni wa jamii.

#### **4.7.3 Dhamira ya Malezi**

Mtafiti amegundua kwamba, mwandishi wa riwaya ya Kiu amelieleza suala la malezi kuwa, linahitaji mashirikiano ya baba na mama. Kukosekana kwa hayo hupeleka mtoto kukosa baadhi ya mbinu na hata kuweza kujiingiza katika vitendo vibaya vinavyokiuka mila za jamii.

Kwa mawanda mapana Mohammed S Mohammed ameweza kusawiri dhamira hii ya malezi kwa kupitia Cheusi ambaye anamlea mwanawe kwa tabu na dhiki sana baada ya mume wake kuondoka kwenda Kongo. Hali hii inamfanya Cheusi akose ushirikiano na ushauri juu ya malezi ya mtoto wake hasa pale Bahati alipoanza kuhusiana na Idi kinyume na maadili ya jamii yao.

Cheusi pia anakumbwa na maisha mazito, na inambidi afanye kazi ya kuuza maandazi, ili ayamudu maisha. Cheusi hakubaliani na mwenendo wa mwanawe. Daima anakuwa mkali lakini wapi, Bahati anatoka nje ya nyumba yao na kurejea nyakati za usiku. Msanii anatueleza hilo kwa kusema:

“Ah! mwanangu we, sasa naona umezidi tena!”, Cheusi alinena lakini Bahati akawa kimya; ah, fisadi wa roho yako we, unajiharibu namna hii? mtoto mwenye wazee wako, uliezaliwa ukazalika ukalelewa kwa viganja vya mikono, leo unajichafua namna hiyo? Hebu sema, ulikwenda wapi tangu asubuhi ya Mungu? sasa kwa nini umerudi hapa usilale huko huko kwa mwanamme wako?”

Duniani nitakaa na nani mimi. Baba yako kanikimbia!” Alianguka kitandani na kuanza kulia kwa kwikwi, kisha akamshika mkono na kumwita.... Siyo kusudi langu kukuumiza, mwanangu. Lakini nimefanya hivyo ili kutimiza wajibu unipasao kwako, nikiwa mzazi na mlezi wako....” (uk:46-47)

Mtafiti amegundua kwamba, dhamira hii ya malezi imelandana na jina la mhusika Cheusi. Kwasababu, jina hilo, limechorwa kiishara juu ya matatizo yanayomkumba Cheusi katika suala la malezi, likiwa na maana ya matatizo na tabu. Hali hiyo, inawiyana na matukio yanayomtokea Cheusi baada ya kukimbiwa na mume wake, huku nyuma akikabiliwa na hali ngumu ya maisha pamoja na kumlea Bahati. Aidha, Cheusi anakabiliwa na hali ngumu ya malezi ya mtoto wake, Bahati baada ya kuanza kufanya mapenzi kabla ya ndoa. Jambo hilo lilimtia wasiwasi sana katika maisha yake.

#### **4.7.4 Dhamira ya Ujirani**

Ni kawaida ya jamii nyingi za Kiafrika kuhusiana katika maisha yao kama majirani. Aidha, jamii hushirikiana katika mambo mbalimbali kama, vile arusi, malezi, msiba nakadhalika.

Mtafiti alichambua data na kugundua kuwa, dhamira ya ujirani imesawiriwa vyema na mwandishi wa *Kiu*. Kupitia mhusika Bi Songoro, Salama na Mwandawa. kwanza, Salama; jina hili limetoholewa kutoka katika lugha ya Kiarabu likiwa na maana ya amani. Mhusika huyo anajenga mashirikiano mema katika shughuli ya harusi ya Bahati. Anashirikiana na Cheusi kufanikisha arusi ya Bahati. Hali hii inampa faraja na matumaini mema Cheusi na kuwa na amani katika kufanikisha furaha yake iliyokuwa ndoto katika maisha yake ya kutaka mtoto wake aolewe, ili asaidiwe ulezi ambao ulikuwa umemwelelea peke yake mara baada ya mume wake kuondoka.

Pili, Mwandawa; jina linalomaanisha kitu chenye kuondoa matatizo. Mhusika huyu anatoa mashirikiano ya dhati kwa Bahati katika kufanikisha harusi akiwa ni miongoni mwa jirani mwema.

Aidha, neno “songoro” kwa mujibu wa (BAKIZA, 2010), lina maana ya samaki mwenye rangi ya dhahabu na kufanya awe na mvuto kwa watu. Mwandishi anatueleza hilo kwa kusema:

“Ndugu yangu unifae kwa langu nikufae kwa lako. Wageni wamezidi nataka uniazime nyumba yako,” alisihi.

“Ah , mpenzi wangu we, nyumba gani hii ya kukaribisha wageni?” alijibu.

“Haidhuru, dada. Kupata si kukosa, sina la kufanya” Haya basi wakaribishe. Ngoja nifagie kidogo”

“Bwana je, hatakasirika?” Cheusi alimuuliza?” Mimi nikishakubali  
 bwana hana maneno” Binti Songoro alimjibu huku ameshika  
 ufagio.”(uk:62).

Mhusika Binti Songoro analandana na dhamira ya ujirani kutokana na matendo na tabia zake njema kwa Cheusi. Tunaeleza kwamba, binti Songoro anamuazima nyumba Cheusi, ili wafikie wageni wake wengine wanaokuja harusini. Kutokana na kitendo chake hicho anakuwa ni jirani mwenye mvuto mbele ya Cheusi na Bahati.

#### **4.7.5 Dhamira ya Ulevi**

Mtafiti amebaini kwamba, mwandishi anaona ulevi ni tatizo kubwa lililoivamia jamii. Watu wengi wamekuwa wakitumia ulevi wa kupidukia hasa pale wanapokuwa na kipato kikubwa. Sula la ulevi limekuwa likifanyika sana hasa wakati wa kusherehekea siku za sikukuu. Matokeo ya ulevi ni kupoteza pesa nyingi pamoja na kuathiri afya ya mtumiaji.

Dhamira hii ya ulevi imejitokeza zaidi kwa mhusika Idi ambaye ni miongoni mwa wahusika wakuu wa riwaya hii ya Kiu. Msanii anaonesha kuwa, miongoni mwa matendo yasiyo na utu ni ulevi kwani, mtu anapolewa hupotewa na akili na huwa na maamuzi magumu ambayo katika hali ya kawaida si rahisi kuyatoa. Tabia ya kunywa ulevi huchangiwa na fursa ya kipato alichonacho mtu. Kwa mfano, tunaoneshwa kuwa, fedha ndio nyenzo iliyotumiwa na Idi katika kuendeleza tabia ya kunywa ulevi. Msanii anatueleza hilo kwa kusema:

“Baadae, Idi alijidai anakwenda haja. Alitoka majini akaingia chumbani, akafichua chupa yake ya mvinyo na kuipiga mafunda ya

haraka. Kisha akafuta midomo na kutafuna chembe ya karafuu na kubabaisha harufu, kwani Mwinyi alikuwa hapendi pombe” Akarudi majini na kuogelea” (uk. 12)

Vilevile, msanii anatueleza kwamba tabia ya ulevi ya Idi ilikuwa kero na maudhi makubwa kwa mkewe. Wakati mwengine Idi alijitapikia kitandani na kumpa harufu ya matapishi mke wake. Starehe ya ndoa kwa Bahati haikuwepo kabisa. Daima yeye aliishi kwa hofu kubwa. Hakuwa na maamuzi wala ushauri alioweza kuutoa kwa mumewe na ukakubaliwa. Hayo yote yalisababishwa na tabia ya ulevi. Msanii anatueleza:

“Bahati hakutarajia jema lolote. Alipoikuta fodi ya rangi ya maziwa mlangoni badala ya bandani, mlango wake wazi, na ndani mnatanda matapishi, hakustaajabu, kwani mtu hustaajabu mageni” (uk.89).

Pia, msanii ametuonesha Idi anavyodiriki kulala nje ya nyumba yake kwa siku kadhaa huku akishiriki ulevi na kustarehe na wanawake. Baya zaidi ni kitendo akifanyacho cha kulewa na kuchukuwa wanawake ndani ya nyumba yake huku akitoa maneno ya dharau kwa mke wake wa ndoa. Mwandishi anasema:

....Aliona bora amvue na viatu; akamvua. ...pamoja na ile ya ulevi na matapishi harufu ngeni ya mafuta mazuri ya kike. Mbio alipitisha pua yake kifuani pote, hadi shingoni, mpaka kwapani, kama mbwa anaenusia harufu ya mnyama aliejificha kichakani. Harufu ya mafuta ya kike ilikuwa imehanikiza. Aliondoka asimfungue tena, akamsimamia huku amekaza meno, moyo wake ukapiga kwa ghadhabu, jasho limemtanda..... (uk:90-91).



Dhamira ya ulevi imelandana na jina la mhusika Idi, kutokana na neno “idi,” ni miongoni mwa sikukuu za Kiislamu, ambapo watu siku hizo hula vizuri, huvaa vizuri na kunywa vizuri ingawa watu wengine huenda kinyume kwa kunywa ulevi, kufanya uzinzi, wizi na ujambazi na aina nyengine za uhalifu. Aidha, siku ya Idi, watu wengi huishi maisha ya anasa ingawa hawana uwezo huo. Hivyo, mhusika Idi analandana na dhamira ya ulevi kutokana na tabia yake ya kutumia ulevi kama ni anasa, ikiwamo uzinzi kama wafanyavyo watu wengi katika siku ya Idi.

#### **4.7.6 Dhamira ya Umasikini**

Umaskini ni hali ya mwanadamu kushindwa kupata mahitaji muhimu ya msingi katika maisha yake kama vile chakula, mavazi, makaazi na matibabu katika hali ya kawaida. Katika kuchambua data mtafiti aligundua kujitokeza kwa dhamira ya umasikini.

Mtafiti alichambua data na kugundua kuwa, Mohamed S. Mohamed amepiga tochi katika jamii na kugundua kuwa, suala la umasikini bado ni tatizo kubwa lililoiigubika jamii. Ameonesha kuwa, miongoni mwa sababu zinazochangia uwepo wa hali hii ni kutawaliwa na wakoloni ambao wao waliuhujumu uchumi wa nchi. Kwa mfano, msanii anaeleza:

“...ua wenyewe haukuwa mkubwa, kuta mbili za kimo cha mtu mrefu ziliunga nyumba na banda. Hilo banda ndilo lililokuwa na jiko na choo, nafasi ile ya ua ilisaidia kuweka vitu ambavyo havikufaa kukaa bandani wala nyumbani...Upande mmoja palikuwa na jaa la vyombo vilivyochoka kutumika, mbuzi mbovu ya kukunia nazi, ndoo

iliyotoboka, mtungi wenye pengo, na takataka zingine. Cheusi alisema ni vibaya kutupa kitu kisichofaa” (uk:23-24).

Aidha, data zinaonesha kwamba, ilikuwa vigumu kupata hata kile cha kutia mdomoni. Msanii anatueleza kwamba, kutokana na hali ya umasikini iliyomkumba Cheusi ilikuwa vigumu kupata hata cha kutia mdomoni. Kwa mfano tunaelezwa:

“Bahati na mama yake walikuwa wamekwisha lemaa katika umaskini, hasa tangu kuondoka kwa mwenzao Jaku, baba yake Bahati, maisha yalikuwa ya tabu na dhiki.. (uk. 28).

Licha ya kuwa na maisha magumu kwa Cheusi na Bahati, lakini pia mwandishi ametueleza kuwa, umasikini umeathiri hata malezi ya mwanawe, Bahati na kumfanya ajiingize katika mahusiano na Idi na Mwinyi kinyume na taratibu na mila zao, kiasi ambacho Cheusi anajikuta kujenga mazoea ya kumkemea mwanawe kila wakati, ili mwanawe afuate mila zao. Msanii anatueleza kuwa:

“Alipokuwa akimfokea hivi mwananwe, Cheusi alionesha uso wa kutisha lakini uliojaa huzuni, utu uzima, umasikini na malimwengu kama viliashiria kumpokonya uzuri wa sura yake. Sasa uso ulibadilika ukawa mweusi, umechujuka na mwili wake, wote ukawa na alama za kuvumilia kwa shida... Alifanya hivyo kujaribu kumfumbua macho aone hatari iliyomkabili, aepuke, aokoke, arejee katika salama. (uk:26).

Hivyo, dhamira ya umasikini inlandana na jina la mhusika Cheusi, kutokana na maisha ya umaskini aliyonayo mhusika huyo. Tunaelezwa kuwa Cheusi alikuwa

akiishi katika nyumba ndogo, kongwe na chakavu ambayo ina kila dalili ya hali ngumu ya maisha.

#### **4.7.7 Dhamira ya Ujasiri**

Mtafiti amebaini kwamba, dhamira ya ujasiri imejitokeza zaidi kwa mhusika Mwajuma na Bahati. Suala la ujasiri limeambatana na uwepo wa kutofanyika haki kati ya Idi na Bahati katika mfungamano wa maisha ya ndoa yao. Kitendo cha kudhalilishwa kwa Bahati na mumewe kinamkera sana Mwajuma kama yeye ni mwanamke mwenzake. Hivyo, Mwajuma anaamua kumkabili Bahati na kumueleza ukweli wote kuhusu tabia ya Idi ya kuja na wanawake ndani ya nyumba yake na kunywa ulevi na hatimae kufanya mapenzi. Hali hii ilitokea baada ya Bahati kumueleza hali halisi ya maisha ya ndoa, ambapo Idi hamthamini, na hamtendei haki kama mke na mume. Mwandishi anaeleza:

“Kuwa mimi ni mke ningemstahamia mume wangu kwa yote isipokuwa kunila kivuli, ulevi sio kitu, umasikini sio kitu, domo si kitu, ingawa yote si mazuri, kunizinia nyuma yangu kunifanya mimi si mwanamke kitu baada ya kunichagua mwenyewe; hilo nisingekubali. Bora niishi mjane kuliko kuwa na mume kama huyo.....wiki mbili hizi nilizokaa hapa, bibi niliyoyaona ukitendewa mimi yamenitia huzuni, je wewe unayetendewa?...ulipokuwa spitali nilimuona mumeo akija na mwanamke siku zote, akilala naye juu ya kitanda kile kile ambacho ni haki yako wewe tu, bibi... (uk.110-111).

Katika jitihada za kumweleza ukweli, Mwajuma anapanga mpango wa kumwonesha jinsi atakavyofanikiwa kumfumania mumewe. Hivyo, anamshauri

Bahati amuage mumewe kuwa anakwenda kwao kwa siku kadhaa na mara arudi nyumbani kwake ghafla bila Idi kuelewa dhamira yake. Bahati anashindwa kujizuia na kilio wakati akielezwa hali halisi ya mumewe. Hata hivyo, anapata nguvu mpya baada ya kupewa mpango huu na kupiga moyo konde. Tunaeleza na mwandishi:

“Nyanyuka upanguse, machozi; bibi, hiyo ni kazi ndogo tu,  
ukiondoka nyumbani siku moja tu, nyuma yake atamleta” (uk.112).

Bahati anakubaliana na mawazo ya Mwajuma. Hili linadhihirika juu yake pale aliposema:

“Mwajuma leo nitamwaga nakwenda kwa mama kukaa wiki moja”  
(uk:112)

Dhamira ya ujasiri inlandana na jina la mhusika Mwajuma. Jina la Mwajuma linaashiria ujasiri, kujiamini, ustahamilivu na uhodari. Hivyo, ni wazi kwamba, jina hilo limelandana na dhamira ya ujasiri, kutokana na ujasiri wa Mwajuma wa kumshughulikia Mzee Mwinyi katika umri wake wote hadi anafariki. Aidha, Mwajuma anatumia ujasiri na kutoa siri za Idi kwa Bahati bila kujali linaloweza kumtokea.

#### **4.8 Dhamira Zinazojengwa na Wahusika wa *Kiu ya Haki* na jinsi Zinavyolandana na Majina Yao**

Baada ya kukusanya na kuchambua data mtafiti alibainu kujitokeza kwa dhamira ya Haki, Rushwa, Ujambazi, Siri, Umuhimu wa Elimu na Ukiukwaji wa Sheria ambazo zinalandana na majina ya wahusika katika riwaya ya *Kiu ya Haki*, kama zifuatavyo:

#### 4.8.1 Dhamira ya Haki

Kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010), haki ni jambo linalomstahikia mtu alipate. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa haki ni jumla ya mambo ama vitu, fursa, inayostahiki mtu aipate kutoka kwa mtu mwengine, kikundi cha watu, serikali ama taifa.

Baada ya kukusanya na kuzichambua datas, mtafiti aligundua kwamba, katika riwaya ya Kiu ya Haki, bado jamii imekuwa ikikosa haki zao mbali mbali kutokana na kushamiri kwa dhulma katika maeneo tafauti. Kwa mtazamo wake mwandishi anaona ni lazima juhudi ifanyike, ili hali hii iondoke. Aidha, mwandishi ametuonesha mgogoro baina ya watetezi wa haki yaani Mzee Toboa, Mama Asha, Jaji Utakunywa na Inspekta Mtayaona, dhidi ya wale wanaopinga haki ambao ni, Sikujua, Jaji Pwagu na Inspekta Pwaguzi. Mgogoro huu umeibuliwa kutokana na kuuwawa kwa Pondamali kulikofanywa na Sikujua.

Msanii amemuonesha Mzee Toboa mara sbaada ya kuzipata taarifa zinazohusu mauaji akizipeleka katika vyombo vya sheria ili haki ichukue nafasi yake. Kwa mfano, tunaeleza na msanii:

“Baada ya kusalimiana Mzee Toboa hakupenda kupoteza muda, hivyo alimweleza Paukwa kilichompeleka ofisini mwake asubuhi ile. Alimtobolea kisa chote cha kifo cha Pondamali kama alivyoeleza na Sikujua” (uk. 35).

Katika kusawiri vyema dhamira hii, mwandishi ametuonesha kwamba haki imeambatana na mambo kama vile rushwa, hongo, tamaa kwa wenye dhamana ambayo yote haya yanapelekea haki kutokufanyika na kutowafikia wale wanaostahiki kutokana na jamii kukaa kimya.

Kwa mfano, tumeoneshwa jinsi Jaji Pwagu ambaye amekabidhiwa kusimamia kesi ya mauaji ya Pondamali anavyoigeuza kesi hiyo kuwa njia ya kuchuma mali.

Msanii anafafanua hili kwa kusema:

“Pwagu alipata wazo la kutumia kesi hiyo kuchuma fedha. Miiko na desturi za kazi yake zinakataza uchumaji wa mali kwa njia hiyo aliyokuwa wanaifikiria. Alikunja ngumi na kuinua juu mkono wake wa kiume, “Ni ngumu fikra za chama na serikali,” alisema kimoyomoyo...jinsi alivyozidi kulisoma jalada la kesi ya mauaji, ndivyo wazo la kupata pesa za haraka lilivyozidi kumtawala. Tamaa ya kuchukuwa pesa kwa njia hiyo ilimpagaa....” (uk: 45).

Pwagu ni Inspekta wa Polisi, anayefanya kazi ya kutoa hukumu ya kesi mbali mbali lakini anafanya kazi yake kwa misingi ya dhuluma. Ndivyo walivyo baadhi ya wengine wenye dhamana kama ya Pwagu.

Vilevile, mwandishi anatubainishia kwamba, suala la kutetea haki linaambatana na matatizo mbali mbali, ambayo huwafikia watetezi wa haki. Mathalan, Mzee Toboa aliwekwa pingu na kutupwa korokoroni, anakoswa koswa na risasi wakati alipotoboa siri ya meneja wa kampuni kuhusu suala la kufanya magendo ya mkaa. Pia, Mzee Toboa anatengana na familia yake siku kadhaa na kukosa kuendesha

biashara yake ya teksi kwa sababu ya kutetea haki. Haya na mengine mabaya yanaweza kutokea kwa wanaotetea haki. Kutetea haki kunahitaji kujitoa mhanga kama alivyo Mzee Toboa. Tunaelezwa na mwandishi:

“...Hapo ikawa vita baina ya Mzee Toboa na meneja wa mkaa. Meneja alivamia nyumba ya Toboa saa za usiku. Alipiga risasi chungu mzima kupitia dirishani lakini kwa bahati nzuri hazikuwapata, lakini cha moto walikiona. Walijawa na wasiwasi, wakaona maisha yao yamo hatarini.” (uk: 35).

Licha ya kuwepo kwa mapambano baina ya watetezi wa haki na wavunjao haki, mwandishi anatueleza kuwa, siku zote haki itaendelea kushinda mbele ya batili, mfano mzuri ni ule uhusio kesi ya mauaji ya Pondamali. Baada ya uchunguzi kufanyika wote wenye makosa Sikujua, Somba, Killa, Kazamoyo, Fundisha na mke wake wanapewa adhabu kwa mujibu wa makosa yao. Jaji Utakunywa anatumia sheria ya nchi kutoa hukumu ifaayo, kama tunavyoelezwa,

“Baada ya kuchambua maelezo kutoka kwa washtakiwa wote na ushahidi uliotolewa, sasa natoa adhabu kwa wenye hatia,” aliendelea Jaji Utakunywa. Somba, Killa na Kazamoyo, wanahukumiwa kifungo cha miaka mitano na kazi ngumu kila mmoja kwa kosa la ujambazi. Mzee Fundisha na mkewe wanatozwa faini ya shilingi 300/= kila mmoja kwa kosa la kumficha muuaji...”.

Sikujua amepatikana na hatia ya kuua kwa makusudi. Mahakama hii haina adhabu nyingine ya kumpa bwana Sikujua bali, adhabu ya kunyongwa hadi afe!.” (uk. 89-90).

Dhamira ya haki inlandana na jina la Mzee Toboa, kwa sababu daima Mzee Toboa amekuwa akitoboa siri za waovu katika vyombo vya sheria, ili haki ipatikane. Mzee huyu anafanya hivyo bila hofu yoyote. Aidha, katika kufanikisha dhamira hii, mhusika Utakunywa, jina hilo inlandana na dhamira ya haki kutokana kitendo cha kuwanyesha hukumu wale wote wanye kupinga haki.

#### **4.8.2 Dhamira ya Rushwa**

Rushwa ni hongo anayotoa mtu kumpa mwengine kwa lengo la kupinga utaratibu maalum uliowekwa. Waswahili husema; “Rushwa ni adui wa haki” kufuatana na msemu huu, mwandishi anatueleza kuwa, rushwa imekithiri sana hasa katika vyombo vya sheria ambapo haki zimekuwa zikikosekana. Kwa mfano, tunaeleza kuwa, Polisi wanakwenda kwa Mzee Fundisha hotelini kwake na kuchukua rushwa. Msanii anaeleza:

“Njia fupi ni kumnyamazisha yule aliyetutuma kumpa chochote mzee na mambo yatakwishia,” alitamka yule Polisi wa kwanza kwa aibu kidogo. “Tena usiwe na wasiwasi. Akishapokea chochote basi, hatathubutu kukufuata tena,” aliongeza Polisi wa pili”. Mzee Fundisha aliingia chumbani, akachukuwa shilingi 2,000/= na kuwakabidhi hao Polisi. Nao bila kuuliza swali zaidi walipokea na kuondoka huku maneno ya kumpooza Mzee Fundisha yakiwatoka (uk: 9).

Vile vile, mwandishi anamtumia mhusika Pwagu na Pwaguzi ambao ni majaji wa Mahakama Kuu wakichukua hongo ya shilingi laki moja kutoka kwa Sikujua, ili wamsaidie katika kesi yake ya mauaji. Kitendo wakifanyacho Pwagu na Pwaguzi ni



cha kikatili kwani wanachukua rushwa na kutaka kubatilisha haki. Pwagu na Pwaguzi wanasawiriwa na mwandishi kutokana na tabia yao hii ya kutokuwa waaminifu katika kazi yao. Kwa mfano tunaeleza:

“Inspekta Pwaguzi aliwaza hayo huku bado ameshikilia mtoto wa meza. Alijuwa sana miiko ya kazi yake, imani ya chama na umuhimu wake pia alivitambua vema, lakini moyo wake ulishakufa ganzi juu ya suala la kula rushwa. Alijua ubaya wa kula rushwa lakini alishindwa kuacha tabia hiyo kwani mwonja asali haonji mara moja, na asali sasa ilikuwa imemnokea!” (uk:47).

Dhamira ya rushwa inalandana na majina ya wahusika Pwagu na Pwaguzi. Hii ni kwa sababu, maneno hayo `pwagu` na `pwaguzi` yana maana ya kufanya mambo kinyume bila mazingatio. Hivyo, kitendo cha wahusika hao kuchukua hongo kinaenda kinyume na maadili ya kazi yao.

#### **4.8.3 Dhamira ya Ujambazi**

Mtafiti baada ya kuchambua data aligundua kwamba, suala la ujambazi katika riwaya hii limesawiriwa kupitia wahusika Somba, Killa na Kazamoyo. Mwandishi ameonesha jinsi ujambazi ulivyokithiri katika nchi yetu. Kwa mfano, majambazi wamekuwa wakitumia silaha za moto kuyateka nyara magari ya Sikujua na Pondamali na kufanikiwa kupora fedha na saa ya mkononi. Killa yuko tayari kuua ili apate mali, Somba hajali kitu cha mtu anasombasomba kwa kutumia nguvu na silaha, wakati Kazamoyo, anaukaza moyo wake kufanya matendo ya hatari ya ujambazi. Mwandishi anatumia kuwa:

“Abiria aliyekuwa kiti cha mbele akichomoa funguo za gari kutoka kwenye swichi akawa anazikaguwa. Yule abiria aliyenilenga bastola aliniongoza hadi kichakani, ambako alinipekua mifuko na kuchukua shilingi 200/= na saa ya mkononi. Abiria aliyebaki kwenye gari nilijua naye anafanya shughuli ya kufungua kisanduku cha fedha, ambamo mlikuwa na shilingi elfu mbili maana funguo alikuwa nazo. .... (uk. 20).

Mwandishi ametueleza kuwa, majambazi hutumia zaidi nyakati za usiku kuhujumu mali za wananchi. Kwa mfano, Sikujua tunaenezwa kuwa, aliingiliwa na majambazi wakati wa usiku na kuibiwa fedha. Mwandishi anatueleza hilo kwa kusema:

“Mzee Toboa alipofika nyumbani kwake, mkewe alimpa habari ya kusikitisha kuhusu Sikujua. Alimwambia kuwa, Sikujua aliingiliwa na majambazi usiku wa Jumanne, yani jana, saa saba na nusu usiku. Aliibiwa pesa zote na vitu vyengine”  
(uk. 40).

Pia, mwandishi anaeleza kuwa, licha ya kuwepo juhudi za kupambana na matendo ya ujambazi na mengine ya uhalifu, bado serikali inakabiliwa na changamoto kubwa kwa watendaji wake. Kwani miongoni mwa watendaji wa serikali wanaendelea kushirikiana na wahalifu ambao husababisha maovu kuendelea kadri siku zinavyoendelea. Jambo hili linaitia doa serikali na kuifanya jamii kukosa imani na viongozi wao. Kwa mfano, Jaji Pwagu na Inspekta Pwaguzi ni mfano mzuri wa viongozi wa serikali wanaotenda maovu hayo.

Dhamira ya ujambazi inlandana na majina ya wahusika Killa, Somba na Kazamoyo, kutokana na jinsi wahusika hawo wanavyoendeleza vitendo vya ujambazi. Kwa mfano, wahusika hao wanasomba na kuwa tayari kuuu ilimradi wapate mali bila kuzingatia kuwa wanaweza kukutwa na hatari baadaye ikiwa ni pamoja na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

#### **4.8.4 Dhamira ya Siri**

Baada ya kufanya uchambuzi wa data, mtafiti aligundua kuwa, kuna dhamira ya Siri. Mwandishi anaeleza kwamba, suala la siri ni jambo linalohitaji umakini mkubwa. Mwandishi ametueleza kuwa hakuna siri ya watu wawili. Amemtumia Mke wa Sikujua kuwa anafanya mapenzi ya siri na Pondamali, hatimaye tunaelezwa jinsi siri hiyo ilivyofichuka, kutoka kwa Pondamali mwenyewe. Pondamali alitoa siri ya uhusiano wa mapenzi kati yake na mke wa Sikujuwa. Baadae Sikujua alitoa siri ya mauaji aliyoyafanya kwa mke wake. Jambo ambalo lilipelekea Mke wa Sikujuwa kutoa siri ya mauaji kwa Mke wa Mzee Fundisha, kutokana na ukaribu waliokuwa nao hali iliyosababisha taarifa za mauaji kuzagaa na kuripotiwa katika vyombo vya sheria. Mwandishi anasema:

“...Maneno hayo yalimkasirisha sana marehemu. Hasira yake ilimfanya aseme maneno mengi, hadi kunitolea siri ya maudhi ambayo mimi sikuwa naifahamu. Aliniambia eti mke wangu kamfilisi! Kila siku alidai fedha na starehe zingine ambazo zilimfanya ashindwe kuweka fedha, na kwamba muda wake mwingi wa kazi alikuwa akiupoteza kwa mke wangu mimi niwapo kazini.” (uk:28).

Msanii anatutahadharisha kuwa tusiwe na tabia ya kujenga imani ya kuwa siri haitoki pale unapompa mtu mwengine. Anatueleza kuwa ni vyema tukapeana siri zihusuzo matendo mema na sio maovu. Kwa mfano, mwandishi anaeleza:

...Mke wa Sikujua alitoa siri ya mumewe kwa jirani yake, mke wa Mzee Fundisha...mke wa Fundisha alimpa siri hiyo mumewe. Mzee Fundisha alimdokeza Mzee Toboa siri hiyo siku ya jumapili, Toboa alipokwenda kunywa kahawa (uk.13).

Dhamira ya siri inlandana na jina la mhusika Sikujua kutokana na kitendo chake cha kutoa siri ya mauaji ya Pondamali kwa mke wake. Ni wazi kwamba Sikujua hakujua kabla kuwa, hakuna siri ya watu wawili.

#### **4.8.5 Dhamira ya Umuhimu wa Elimu**

Mtafiti baada ya kuchambua data aligundua kwamba, mwandishi wa *Kiu ya Haki*, Zainab M. Mwanga amesawiri dhamira ya umuhimu wa elimu kwa kuwatumia wahusika Fundisha na mke wake. Mwandishi anaona kuwa, hadi sasa jamii imekosa mwamko juu ya umuhimu wa kuwafichua waovu. Kwa mazingira haya, ipo haja kwa jamii kuelimishwa juu ya umuhimu wa kutoa taarifa mbali mbali, ili kuwafichua wahalifu na kuwapeleka katika vyombo vya sheria. Mwandishi anatuonesha namna ambavyo watu huwa na woga katika kutoa taarifa za wahalifu katika vyombo vya sheria kama ifuatavyo:

“Dunia ya siku hizi imekuwa ya hatari ndugu yangu. Nikikueleza wewe hapa, hutakosa kumweleza mkeo. Mkeo atamweleza shoga yake, na huyo shoga yake atayaendeleza kwa mashoga wengine.

Hatimaye mambo yatanigeukia mimi. Nitaitwa mfitini, mwongo au hata kushukiwa kuwa nimehusika na mauaji haya! (uk:6).

Licha ya kuficha ukweli, baadae Mzee Fundisha na Mke wa Fundisha wanaamua kukata jongoo kwa meno na kusimama kidete mahakamani, ili kutoa ushahidi wa mauaji yaliyotendeka. Kwa mfano, msanii anaeleza:

“Shahidi wa kwanza wa Mzee Toboa alikuwa Mke wa Fundisha. Aliingia kizimbani na kuanza kutoa maelezo yake. Aliieleza Mahakama kisa cha mauaji kama alivyokifahamu..... Alisema kuwa Sikujua alikula njama na Jaji Pwaguzi na Inspekta Pwagu kumsingizia MzeeToboa kuwa ndiye muuaji wa Pondamali. Sikujua alikuwa anawalipa Inspekta na Jaji shilingi laki moja ili wamuokowe kutoka katika janga la kuuu kwa makusudi. Aliongeza kuwa Inspekta Pwagu na Jaji Pwaguzi ndio waliomfundisha Sikujua maneno ya kusema mahakamani... kwa uthibitisho alitoa hati ya madai kati yake na Mke wa Sikujua” (uk:79).

Dhamira ya umuhimu wa elimu inlandana vyema na majina Fundisha na Mke wa Fundisha kutokana na jinsi wahusika hao walivyojitoa mhanga kutoa ushahidi wa kesi ya mauaji ya Pondamali huko Mahakamani. Wahusika hawa wanaifundisha jamii kwamba maovu yanaweza kudhibitiwa iwapo wanajamii watakubali kutoa siri za waovu wanazozipata katika vyombo vya sheria.

#### **4.8.6 Dhamira ya Ukiukwaji wa Sheria**

Baada ya kukusanya data na kuzichambua, mtafiti aligundua kuwa kuna dhamira ya uvunjaji wa sheria. Mwandishi anaona kwamba katika jamii nyingi sheria huwa hazifuatwi. Mwandishi anaona kwamba walio mstari wa mbele katika kuvunja sheria ni wale waliopewa dhamana ya kusimamia sheria. Mathalani, mwandishi anamtumia Jaji Pwaguzi anaevunja sheria kutokana na tamaa ya fedha. Kwa mfano, mwandishi anaeleza:

Mheshimiwa Jaji Pwaguzi na baadhi ya wananchi wengine walikuwa hawatii nguzo hii ya imani ya chama.....dhamiri yake ilikuwa haigutushwi tena na imani ya chama inayozuia kula rushwa. ( uk. 47)

Mtafiti amegundua kwamba, dhamira ya uvunjaji wa sheria imelandana na jina la mhusika Pwaguzi kutokana na jina hilo kuashiria kwenda kinyume na vile mambo yalivyo. Kama inavyoelezwa kwamba, mhusika huyo alikuwa tayari kuvunja sheria kwa kuchukua hongo, ili mradi apate fedha za matumizi. Hakujali wala hakuogopa sheria ya chama chake na serikali iliomuajiri isemayo kuwa rushwa ni adui wa haki.

#### **4.9 Hitimisho**

Uchambuzi wa data uliofanywa na mtafiti ulizingatia malengo mahsusi matatu ya utafiti huu. Imedhihirika wazi kuwa wahusika katika riwaya teuliwa wamewekwa katika matapo matatu, yaani wahusika wakuu, wasaidizi na wajenzi. Pia mbinu kadhaa zimejitokeza katika kuwalandanisha wahusika na kubeba dhamira mbali mbali.

## SURA YA TANO

### 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Utangulizi

Sura hii ni ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu muhtasari, sehemu ya pili inahusu hitimisho la utafiti huu na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

#### 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza wahusika wanavyolandana na majina yao kwa kutumia mifano kutoka katika riwaya ya *Kiu* na *Kiu ya Haki*. Katika utafiti huu tulichunguza kazi mbili za wasanii tofauti wa kifasihi, mwandishi wa riwaya ya *Kiu* (Mohamed S. Mohamed), na *Kiu ya Haki* (Zainab M. Mwanga), ambao wanatofautiana katika mazingira ya utunzi, ambapo Zainab M. Mwanga anatokea Tanzania Bara na Mohamed S. Mohamed anatokea Tanzania Visiwani. Lengo kuu la kufanya utafiti huu ni kuchunguza dhana zilizobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao katika riwaya ya *Kiu* na *Kiu ya Haki*. Aidha, Utafiti huu una malengo mahsusi matatu ambayo ni: Kubainisha wahusika wanaotumika katika riwaya ya *Kiu* na *Kiu ya Haki*, kuchambua mlandano wa majina ya wahusika katika riwaya teuliwa mbinu na kuchambua dhamira zinazobebwa na wahusika hao na jinsi zinavyolandana na riwaya teuliwa. Muhtasari wa matokeo hayo kulingana na malengo hayo ni kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Dhumuni la kwanza

Dhumuni la kwanza la utafiti huu lilikuwa; ni kubainisha wahusika waliotumika katika riwaya ya *Kiu* na *Kiu ya Haki*. Mtafiti aliweza kuchambua data zilizokusanywa katika riwaya teuliwa na kubaini kuwa, wahusika katika riwaya teuliwa wamegawika katika matapo makuu matatu. Wahusika wakuu, ambao ndio nguzo na muhimili wa kazi za fasihi. Wahusika hawa ndio waliobebeshwa dhamira kuu za waandishi. Wahusika wakuu katika riwaya ya *Kiu* ni Idi, Bahati na Mwinyi. Wakati katika riwaya ya *Kiu ya Haki*, wahusika wakuu waliojitokeza ni Mzee Toboa na Sikujua.

Aidha mtafiti aligundua kuwa, wapo wahusika wasaidiazi. Katika riwaya ya *Kiu*, wahusika wasaidizi ni Cheusi na Mwajuma. Pia, katika riwaya ya *Kiu ya Haki*, wahusika wasaidizi ni Pondamali, Mke wa Sikujua, Mzee Fundisha, Mama Fundisha na Inspekta Paukwa. Wahusika hawa wanashirikiana na wahusika wakuu katika kufanikisha dhamira za wasanii.

Pia, mtafiti amegundua kuwa, riwaya hizo zote mbili zimetumia wahusika wajenzi. Kundi kubwa la wahusika limeingia katika tapo hili. Wahusika wajenzi waliojitokeza katika riwaya ya *Kiu* ni Jaku, Kidawa, Tatu, Makame (mume wa Kidawa), Ali, Bi Mvita, Sihaba, Salama, Mwandawa, Riziki, Bintawa, Binti Songoro, Makame (mume wa Salama), Binti Jaku, Hadija, Baraka, Muuza samaki, Awadhi, Mcha, Rehema, na Rehema binti Mwinyi. Aidha, katika riwaya ya *Kiu ya Haki*, wahusika wajenzi wakiojitokeza ni Inspekta Pwagu, Inspekta Pwaguzi, Jaji Utakunywa, Somba, Killa, Kazamoyo, na Swalehe.



### 5.2.2 Dhumuni la Pili

Dhumuni la pili lilihusu kuchambua mlandano wa majina ya wahusika katika riwaya teuliwa. Mtafiti alikusanya data zinazohusu kipengele hicho na kugunduwa kwamba riwaya hizo zimetumia mbinu changamano. Baadhi ya mbinu zilizotumika katika kuwasawiri wahusika na majina yao ni pamoja na mbinu ya maelezi, mbinu ya kidrama, mbinu ya uzungumzi nafsi wa ndani, mbinu ya matumizi ya majina au majazi, mbinu ya ulinganuzi na usambamba na mbinu ya kuwatumia wahusika wengine. Aidha, mtafiti amegundua kwamba, majina ya wahusika huweza kusawiriwa kwa njia zaidi ya moja. Baada ya kuchambua data mtafiti aligundua jinsi wahusika walivyolandana na majina yao kwa kutumia mbinu za majazi au majina, uzungumzi nafsi wa ndani, kidrama, ulinganuzi na usambamba, kuwatumia wahusika wengine, na kimaelezi.

### 5.2.3 Dhumuni la Tatu

Dhumuni la tatu la utafiti huu lilihusu kuchambua dhamira zinazobebwa na wahusika hao na jinsi zinavyolandana na riwaya teuliwa. Baada ya mtafiti kukusanya data na kuzichambua, aligundua kuwa, kumejitokeza dhamira kadhaa ambazo zimejidhirisha kupitia wahusika na zinalandana na riwaya kama ifuatavyo:

Kwanza, mtafiti aligundua katika riwaya ya *Kiu* kuna dhamira ya mapenzi ambayo imejitokeza kupitia mhusika Bahati. Kama lilivyo jina la mhusika Bahati, Bahati anapata Bahati ya kupendwa na Mzee Mwanyi, mzee ambaye ni tajiri na kupata fursa ya kupata pesa taslimu na Bahati ya kununuliwa nyumba na Mzee Mwinyi. Aidha Bahati anapata mapenzi ya kupendwa na Idi. Hatimaye anafunga ndoa na Idi.

Vile vile, Bahati anapata Bahati yakupata mapenzi ya kweli ya mama yake (Cheusi).

Pia, mtafiti aligundua kuna dhamira ya ndoa kupitia mhusika Jaku na Cheusi. Neno jaku katika lahaja ya Kipemba lina maana ya; udanganyifu, kwenda kinyume au kufanya mambo sivyo. Mhusika Jaku mara baada ya ndoa yake anamuachia Cheusi ulezi wa mtoto wao, huku akikimbilia Kongo. Aidha, mhusika Cheusi analandana na jina lake na dhamira hii ya ndoa kwasabau, ndoa yake ilimuingiza katika kiza cha ukiwa, simanzi na majonzi.

Aidha, mtafiti aligundua kuwepo kwa dhamira ya umaskini. Mwandishi alimtumia mhusika Cheusi, akiwa anaishi katika nyumba ndogo, kongwe, chakavu na anaishi katika maisha ya kijungu jiko. Anajaribu kutaka kujinasua na hali hiyo ya umaskini, lakini, anaishia kudumu na hali hiyo. Jina Cheusi ni kielelezo cha Waafrika wengi ambao wamejikuta njia panda na katika kiza totoro kutokana na hali ya umasikini unaoongezeka kila uchao.

Pia, mtafiti aligundua dhamira ya utamaduni wa Mwafrika kupitia jina la mhusika Bi Mvita. Daima Bi Mvita amekuwa akipiga vita tamaduni za kigeni zilizo likumba bara la Afrika zenye muelekeo wa kupotosha na kufifisha utamaduni wa asili wa Mwafrika. Kwa hali hiyo, anaamua kusimamia harusi ya Bahati akisisitiza suala la unyago. Jambo hili ndilo lililopelekea mhusika huyo kupewa jina Bi Mvita.

Vile vile, mtafiti amegundua uwepo wa dhamira ya ulevi kupitia mhusika Idi. Dhamira hii inlandana na jina la Idi kutokana na desturi yake aliyokuwa nayo ya

kunywa ulevi kupindukia. Idi ni moja kati ya siku kuu za Kiislamu. Baadhi ya watu hutumia fedha kwa kula vyakula vizuri, kuvaa nguo mpya kushiriki katika ngoma na wengine kunywa ulevi wa kupindukia. Hivyo, mhusika Idi amelandana na dhamira ya ulevi kutokana na tabia ya kunywa kupindukia. Pia, jina hilo limelandana na dhamira ya ulevi kutokana na kitendo chake cha kutotokwa na ulevi kila wakati, kama wafanyavyo watu wengi wenye kipato siku hiyo ya Idi.

Aidha, mtafiti amegundua kuwa, katika riwaya ya *Kiu* kunapatikana dhamira ya ujirani mwema kupitia kwa mhusika Binti Songoro. Jina Songoro limelandana na dhamira ya ujirani mwema. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010), neno 'songoro' lina maana ya samaki mwenye rangi ya fedha. Samaki huyo huwa na thamini na mvuto kwa watu. Hivyo, Binti Songoro alivutia majirani wengi kwa wema na ukarimu wake. Tumelezwa kuwa, alimuazima nyumba Cheusi, ili wageni wanaokuja katika shughuli ya harusi ya Bahati wafikie.

Kwa upande wa riwa ya *Kiu ya Haki*, mtafiti alifanya uchambuzi wa data na kugunduwa kuwa, majina ya wahusika yamelandana na dhamira kwa baadhi ya wahusika. Majina yaliyolandana na dhamira ni haya yafuatayo:

Kwanza, mtafiti aligundua kuwa, kuna dharmo ya Siri inayojitokeza kwa mhusika Sikujua na Mke wake. Dhamira hii imelandana na majina ya wahusika hao kutokana na kutotambua kuwa, hakuna siri ya watu wawili. Hali hiyo, ndio iliyo pelekea siri ya mauaji ya Pondamali kuzagaa, baada ya mke wa Sikujua kutoa siri kwa mke wa Mzee Fundisha.

Pia, mtafiti amegundua kuwa, kuna dhamira ya ujambazi kupitia kwa wahusika Killa, Somba na Kazamoyo. Majina hayo yote yanalandana na dhamira ya ujambazi. Kwa mfano, jina la “Killa” limetoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza likiwa na maana ya muaji kama anavyoonekana mhusika huyo akiwateka nyara Pondamali na Sikujua. Pia, jina la Somba lina maana ya kuchukuwa vitu kwa pamoja. Kwa hivyo, Somba linawiana na dhamira ya ujambazi kutokana na mhusika huyo kusomba pesa za Sikujua na saa ya mkononi. Aidha, Kazamoyo ni jina la jambazi aliyekaza moyo wake na kuzungumza ukweli pale alipohojiwa na Jaji Mahakamani na kufanya vitendo vya ujambazi hasa wakati wa usiku.

Vile vile, mtafiti aligundua kuna dhamira ya rushwa kupitia kwa wahusika Pwagu na Pwaguzi. Kwa mujibu wa BAKIZA (2010), majina Pwagu na Pwaguzi yana maana ya mtu ambaye kauli zake si za kutegemewa na kutokuwa na busara kutokana na tabia yake. Majina hayo, yanalandana na dhamira ya rushwa kutokana na wahusika hao kuchukua rushwa kutoka kwa Sikujua ili wamsaidie katika kesi inayomkabili ya mauaji ya Pondamali pale Mahakamani wakiwa wao kama ni majaji wa kesi hiyo.

Pia, mtafiti aligundua kuwa, kumejitokeza dhamira ya uvunjaji wa sheria. Dhamira hii imelandana na majina ya wahusika Pwagu na Pwaguzi. Wahusika hao wanadhamana katika vyombo vya kusimamia sheria. Hata hivyo, wanasahau wajibu wao na wanavunja sheria kwa kuchukua hongo, ili kuwasaidia wahalifu.

Vile vile, mtafiti aligundua kuwa, kuna dhamira ya umuhimu wa elimu. Dhamira ya umuhimu wa elimu imelandana na majina ya Mzee Fundisha na Mama Fundisha. Wahusika hao wametumiwa na mwandishi kutoa fundisho kwa jamii juu ya umuhimu wa kuwafichua wahalifu, ili kupelekwa katika vyombo vya sheria na hatimae sheria kuchukua mkondo wake.

### **5.3 Mapendekezo ya Utafiti**

Mtafiti amechunguza dhana zinazobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao. Mtafiti anaamini kwamba ametoa mchango mkubwa katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili pamoja na kuwasaidia waandishi, wanafunzi, walimu na watafiti wengine jinsi wahusika wanavyotumiwa na msanii katika kazi za fasihi. Aidha, mtafiti anaamini kwamba ameziba pengo la kitaaluma lililokuwepo kuhusiana na jinsi wahusika wa riwaya ya *Kiu* na *Kiu ya Haki* wanavyolandana na majina yao pamoja na dhamira walizobebeshwa. Hata hivyo, hakuna mtafiti yoyote anayeweza kudai kuwa amefanya utafiti na kukamilisha kila kitu. Kutokana na wazo hilo, mtafiti anapendekeza mambo yafuatayo:

#### **5.3.1 Kwa Watafiti Wengine**

Utafiti mwengine ufanyike, ili kuchunguza vipengele vyengine vya fani katika riwaya hizo teuliwa. Vipengele kama vile lugha, mandhari, muundo na mtindo vinaweza kutafitiwa.

#### **5.3.2 Kwa Watunzi wa Fasihi**

Utafiti unaweza kufanyika kulinganisha dhamira za mwandishi wa *Kiu* na zile za mwandishi wa *Kiu ya Haki* kwa kuzingatia mandhari wanayotoka. Aidha, utafiti

unaweza kufanyika kuchunguza Ufasihi Simulizi katika riwaya ya *Kiu na Kiu ya Haki*.

### **5.3.3 Kwa serikali**

Serikali itilie mkazo tafiti katika masuala yanayohusu taaluma ya fasihi, ili kulinda na kueneza tamaduni za jamii yetu, kwa kuendelea kuwaunga mkono wote wanajishughulisha na kazi za utafiti.

**MAREJELEO**

- BAKIZA (2010), *“Kamusi la Kiswahili Fasaha”*, Oxford University Press, Nairobi
- Enon, J. C. (1998), *“Educational Research, Statistics and Measurement”*,  
Department of Distance Education: Institute of Adult and Continuing  
Education Makerere University Kampala.
- Gibe, P. (1975), Uhakiki wa Tamthilia ya Mwanzo wa Tufani,  
katika *“Mulika Na. 15 uk:29-30”*, Taasisi ya Kisahili  
Chuo cha Dar es salaam.
- Haji, A. A (1982), *“Misingi ya Nadharia ya Fasihi”*, Sweden by Berlings, Arlov
- Kenan, S. R. (2007), *“Narrative Finction”*, London and New York: Routledge.
- Keys, B. (1989), Four Faces of Fully Function Middle Manger; California  
Management Review; Vol. xxiv. No. 4 pp. 59-67.
- Kezilahabi, E. (1990), *“Nagona”*, Printing Services Ltd, Nairobi
- Kezilahabi, E. (1974), *“Kichwa Maji”*, East Africa Publishing House, Dar es Salam
- Kothari, D. (1990), *“Research Methodology: Methods and Techniques”*, New  
Delhi, New Age International (P), Limited
- Kyando, L. (2012), Majina Sadfa ya Wahusika Katika Kusadikika na Kichwamaji:  
katika *“Mulika Na.31uk:37-50”*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo  
Kikuu cha Dar es salaam
- Lihamba, A. (1980), *“Hawala ya Fedha”*, Tanzania Publshing House. Dar es  
Salam.
- Lothe, J. (2000), *“Narrative in Fiction and Film”*, Oxford University Press
- Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2006), *“Nadharia ya Fasihi”*, The General  
Booksellers LTD, Dar es salaam.

- Madumulla, J. S. (2009). *“Riwaya ya Kiswahili: Nadharia Historia na Misingi ya Uchambuzi”*, Phoenix Publishers Limited, Nairobi.
- Manzi, Z. M. (2007), *“Civics for Secondary School(2<sup>nd</sup> ed)”*, BPL Publishers, Dar es Salam.
- Masoud, S. M. A. (2013). *“Maudhui na Fani katika Tamthilia za Kiswahili: Mashetani na Kivuli Kinaishi. Tasnifu ya Uzamivu”*, Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania.
- Mbogo, E. (2010), *“Siri za Maisha”*, E & D Publishing Limited, Dar es Salam.
- Mbogo, E. (2010), *“Watoto wa Mamantilie”*, Heko Publishers Limited, Dar es Salam.
- Mohamed, S. M. (1990), *“Kivuli Kinaishi”*, Oxford University Press, Dar es Salam.
- Mohamed, S. M. (1975), *“Kiu”*, Colourprint Limited, Nairobi.
- Mshindo, H. B. na Snoxall, R. A. (2002), *“Kamusi ya Kiingereza- Kiswahili”*, Oxford University Press, London .
- Mtobwa, R. N. (1987), *“Zawadi ya Ushindi”*, Heko Publishers Limited, Dar es Salam.
- Mtobwa, R. N. (2002), *“Pesa Zako Zinanuka”*, Heko Publishers Ltd, Dar es salaam.
- Mvungi, T. A. K. (1988), *“Kiswahili Sekondari”*, Taasisi ya Elimu Tanzania, Dar es Salam.
- Mwakamele, I. (2013), *“Introduction to Educational Research”*, The Open University of Tanzania.
- Mwanga, M. Z. (2004), *“Kiu ya Haki”*, Ruvu Publishers Ltd, Dar es salaam.



- Newman, W. L. na Wenzake, (2006), *Social Research*. Sixth Edition, Boston: Pearson.
- Ngemea, R. A. na Kahigi, K. K. (1975), “*Mwanzo wa Tufani*”, Tanzania Publishing House LTD, Dar es salaam.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1998), “*Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*”, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- Omari, S. (2011), *The Role of Pseudonyms in Bongo Flewa Music*. 14 February 2013, www. Ifeas. Uni-mainze.de/SwaFo.
- Pauline, R. (2003). “*Kidagaa Kimeingia Mchanga*”. Tasnifu ya MA Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Robert, S. (1952), “*Adili na Nduguze*”, Macmillan Education Limited, London.
- Robert, S. (2008), “*Kufikirika*”, Mkuki na Nyota Publishers Limited, Dar es Salam.
- Robert, S. (1981), “*Kusadikika*”, Nelson East Afrika, Nairobi.
- Ruhumbika, G. (1995), “*Miradibubu Ya Wazalendo*”, Tanzania Publishing House Limited, Dar es salaam.
- Sengo, S. Y. M. na Kiango, S. K, (2012), “*Hisia Zetu*”, Taasisi Ya Taaluma za Kiswahili:Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Sengo, S. Y. M. (2009), “*Sengo na Fasihi za Kinchi*”, Aera Kiswahili Researched Products, Dar es salaam.
- Senkoro, F. E. K. (1982), “*Fasihi*”, Press and Publicity Centre, Dar es Salam.
- Senyamanza, C. A. (2010), “*Misingi ya Kazi za Kubuni: Nadharia Mbinu na Mifano ya kazi Bunilizi*”, Karljamer Print Technology, Dar es Salam.
- Shafi, A. S. (1994), “*Kul*”i, Tanzania Publishing House, Dar es salaam.
- Shafi, A. S. (1999), “*Vuta Nkuvute*”, Mkuki na Nyota Publishers, Dar es salaam.

- Suweid, A. A. (2013), "*Usawiri wa Ujinsia katika Filamu: Uchunguzi wa matumizi ya Lugha katika filamu za Steven Kanumba.*" Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Topan, F. (1971), "*Mfalme Juha*", Oxford ress, Dar es Salam.
- TUKI, (1998), "*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*", Oxford University Press, Kenya.
- Wafula, R, M. na Njogu, K. (2007), "*Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*", Sai Industries Limited, Nairobi.
- Wamitila, W. K. (2002), "*Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*", Phoenix Publishers LTD, Nairobi.